ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 4 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuruni sana kwa kujumuika kwenye shughuli zetu za asubuhi ya leo mapema saa 3.00 barabara, inafurahisha mbele ya macho ya wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe kama kawaida leo tunao wageni kutoka Kenya, chombo chetu kinapata bahati ya kutembelewa na wageni mbali mbali na leo hii tunao ndugu zetu Wabunge wenzetu kutoka *County* ya Kwale - Kenya. Wageni hao watakuwa hapa Zanzibar kwa ziara ya siku 5 na ujumbe huo wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na watendaji wa Bunge hilo la *County* ya Kwale, wanaongozwa na Mhe. Spika wa *County* hii ya Kwale Mhe. Sami Nyamawi Vuwa, amefuatana na Wabunge wake 20 kutoka *County* hiyo pamoja na watendaji wa *County* hiyo 4. Naomba basi Waheshimiwa wote wakiongozwa na Mhe. Spika, wanyanyuke ili kusalimia na Waheshimiwa Wajumbe, karibuni sana (*Makofi*).

Mhe. Spika Sami na ujumbe wako tunawakaribisha sana katika shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi muone ndugu zenu tunafanya nini kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar, karibuni sana (Makofi).

Wageni wengine ni mtiririko wa vijana wetu ambao sehemu yake walikuja jana walikuja walikuwa 50 ambao walifuatana na walimu wao, hao ni wanafunzi kutoka Mwanakwerekwe F, wanafunzi wenye ulemavu, hii ni *group* nyengine pia wale wa jana kwa sababu hii skuli ni kubwa kidogo, ni *group* nyengine ambayo nao wamekuja kuwasalimia wazee na kuona wanafanya nini kwa ajili yao. Niombe basi walimu pamoja na vijana hao wasimame kusalimiana na Waheshimiwa Wajumbe (*Makofi*).

Walimu pamoja na vijana wetu karibuni sana muone shughuli za wazee wenu wanafanya nini kwa ajili yenu. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya ya mwaka 2013/14. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hassan Hamad Omar: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa niaba yako na kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake wa Ustawi wa Jamii kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2013/14. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam.145

Huduma Rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikijenga majengo ya kisasa lakini huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu zimekuwa hazizingatiwi na kusababisha usumbufu mkubwa wa kupata huduma kwa watu wa aina hiyo.

(a) Kwa nini Serikali imekuwa ikirudia makosa kujenga majengo bila ya kuzingatia huduma hizo kama ilivyotokea katika majengo ya Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) huko Tunguu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(b) Sababu gani za msingi wakandarasi wanashindwa kuzingatia umuhimu wa huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu katika michoro yao ya ujenzi

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 145, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, mkataba wa kimataifa wa haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu katika ibara ya 9 unaeleza kwamba nchi zilizoridhia mkataba huu zitachukua hatua zinazofaa kuwawezesha watu wenye ulemavu kuishi kwa kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maisha kwa misingi sawa na wenzao wasiokuwa na ulemavu kwa kuondoa vikwazo na vizuizi vya

kufikia vyombo vya usafiri, barabara na majengo ya huduma za jamii na sehemu za kazi mijini na vijijini, bahari na mawasiliano na huduma nyengine.

Mhe. Spika, pia katika sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya haki na fursa sawa ya mwaka 2006 katika ibara ya 12 kifungu kidogo cha tatu kinaeleza kwamba wasanifu wa majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengineo wanaohusika na usanifu na ujenzi wa majengo watalazimika kuzingatia upatikanaji wa vifaa wakati wanaanza taratibu za kuandaa michoro na kuhakikisha kwamba majengo yote mapya yanaendelea sambamba na michoro yenye lengo la kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika**,** sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 145 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imekuwa ikisisitiza uwekaji wa mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu ili kuyafikia mazingira ya aina zote na wao kujumuika katika jamii kama watu wasio na ulemavu.

   Mhe. Spika**,** kuondoa vikwazo kwa watu wenye ulemavu ni kujenga maisha bora yasiyo na unyanyapaa na udhalilishaji, kwa mantiki hii Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Tume ya Marekebisho ya Sheria inaendelea kuifanyia mapitio Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2006 ili iende sambamba na mkataba wa kimataifa wa haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu na mkataba wa kimataifa wa haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.

b) Mhe. Spika**,** mara nyingi wakandarasi hukimbia gharama kubwa ya ununuzi wa vifaa vya watu wenye ulemavu na kuviweka katika majengo yanayojengwa, aidha wakandarasi huzingatia zaidi michoro ya awali pamoja na mikataba yao ya ujenzi, ikitokea katika michoro yao ya awali haikuonesha kuwepo kwa mazingira rafiki ya watu wenye ulemavu huwa ni wagumu wa kuingiza vifaa hivyo.

c) Mhe. Spika, kupitia Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu juhudi za makusudi zimechukuliwa ili kuwakumbusha mawizara na taasisi za umma ikiwemo Baraza la Wawakilishi, hata hivyo bado nguvu za pamoja zinahitajika kuona mabadiliko hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini inaonekana haioneshi nia ya kuondosha tatizo hili, ukizingatia majengo ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) na Baraza la Wawakilishi ni majuzi tu. Hivi juzi Mkurugenzi wa Walemavu Bi. Abeda, alivyokuja kusikiliza hotuba yako hapa alipata shida kwenda juu na matokeo yake akaishia chini. Je, unalizungumziaje suala hili na pili kwa kuwa sheria ya watu wenye ulemavu tangu kupitishwa hadi sasa kanuni hazijatungwa ni lini zitatungwa kanuni hizo.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana, kwa idhini yako Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo.

Mhe. Jaku, naomba awe na subra na kuona kwamba jitihada za makusudi zinachukuliwa na ofisi yetu kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu kuona kwamba hali inabadilika. Ni kweli Baraza hili la Wawakilishi wakati linajengwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu ilifika na iliwasiliana na waliochora michoro, lakini kama nilivyoeleza awali kwamba wakandarasi wanakua vigumu kuweka mabadiliko katika michoro yao ya awali ambayo tayari wanakuwa wametiliana mikataba na wale waliowapa kujenga majengo hayo. Kwa hivyo tatizo hili ni bora lilaumiwe Baraza la Wawakilishi wenyewe kuliko Idara ya Watu Wenye Ulemavu ambayo imefanya jitihada zote.

Lakini Mhe. Spika, naomba akubaliane na mimi kwamba jitihada hizi zimeanza kuzaa matunda. Hivi karibuni katika majengo yetu mapya naweza kutoa mfano hapa tuna jengo letu la Kodi ya Mapato (*ZRB)* tayari lina miundo mbinu ya watu wenye ulemavu kuweza kulifikia lakini jengo letu vile vile la uhamiaji ambalo nalo ni jipya tumesimamia na kuona kwamba lina miundo mbinu ya aina hiyo, lakini hata skuli hii inayojengwa hapa Kiembe Samaki nalo tumesimamia kuona kwamba ina miundo mbinu hiyo.

Mhe. Spika, naomba kumueleza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba ni kweli kanuni za sheria hii ya mwaka 2006 ni za muda mrefu na hazijatungwa, lakini sheria hii ni ya mwaka 2006, mkataba wa kimataifa wa ku-*recognise* haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu Mhe. Spika, ni wa mwaka 2007. Kwa hivyo kwanza ukiangalia utaona kwamba sheria hii ina mapungufu makubwa na haiendani sambamba na mkataba huu wa kimataifa ambao Tanzania imeridhia. Hiyo sheria yetu kwanza ni lazima tuifanyie marekebisho ili iweze kuendana sambamba na mkataba huu wa kimataifa na baadae kutengeneza kanuni. Hivi sasa ofisi pia utakuta kwamba sheria hii ilivyotengenezwa hakukuwa na sera ya watu wenye ulemavu. Ofisi yangu imo katika mchakato na mtaona katika maelezo ya bajeti ambayo nimeyatoa Idara hii

inashughulikia kuweza kumalizia sera za watu wenye ulemavu ili sheria ambayo itakidhi haja iweze kutungwa ili kuweza kuwachukulia hatua zinazofaa wale wote watakaokiuka maagizo ambayo yatatolewa ndani ya sheria hii.

Mhe. Farida Amour Mohammed:Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mlemavu ana haki sawa sawa na binadamu yeyote kwa sababu na wao wameumbwa kama tulivyoumbwa sisi na sote ni walemavu watarajiwa, na kwa kuwa kitabu tulichogaiwa hivi karibuni kinaonesha jengo kubwa na zuri la Wizara ya Katiba na Sheria. Je Mhe. Waziri, una uhakika gani kama huduma za walemavu pale zimezingatiwa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mjumbe, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Jengo lile namuhakikishia kwamba shughuli zote zinazohusiana na walemavu zimeingizwa katika jengo hilo. Kwa hivyo inshallah kutakuwa hakuna matatizo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru na nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba haijakuwa na sheria mahsusi ya kusimamia jambo hilo na kwa kuwa walemavu wetu sasa wanaendelea kusoma kwa kazi na wanahitaji huduma za kupatiwa na serikali. Je, katika yale majengo ambayo hayajazingatia viwango vya kilemavu, serikali itaamua kuweka huduma maalumu ili kuwaongoza walemavu ili wapate haki yao.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako tena naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hija Hassan Hija na Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kiwani kama hivyo ifuatavyo.

Mhe. Spika, nimeeleza kwamba mkataba huu wa kimataifa unaozingatia haki na fursa sawa za watu wenye ulemavu ni wa mwaka 2007. Majengo mengi ambayo yanatoa huduma kwa jamii yalijengwa bila ya kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Ofisi yangu inachofanya hivi sasa kwanza ni kukaa na kuzipitia taasisi zote hizi ambazo zinatoa huduma kwa wananchi kuweza kuona ni njia gani wanaweza kufanya angalau ya kuweza kujenga miundo mbinu ya aina *ramp* ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kufikia huduma hizo, na mfano wa hiyo ni *ramp* iliyoko katika Hospitali ya Wazazi ya Mwembeladu. Ni imani yangu kwamba taasisi hizi zinazotoa huduma kwa

jamii zitakuwa sambamba na maagizo yetu kuweza kuona kwamba zinafanyiwa marekebisho ili ziweze kufikiwa.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Spika, kuanzia sasa ni kutaka kuona kwamba hakuna jengo lolote ambalo litajengwa kwa ajili ya matumizi ya kutoa huduma kwa jamii litajengwa bila ya kuzingatia miundo mbinu hii itakayowawezesha watu wenye ulemavu kuweza kuifikia.

Nam. 78

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Chuo cha Kiislamu Mazizini ni moja kati ya Vyuo vinavyomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kinachotoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Stashahada (*Diploma*). Kwa kuwa zipo taarifa kuwa ardhi ya chuo hicho tayari imevamiwa na wananchi pamoja na wafanyabiashara kwa ajili ya biashara pamoja na shughuli nyengine.

(a) Je, Serikali inayo habari hiyo.

(b) Kwa kuwa Chuo hicho hakina uzio, jambo linalohatarisha usalama wa chuo. Je, ni lini Serikali itajenga uzio huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 78 lenye sehemu (a), na (b) Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi:-

Wizara inalielewa eneo lote la Chuo cha Kiislamu, Mazizini. Eneo hilo limepimwa na lina hati miliki yake. Pia, ni kweli kuwa katika eneo la mbele la Chuo cha Kiislamu Mazizini, mkabala na eneo linalojengwa skuli mpya ya sekondari wapo wafanyabiashara ndogo ndogo, wanaoendesha shughuli zao ndani ya eneo la chuo. Wafanyabiashara hao wanaendesha shughuli hizo kwa mikataba maalumu iliyotiwa saini na Chuo. Eneo jengine ni eneo lilofanywa kuwekea na kuuza magari. Ingawa eneo hilo limejitenga na Chuo na lipo baada ya kituo cha kuuzia mafuta, lina mgogoro kati ya mmiliki wa yadi hiyo na Wizara. Mgogoro huo unatokana na mmiliki wa yadi kudai kuwa na hati miliki ya eneo hilo. Maeneo mengine yaliyobakia yako salama na Wizara inayalinda kwa nguvu zake zote. Baada ya maelezo hayo napenda kumjbu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Nakiri kuwa Serikali inalielewa suala hilo na inalifanyia kazi.

b) Serikali ina azma ya kujenga uzio kuzunguka vyuo vya Kiislamu Mazizini na Micheweni. Hata hivyo kutokana na uhaba wa fedha, juhudi zaidi zimeelekezwa katika kujenga uzio katika Chuo cha Kiislamu Micheweni ambapo tayari kazi za ujenzi zimeshaanza rasmi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa kuweza kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa amekiri kwamba huku pembezoni kuna wafanyabiashara ndogo ndogo ambao wamekaa katika maeneo yale kwa mikataba maalumu na kwa kuwa inaonekana kuna biashara ndani ya ardhi ile ambayo wamesema wameshapata hati miliki ambayo inafanyiwa biashara kubwa kwa mfano ya *Petrol Station* pamoja na hii ardhi aliyoko Sheikh Al-Youssuf nayo tunasikia ni sehemu vile vile ya ardhi ya Chuo. Je, hii sehemu aliojenga nyumba Al-Youssuf pamoja na hii *Petrol Station* imetolewa kwahala kama zawadi au ni uzembe tu wa Wizara imewaachia waje wakae pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi, swalia lake la nyongeza.

Mhe. Spika, ni kweli kama alivyozungumza au kama alivyouliza kama kuna sehemu ile aliyejenga Mzee wetu Al-Youssuf ni eneo la Chuo pia kuna ile sehemu ya *Shell*, kuna ile sehemu ambayo inawekwa magari kweli ilikuwa ni sehemu ya Chuo lakini ninalotaka kumuhakikishia kama sehemu hizo na ndio pale nilipozungumza kwenye suala langu mama kama hapa kwenye eneo la magari, hawa tuna mgogoro nao kwa sababu hawana kibali cha kujenga pale eneo, lakini hawa wengine wote wenye Shell, Mzee Al-Youssuf wana hati zao miliki, wako pale na *ZANTEL* wana hati miliki ambao wamepewa na serikali. Kwa hivyo mimi sitaki niseme wala Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu wasidhani kama ni uzembe wa Wizara, si uzembe wamepewa na Serikali kwa sababu kama *ZANTEL* tunajua kama Serikali ina ubia. Hivyo tunapata cho chote kutoka *ZANTEL* kutokana na *shares* ambazo tunazo. Kwa hivyo si vibaya Serikali kuchukua sehemu ambayo inataka kutumiwa kwa kazi nyengine.

Mhe. Spika, na wale wafanyabiashara wengine wadogo wadogo wapo pale kwa mkataba wameekwa kwa muda na wanalipia Chuoni karibu 280,000/=

inapatikana pale, wanapewa Chuo kutokana na zile biashara zao ndogo ndogo wanazozifanya.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad:Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza. Kwa kuwa walimu wanaomaliza elimu ya *Diploma* ya Dini wanapata shida sana kuajiriwa, ikiwa ni hivyo kuna sababu yoyote ya kuendelea kulipia fedha wakati mahitaji hayako tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sidhani kama nimemfahamu.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, kwa kuwa wanaomaliza elimu *diploma* ya elimu ya juu wanapata shida sana kuajiriwa, ikiwa ni hivyo kuna sababu yoyote ya kuendelea kulipia fedha za walipa kodi wakati mahitaji hayapatikani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, sidhani kama hili lilikuwa ndio limo katika *issue* hii ya msingi lakini naomba nimsaidie kama ambavyo alitaka. Mhe. Spika, nia ya Wizara ni kusomesha wananchi wake wote kila mwenye haja ya kupata elimu. Suala la kuajiriwa ni suala jengine na sio kama hatuajiri wala hatuendelei kusomesha, lakini tunatizama na mahitaji ya nchi, mahitaji hivi sasa ambayo tunayo katika Wizara ya Elimu, si walimu wa Dini ya Kiarabu, mahitaji tuliyonayo zaidi ni walimu wa sayansi na ndio ambayo tunaajiri. Itakapofikia kipindi cha kuhitaji walimu wa Dini basi Wizara haitosita kufanya hivyo. Nakushukuru sana kufanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora:Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu majibu ya nyongeza na kuongeza kutoa ufafanuzi kuhusu swali la Mhe. Mwakilishi.

Nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ameyatoa lakini nataka niseme kwamba serikali adhma yake kubwa ya kuwasomesha vijana wake na wananchi wake, kwanza ni kuwapa taaluma ili waweze kuwa na uelewa wa shughuli ambazo zinaweza zikawasaidia katika maisha yao ya baadae, na Serikali ina jukumu la kuwasomesha ili waweze kuajiriwa ama kujiajiri. Kwa hiyo sio kila mtu au kila kijana anayesomeshwa na Serikali kuwa inawajibika lazima imuajiri, kama nafasi zipo Serikali inamuajiri lakini kama nafasi hazipo na anayeweza kujiajiri kwenye sekta binafsi anaweza

akaajiriwa kwenye binafsi, lakini vile vile kama ameshapata elimu na anaweza kujiajiri anaweza akajiajiri mwenyewe. Kwa hiyo isionekane kwamba kila anayesomeshwa na Serikali, hivyo jukumu la Serikali ni kumuajiri kila mtu ambaye anasomeshwa. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo lenye sehemu (a) na (b) kuhusiana na suala lilioko mbele yetu.

Kwa kuwa Chuo cha Kiislamu Zanzibar kiliasisiwa na mwana mapinduzi wa Zanzibar Mhe. Abeid Amani Karume kwa lengo la kukifanya Chuo hichi kuwa Chuo Kikuu cha Kiislamu Zanzibar, na kwa kuwa bango la kwanza lililopachikwa pale mwaka 1972 kilipoasisiwa Chuo kichi lilitangaza Chuo Kikuu cha Kiislamu Zanzibar, na kwa kuwa juhudi hizi hazikuendelezwa Chuo kile kimebakia mpaka kimekuwa Chuo cha kawaida tu haikufikilia ile azma ya mwana mapinduzi. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kukifanya Chuo kile kuwa Kikuu.

Jengine Chuo cha Kiislamu Micheweni, katika utaratibu wa kujenga uzio kuna sehemu ina mgogoro kati ya wazee wa Kiuyu Micheweni na wizara kuliendeleza suala la kujenga uzio. Je, suala lile limefikia wapi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama alivyozungumza Mhe. Mjumbe ni kweli kuwa nia ya Muasisi wetu wa nchi hii ni kukifanya chuo kile kiwe chuo kikuu. Naomba nijuilishe Baraza lako tukufu kwamba bado azma hiyo ipo, lakini chuo ili kiwe chuo kikuu kuna mahitaji yake ya lazima ambayo yanahitajika yawepo. Kwa kufahamu hilo Mhe. Spika, Wizara ya Elimu hivi sasa ina mpango mkubwa na Serikali ya Oman kukitanua chuo kile kuwa ni kituo cha Kiislamu kwa kujenga kwanza Msikiti mkubwa, ukumbi wa mkutano na madarasa, *computer laboratory* na maabara ya lugha.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kufikiwa basi nina hakika muda utakuwa si mrefu tutakigeuza chuo kile na kuwa ni Chuo Kikuu cha Kiislamu. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza watustahamilie kwa muda mdogo tu kwa hili, nia ipo kabisa na tayari tumefikia makubaliano mazuri na wenzetu Serikali ya Oman.

Pili kuhusu Chuo chetu cha Micheweni. Ni kweli Mhe. Spika, kama katika kujenga ukuta pale kuna mgogoro ambao una wananchi wa Kiuyu, Micheweni wanadai kama sehemu ile ni yao. Mimi binafsi nishakwenda karibu mara tatu nishazungumza na watu mbali mbali na tayari tumefikia

makubaliano. Nataka nijuilishe Baraza lako tukufu kwamba ujenzi ule hivi sasa unaendelea kwa kasi karibuni nilikuweko na tumefikia karibu mita 300 za uzio kujenga. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Nam. 129

Kufanyiwa Matengenezo "*Round About*" ya Michenzani

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la mzunguko wa barabara ya *round about* ya Michenzani haiko katika hali nzuri mbali na juhudi kubwa za Manispaa ya Zanzibar kuweka mtambo wa kurusha maji katika '*round about*' hiyo, lakini mazingira yake bado si mazuri.

Je, kuna mpango gani wa kuifanyia miundombinu mipya *'round about'* ya Michenzani ili ilete haiba na mandhari nzuri ya eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake Nam. 129 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakiri kwamba eneo la mzunguko wa barabara ya *round about* ya Michenzani linahitaji marekebisho zaidi ili irejee katika hadhi yake ya zamani. Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na wataalamu mbali mbali wa Idara ya Mipango Miji, Idara ya Mazingira na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara walishirikiana na kwa mafanikio makubwa kuweza kurejesha tena ile miundombinu ya kurusha maji pamoja na taa za rangi ambayo ilikuwa na mandhari nzuri ya kuvutia kwa wananchi wanaoishi Michenzani, wapita njia na wageni wanaotembelea Zanziar kwa ujumla.

Mhe. Spika, hivi sasa Baraza la Manispaa wanajiandaa kuweka mnara wa aina yake tena wenye urembo hasa wakati huu tukijiandaa kwa sherehe za kuazimisha miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanziabar. Tayari tumeshapokea mapendekezo kadhaa ya michoro na tutakaa pamoja na wadau wote ili tupate mchoro mmoja mzuri ambao tutauweka pale na kuwa wa kudumu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, *round about* ya Michenzani ipo katikati ya mji wa Zanzibar, na majumba ya Michenzani ni majumba ambayo

yamejengwa na muasisi wa nchi hii, mzee wetu Mzee Abeid Amani Karume. Je, haoni kwamba ipo haja ya kujenga mnara na picha ya kumbukumbu ya Mzee wetu ili iwe kumbukumbu kwa vizazi vijavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mzee Abeid Amani Karume alikuwa Michenzani kama ndio *centre* yake, na ile mipango aliyokuwanayo *visión* ya kuifanya Michenzani kama *centre* ya mji mpya wa Zanzibar tumeiona. Kama nilivyosema ile *round about* yote hasa ilikuwa ni ubunifu wake kwamba tuweke kitu pale *fountain* ya kurusha maji watu wafurahi. Kwa hivyo, nakubaliana na yeye kwamba ile *vision* yake aliyokuwanayo Mzee Karume tutaiendeleza na kwa kiwango fulani tukiri kwamba kweli kulikuwa na matatizo pale mwanzo kama alivyosema miundombinu ile ya maji ilikufa lakini sasa tumedhamiria kuizindua na huo mnara tutakaoujenga sasa tutaujenga kwa kumbukumbu yake mwenyewe Mzee Abeid Amani Karume.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nampongeza kwanza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia nataka niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa *round about* ya Michenzani ni pambo ambalo linapendezesha mji wetu, na kwa kuwa lengo la serikali ni kuendelea kuona mji wetu unakuwa kivutio siku hadi siku. Je, ni sababu gani hasa zinazoikabili *round about* ile mpaka ikawa inaonekana kupoteza haiba yake.

Pili, ni lini hasa serikali itatilia maanani kukidumisha hasa kivutio kile. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, sababu kubwa hasa iliyofanya miundombinu ile kutokufanya kazi zake siku za nyuma ilikuwa tatizo la maji, hilo hasa ndio lilikuwa kubwa. Ile miundombinu baada ya maji kuwa yana matatizo sote tunafahamu matatizo hayo nchini mwetu na hasa mitaa ya Michenzani basi ile *system* yote ilikufa ikawa wanapata tabu kweli kuifufua. Lakini tunashukuru kama nilivyosema wataalamu wa hizi sekta nilizozitaja walikaa chini wakaona nini wafanye tunaweza kuifufua japo kwa kuanzia kwanza ilibidi tujaze magari kwa magari ili tuone tatizo liko wapi. Lakini tunashukuru sasa wameweza kuifufua ile *system* na tayari kwa kweli imekuwa kivutio, tena yanaruka kama zamani na unapopita na gari lako Bi. Panya nakuomba ufunge vioo tunapowasha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuongezea majibu kidogo ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi. Kwa kuwa ni nia ya serikali katika kuweka kielelezo cha miaka 50 ya Mapinduzi kujenga mnara maalum wa kumbukumbu katika eneo lile, hii yote inaonesha ishara ya wazi kabisa

kuweka kumbukumbu sahihi za mapinduzi yetu na kuzidi kung'arisha mji wetu. Kwa hivyo, naomba tu Waheshimiwa Wawakilishi waelewe kwamba katika kipindi hiki cha kusherehekea miaka 50 kile kielelezo cha miaka 50 kitajengwa katika *round about* ile pale ya Michenzani.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na maelezo yake mazuri aliyotueleza kwamba moja ya kurejesha haiba katika *round about* ya Michenzani amesema kutajengwa mnara wa kumbukumbu mkubwa. Lakini katika kuweka haiba ya mji na kwenye *round about* zetu moja ni kuweka taa za kuongozea magari barabarani na kwa kuwa Zanzibar kila leo magari yanaongezeka zaidi na kwenye *round about* pamoja na kuweka vizuri zaidi basi taa zile zinasaidia kuongoza magari kupita na kuweka haiba nzuri zaidi kwenye mji wetu.

Kwa kuwa serikali ilishaanza kuweka mataa ya kuongozea barabarani kama pale Mkunazini namuuliza Mhe. Waziri. Je, ni lini wataona kwa sababu magari yameongezeka na ajali zinaongezeka kuweka taa za kuongozea barabarani ili kuweka mji wetu mzuri na wenye haiba zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mhe. Subeit kwamba kuongeza mazingira mazuri pale na hasa ukiangalia pana njia nne kubwa na gari zote zinazokuja mjini zinazotoka zinapita pale na ongezeko la magari liliopo nakubaliana na wazo lake la kuweka taa za kuongozea gari. Wazo hilo tunalo katika kutekeleza awamu ya pili ya kuweka taa zile za *solar* katika mji wetu wa Zanzibar.

Nam. 108

Kuharibika kwa Kalavati ya Kijito Mevi

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:

Mhe. Spika, kabla sijauliza swali langu naomba nimshukuru mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi Dr. Salmin Awadh kwa kunitoa wasiwasi kwamba Mwakilishi wake bado hajahamia Chadema Mhe. Nassor hapa.

Baada ya dibaji hiyo naomba swali langu sasa lijibiwe. Vijiji vya Gombani ya Kati, Simwambili, Ng'ambwa na Gawani huunganishwa na barabara kuu ya Wete/Chake-Chake, kupitia kwenye Kidaraja (Kalavati) ya mto wa "Kijito-mevi" ambayo hivi sasa tayari ni mbovu sana ambapo wakati wowote itadata au kukatika jambo ambalo huvifanya vijiji hivyo kuwa kisiwa.

(a) Je, serikali inalifahamu hilo.

(b) Ni lini serikali itafikiria kujenga daraja la kisasa katika eneo hilo pamoja na kujenga barabara ya vijiji hivyo katika kiwango cha lami.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali inalifahamu tatizo hilo.

(b) Mhe. Spika, suala la daraja na barabara hiyo ni suala la Halmashauri husika, kwani hata historia ya ujenzi wake wa daraja hilo lilijengwa na Halmashauri ya Mji wa Chake-Chake. Aidha, ni kweli daraja hilo liko katika hali isiyokuwa nzuri na isiyoridhisha na ni imani yetu wenzetu Halmashauri watashirikiana nasi katika kujenga upya daraja hili.

Hata hivyo, sisi kama wizara husika tumejaribu kuwaomba wenzetu wa Mfuko wa Barabara kuipitia barabara hiyo na daraja husika ili kuona namna gani wanaweza kusaidia wananchi katika ujenzi wa daraja hilo kulirejesha katika hali yake ya uzima wa asilia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sehemu ya Gombani ya Kati, Ng'ambwa, Gawani ni sehemu ambayo muhimu sana kwa uchumi wa Zanzibar kwa sababu ina mikarafuu mingi sana, na isitoshe inatoa zao linalopendwa sana hususan katika mwezi huu wa Ramadhani unaokuja hivi karibuni, zao la ndizi na majimbi. Na kwa kuwa mazao yale hayatumiki Pemba tu, yanatumika mpaka hapa Unguja. Kwa sababu Halmashauri yetu haina uwezo na ina mambo mengi sana ya kufanya huku uwezo wake ukiwa mdogo.

Je, Mhe. Waziri huoni kuendelea kuiachia Halmashauri kutengeneza kile kikalavati huku ukiwanyima futari watu wa hapa Unguja, walioko pale Chake- Chake na Mkoani huoni kwamba utakuwa umefanya kosa kubwa katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.

Pili, kwa kuwa kijidaraja kile mvua inapokuwa kubwa hufunikwa na ikabidi watoto wengine wanabururwa na hatimaye kuhatarisha maisha yao wale watoto wadogo wanapokwenda skuli. Je, huoni wizara yako itakapotengeneza

kile kidaraja itakuwa imeokoa maisha yetu ya vijiji vya Gawani, Vikunguni, Ng'ambwa pamoja na Gombani ya Kati.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kuwa ni kweli kama alivyosema ni sehemu yenye kilimo kuna mambo mawili yanafanyika katika barabara hii aliyoitaja. Kwa hivyo, naomba awe *up date* katika shughuli hii. Kwanza wizara yetu kwa kuanzia inafanya *grading* kuanzia Kianga kupitia Ng'ambwa hadi Mkorosheni ili njia iweze kupitika. Lakini pia barabara hii imeingizwa katika mradi wa uimarishaji wa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hivyo, imo katika mchakato wa kuweza kujengwa katika kiwango cha fusi barabara yote hii anayoizungumza. Naomba Mhe. Mwakilishi awe mvumilivu na kwa niaba ya wananchi wake wote walio katika maeneo haya barabara hii inaonekana na imo katika *pipe line* ya kufanyiwa matengenezo.

Nam. 10

Upatikanaji wa Huduma za Umeme na Maji

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya maji na umeme ni huduma muhimu kwa binadamu.

a) Wizara hasa ina mpango gani wa kuwapatia wananchi huduma hii kwa wale ambao huduma hii haijawafikia kabisa.
b) Kuna utaratibu gani uliowekwa na wizara kuwapatia wananchi taarifa kuhusiana na ahadi ambazo wizara imeshindwa kuzitekeleza.
c) Je, kushindwa kwa wizara kutekeleza kwa ahadi walizozitoa kwa wananchi si sawa na kuidhalilisha serikali na wananchi waliyoichagua serikali hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na juhudi mbali mbali za kuwasambazia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama kupitia miradi inayofadhiliwa na serikali, nguvu za wananchi pamoja na washirika wa maendeleo.

Mhe. Spika, kuhusu kuwapatia huduma ya umeme wizara yangu inatunga bajeti kila mwaka kuhakikisha kuwa vijiji ambavyo bado huduma hiyo haijawafikia inawafikia kama vile inavyokusudiwa na serikali.

Mhe. Spika, naomba kutokubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu imeshindwa kutekeleza ahadi zake kwani ahadi zote zilizotolewa zimetekelezwa kwa mujibu wa MKUZA II mwaka 2020.

Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali la (b) kwamba wizara yangu bado haijashindwa kutekeleza ahadi zake na inatekeleza ahadi zake kama vile zilivyotolewa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba uniruhusu niulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Nakuomba radhi kifungu (a) kitakuwa kirefu kidogo kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na bajeti ya 2012/2013, wizara iliahidi kuwa vijiji vyote vya Mtambwe Kaskazini vitapatiwa huduma ya maji na mpaka hii leo bado.

(a) Kwa sababu katika Wadi hii ya Mtwambwe kuna vijiji kama vile Mtambwe Mkuu hakuna umeme, Chekea/Chanjaani hakuna maji wala umeme, Mkanjuni/Kivumoni hakuna umeme, Makongeni hakuna maji, Mitambuuni/Tondooni pamoja na Kinazini hakuna maji hata umeme wakati wote na wakati Mheshimiwa anasema anatekeleza hatua kwa hatua. Ni kitu gani kilichosababisha vijiji hivi vyote kwa pamoja katika jimbo langu la Mtambwe mpaka leo vikakosa huduma kama hivyo nilivyoeleza.

(b) Kwa sababu Kijiji cha Matuuni kwa makusudi kabisa kutokana na umuhimu wa meme wamejitahidi na wamenunua wenyewe nguzo 26 ambazo wizara imekubali kuwa ni zenye kiwango, na ni mwezi wa nane hivi sasa nguzo zinalala zinaharibika bado wanashindwa kuwapelekea umeme wanasema walipie shilingi milioni 13. Je, Shirika hili la Umeme kufanya kama duka la watu binafsi na vifaa vya umeme ikawa mtu anahudumiwa kwa sababu ya kupeleka pesa zake tu ikiwa hana ndio hapati huduma, haoni kuwa hawatendei haki wnanchi na ni kuonesha kuwa hii wizara labda imeshindwa kufanya kazi ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba lengo la serikali kupitia wizara yangu ni

kuhakikisha kwamba vijiji vyote hufikishiwa huduma ya maji safi na salama pamoja na umeme. Lakini katika hivi vijiji ambavyo amevitaja niseme kwamba tayari tumeshayazungumza na wafadhili ambao wamekubali kutusaidia kuvipelekea huduma ya maji vijiji vya Kidundo, Chanjaani na Chekea ambavyo nategemea baada tu ya ujenzi wa barabara kumalizika kwa sababu sasa hivi hatuwezi kupeleka mtandao wetu wa mabomba wakati kuna ujenzi wa barabara, mpaka tuhakikishe kwamba barabara imeshakamilika na sisi tutapeleka mafundi wetu kwa ajili ya kujenga laini mpya ya maji na kuhakikisha kwamba vijiji hivyo alivyovitaja tutavipelekea huduma hiyo bila ya tatizo lolote.

Kuhusu suala la umeme ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi mimi na yeyé tushirikiane twende tukaangalie hivyo vijiji na mimi nitaziona hizo nguzo na nikishaziona nitawasiliana na watu wangu na ninamhakikishia kwamba vijiji hivyo tutavishughulikia na vitapata huduma hiyo kama inavyostahiki kwa vijiji vyengine.

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo ya kukatika katika kwa umeme kutokana na *transformer* kuzidiwa. Lakini pia kwa kuwa baadhi ya maeneo kuna *line* kongwe sana zimechoka na pia zimezidiwa sana na umeme. Je, Mhe.Waziri suala hili ni lini utalitatua ili kuondosha matatizo ya umeme kabisa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba yako baadhi ya maeneo yanajitokeza matatizo kama hayo ya kukatika umeme mara kwa mara. Lakini ni kweli kwamba kuna uchakavu baadhi ya maeneo kwa miundombinu yetu lakini tayari sasa hivi Shirila la Umeme limeshajipanga kwa kubadilisha nguzo na kuweka nguzo mpya na *transformer* mpya. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi avute subra kidogo, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme liko tayari na inajitahidi kulishughulikia tatizo hilo.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na yanafahamika vizuri. Kama ninavyojua Mhe. Spika, Jimbo la Bububu lina matatizo makubwa sana ya maji na mpaka hivi sasa shida hiyo ya maji inaendelea sasa na huu mwezi wa Ramadhani unakuja. Je, Mhe. Naibu Waziri wamejipanga vipi kutatua tatizo la maji kwa mwezi huu wa Ramadhani kwa Jimbo la Bububu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba baadhi ya maeneo ya Bububu kuna matatizo ya maji lakini sio sehemu yote ya Bububu. Sasa hivi tayari tumeshapeleka mtandao mpya wa maji na kuna baadhi ya wananchi bado wanatumia miundombinu ya zamani, hii miundombinu ya zamani kweli ina matatizo lakini kwenye miundombinu mipya tayari tumeshajipanga vizuri. Kwa hivyo, tunachotaka kukifanya hili suala tunalijua na tutachokifanya ni kwamba tutahakikisha wale wote ambao wanapata matatizo kwa kupitia mtandao wa zamani basi tutaunganisha kwenye line zetu mpya ili tatizo hilo liwaondokee.

Nam. 70

Ununuzi wa Mashine ya *DNA*

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Moh'd Shein kupitia taasisi moja ya Marekani, tayari imeshapata msaada wa sehemu moja ya mashine ya kuchunguza vinasaba (*D.N.A machine*) na bado sehemu nyengine mbili ili mashine iweze kufungwa na kuanza kazi rasmi.

Kwa kuwa Wazanzibari huendelea kupata usumbufu wa kupeleka "s*pecimen*" za vinasaba Tanzania Bara kwa ajili ya uchunguzi, ni lini serikali yetu itakamilisha ununuzi wa mashine hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi mwana Mapinduzi swali lake Nam.70 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshapata kifaa kimoja kwa msaada sehemu ya mashine inayochunguza vinasaba vya *DNA Machine.* Kifaa hicho kilitoka *Brown University* ya Marekani na bado sehemu mbili ambazo ni *Genetic Analyser na PCR machine*, ili kiweze kufungwa na kuanza kazi rasmi. Vifaa hivyo viwili gharama yake ni shilingi 600 milioni, na Wizara ya Afya inafanya taratibu za kuvipata kwa kuwahusisha wafadhili mbali mbali.

Mhe. Spika, suala la kusema kuwa Wazanzibari huendelea kupata usumbufu wa kupeleka "*specimen*" za vinasaba Tanzania Bara kwa ajili ya uchunguzi hilo halina ukweli. Kwa sababu ili huo uchunguzi ufanyike lazima kuwe na

sababu maalum ya kufanya hivyo. Sababu kubwa inayofanyiwa kipimo hicho ni kesi ya mwanamme anayekataa kwamba mimba si yake anapompa uja uzito msichana, hiyo ndio sababu. Na ili *specimen* ipelekwe huko, inahitaji barua rasmi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali iende na *specimen* mbili za baba na mama kwa ajili ya ulinganisho.

Mpaka sasa ni kesi mbili tu ambazo polisi ndio walizozichukulia vithibitisho vya baba na mama kutoka *One Stop Center* huko Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa kesi za kubaka na kulawiti ikiwa mtu anajulikana na mtendewa anao ushahidi wa kitaalamu unaotafuta na ukathibitishwa na *One stop center* hakuna ulazima wa *DNA* kufanya. Uthibitisho huo unatosha kumfikisha mtu Mahakamani na muhanga kupatiwa haki yake.

Tatizo linalokwamisha kesi hizo liko katika vituo vya Polisi anakopelekwa muhanga kwa mara ya kwanza kwa sababu wao ndio wanaandaa kesi.
Pili ni jamii yenyewe kutokutoa ushirikiano kwenye kuendesha kesi. Kesi nyingi zinamalizwa majumbani bila ya kumjali muathirika kwa kuogopa aibu au uhasama wa mitaani au ugomvi wa familia. Pia kesi ikiweza kufika mahakamani wenye kesi wanakataa kwenda kutoa ushahidi na hatimae hupelekea kesi kufutwa, kwa mtazamo huo wa tatizo hili, elimu kwa jamii inahitajika na ushauri nasaha kwa wale wanaofikwa na tatizo.

Mhe. Saleh Nassoro Juma: Kwa kuwa suala lake la msingi zaidi ametilia mkazo kesi hizi za baba kamkataa mtoto kakataa mimba. Lakini kwa kuwa Mhe. Spika, hii *DNA machine* vile vile inaweza ikafanya mambo nyeti sana ikiwemo *criminal* kwa kuweza ku-*dictate* mashiko ambayo kama muhalifu ameyaacha pale kama kashika au kakamata haya pia tunaweza kufanya kama *confirmatory case*.
(a) Na kwa kuwa Tanzania sasa hivi tuko mbele katika masuala ya demokrasia na utawala bora na ndio maana akaja Rais Obama juzi katika hili na alishindwa kufika Zanzibar. Napata wasi wasi kwa sababu kama mambo muhimu yamekosekana huku kwetu. Kwa msingi huo je, Mhe. Naibu Waziri kwa sababu Wamarekani wameshatusaidia hii *DNA machine* na kwa sababu siku zimeshakuwa nyingi hizi mashine mbili Serikali haijazipata. Mhe. Spika, hii ni kwa sababu Serikali haina pesa au ni kwa sababu haishughuliki na wananchi wake au ni kwa sababu ya uzembe tu.

(b) Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa sisi ni sehemu ya Tanzania na wenzetu kama hivyo wanaongaza kwa demokrasia na ndio maana Obama akaja na kwetu asifike upande huu wa Tanzania wa pili huku asifikie. Je, hamuoni kwamba Serikali yetu kutonunua ile mashine ya *DNA* pale ni sehemu ya kutokuiwezesha demokrasia kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kesi za jinai pia zinahitaji *DNA* hasa kama kitu kimejificha miaka mingi, lakini *DNA* inaweza ikatoa ushahidi. Na kesi nyingi tu zinafanyika na ni kweli kwa hali inavyokwenda sasa hivi *DNA* ni muhimu sasa kama ingekuwa ni kitu chepesi na cha rahisi tungekuwa tumeshakipata.

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme jambo moja na nimesema hapa kwamba hivyo vitu viwili vilivyobakia vinahitaji shilingi milioni mia sita, kama wizara kutoa milioni mia sita ikanunua kwa matatizo tulionayo kwa kweli kwetu huo utakuwa ni usawa.

Lakini tukizungumza Serikali, Serikali ya Tanzania ni yetu sote na ya Muungano ni Serikali ya Tanzania na Tanzania Bara kifaa kipo, tukinunua milioni mia sita ukishaitumia ina maana kinafanyakazi bado. Hapo bado kuna vitu vyengine ambavyo pia vinahitajika ili hiyo mashine iweze kufanyakazi inahitaji *spiceman* mia sita ndio iweze kufanya kazi.

Uhusiano wa Afrika Mashariki unasema hivi *centr*e moja ikiwa ina kitu ambacho kinaweza kusaidia sehemu nyengine ni bora kiwe kimoja ili nyote mpeleke kule, kwa sababu ya kupunguza gharama. Kama tungekuwa wakweli wa nafsi zetu Zanzibar tusingekuwa na haja ya kufanya *DNA machine* wakati Tanzania Bara zipo na shilingi laki tatu tu kwa *statement*.

DNA hiyo na picha zikishanunuliwa mpaka tupate *spiceman* ili iweze kufanyakazi. Gharama hiyo kweli inalingana na maneno anayoweza kusema Mhe. Mwakilishi na Serikali ina nia tutafanya, kwa sababu mnasema tukipata uwezo tutafanya lakini hakutakuwa na manufaa hiki chombo kwa ajili ya Zanzibar kwa *statement*.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, sana kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.
Mhe. Spika, kwa sababu tulipopata ajali ya meli na umuhimu wa Zanzibar kuwa na meli yake Serikali ilitafuta namna ya kupata fedha kununua meli hiyo.

(a) Je, kutokana na umuhimu wa chombo hichi ambacho ni king'amuzi cha kung'amua haki, Serikali ina mpango gani wa kutoa kauli kama iliyotoa kule kuona kuwa hizi mashine mbili zilizopungua zimepatikana na chombo hiki kinafanyakazi ipasavyo kwa maslahi yetu.

(b) Kwa sababu kuna kesi nyingi zimetokea ya mambo haya haya vizazi na kusababisha watu kuoana wakati sio waliosababisha mimba katika watoto walioowana. Je, kama mtu Mwenyezi Mungu akitujaalia hichi

chombo kikaanza kufanya kazi akitaka kukata rufaa ikaja ikaonekana kuwa kaozeshwa mtoto ambaye si wake kutokana na sababu akaozwa yeye. Chombo hichi kitaweza kusaidia kutoa ushahidi kuonesha kuwa huku tulikopita nyuma si haki na mtu yule arejeshewe haki yake kutokana na alivyozungumza kwa ufanisi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Utibatu: Mhe. Spika, mini nataka uniuliuze swali ili nifahamu. Nenda moja kwa moja ili nikufahamu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe nenda kwenye swali moja kwa moja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru narudia swali na nitalieleza kwa uzuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa kukosekana chombo hichi zimetokea kesi nyingi hapa baina ya vijana waliopata ujauzito na watuhumiwa waliofanya ujauzito huo wakaozeshwa watu ambao hawajahusika, na kwa sababu hakuna chombo hichi ndio mambo yanaendelea kama yalivyo.

Lakini kwa sababu yule aliyeozeshwa hajaridhika anajua kuwa mtoto yule si wake na chombo hiki kikaanza kufanya kazi kikamilifu, yule mtu akataka siri kuonesha ushahidi kuwahi kuwa hakuwa yeye, kweli chombo kitasaidia kwa kutumia *DNA* ya mtoto, baba na mama aliyesababisha mimba ile ili kuonesha kwa kweli ilikuwa ndiye au siye.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sasa swali nimelifahamu. Napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Baada ya kusema hiyo nadharia yote ya hilo suala lenyewe kipimo kikifanywa kwa sababu ili kipimo kifanyike kuhakikisha kwamba mtoto huyo wa baba na mama lazima *specimen* itoke kwa baba na mama ili iweze kulinganishwa. Na kama baba ni wa kwake kitasema kwamba huyu ni baba yake. Kuna kesi ndogo tu ambayo kama mnasoma magazeti juzi imetokea kuna mwanamuziki anayeitwa Beyonce wa Marekani ana baba yake anaitwa Noel ndiye baba yake na ndiye *director* wa muziki wake anaofanya, ndiye muuzaji, ndiye meneja lakini kamkataa baba yake. Hivi sasa kufanya hiyo kazi kwa sababu baba yake kamsaliti mama yake kwa kutembea na mtu wa nje akazaa naye mtoto.

Lakini baba alikataa katakata na yule baba akasema kwamba huyo mwanamke hamjui mwanamke wa nje, akasema kwamba huyo ndiye baba yake wakapimwa na akakutikana kama huyo ni baba yake.

Kwa hiyo, mwanamke aliyekuwa mwanzo kaachwa na huyu mwengine kilichoendelea sikijui.

Sasa ninachotaka kusema kwamba kama si mwanao itakwambia si wako, lakini nataka nikuhadharisheni kitu kimoja, tukianza utaratibu huu ndoa nyingi zitavunjika, tukianza utaratibu huo tutakuwa tunaikataa misingi ya Kiislamu. Kwa sababu misingi ya Kiislamu inasema hivi, midhali huyu ni mkeo hata ukiondoka miaka minne ukirudi ukimkuta mtoto ni wako na hata mtoto awe anafanana na wewe *copy right* madhali hayuko kwenye ndoa si wako. Kwa hivyo, tutahadhari na mambo mengine. (*Makofi*).

UTARATIBU

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, tulipokuwa juzi tukiijadili bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Machano Othman Said alijaribu kujibu hoja.

Baada ya kujibu hoja Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Makame Mshimba Mbarouk alikaa baada ya kuwa kuna majumuisho alikataa kusikiliza hoja ile na akasema hawezi Mhe. Waziri kutoa majumuisho isipokuwa anataka kwa Mhe. Waziri na kwa sababu Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, hana kiti, hana ofisi wala hana meza.

Sasa narudia kipengele cha Katiba namba 43.5 Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kunukuu:

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar."

Kwa tafsiri hiyo naomba muungozo wako kuweza kujua na Mawaziri wasiokuwa na wizara maalum wanaweza kujibu hoja za Serikali au hawawezi kujibu hoja za Serikali. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe suala ambalo linahitaji muungozo nadhani wale sio suala gumu. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum ni *member* wa *cabinet* na kama ni *member* wa *cabinet* anaweza akapewa kazi wakati wowote na Mhe. Rais kafanye kazi hii. Na kwa mujibu wa kifungu ambacho Mhe. Naibu Waziri amekisoma kwamba Serikali inawajibika kwa pamoja ni pamoja na Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum.

Kwa hivyo, kama kuna jambo ambalo Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum amelisema na linaendana na ukweli wenyewe. Mimi sioni sababu jambo hilo kukataliwa huwa ni sehemu ya majibu rasmi ya kutolewa na Serikali katika chombo hichi. Majibu kama hayo yanakubalika ila kama kutakuwa na suala la kusahihisha basi kiongozi wa shughuli za Serikali anaweza akakukumbusha pale ambapo kumekuwa na makoseo.

Jambo ambalo ni la kawaida hata kwa mawaziri wa kawaida anaweza akatoka taarifa, kwa mfano waziri mmoja amejibu swali lakini kuna taarifa kidogo imetetereka waziri mwengine anaweza kutoa taarifa kwamba suala hili ambalo Mhe. Waziri amelisema kidogo taarifa ile haiko sahihi, sasa akajibu yeye. Huo ni utaratibu wa kikao hichi, Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum ni *member* wa *cabinet* na anaweza akafanya kazi ya Serikali kwa niaba Serikali. Ahsante sana. (*Makofi*).

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara Katiba na Sheria

Mhe. Spika: Ahsante sana sasa namuomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika**,** sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetuwezesha kukutana tena leo hii kwa ajili ya kujadili masuala muhimu yanayohusu mipango yetu ya maendeleo. Tunamuomba atupe hekma na uwezo wa kuyafanikisha hayo kwa faida ya nchi yetu, Amin!

Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha taarifa za wizara yangu naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini ambao umeleta heshima kubwa kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa utendaji wao makini na ushauri wanaompa Mhe. Rais, ambao bila shaka unasaidia kuleta ustawi wa nchi yetu. Napenda pia niwashukuru viongozi hawa kwa kutupa muongozo mzuri

pamoja na maagizo yao ya busara ambayo yamesaidia sana katika wizara yangu kutekeleza vizuri zaidi majukumu yetu.

Mhe. Spika, naomba pia ruhusa yako ili nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Baraza letu kwa upeo na uwezo mkubwa ambao umelijengea hadhi kwa wananchi. Vile vile, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Baraza hili kwa kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, nawapongeza watendaji wa Baraza kwa kufanya kazi zao kwa umahiri.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, naomba ruhusa yako ili nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati zote za Baraza kwa kutekeleza majukumu yao kwa umakini. Aidha, naomba kutoa shukurani maalum kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliyomaliza muda wake chini ya uongozi wa Mhe. Ali Abdalla Ali, kwa kuishauri vizuri Wizara yangu. Nachukua fursa hii kuikaribisha Kamati mpya ya Katiba, Sheria na Utawala, inayoongozwa na Mhe. Ussi Jecha Simai.

Vile vile napenda kuishukuru Kamati ya *PAC* iliyomaliza muda wake kwa kufanya kazi nzuri kwenye Wizara yangu na tunaikaribisha kwa dhati *PAC* mpya chini ya uongozi uliokomaa wa Mhe. Omar Ali Shehe. Tunatarajia Kamati hizo na nyengine, zitaendelea kutushauri ipasavyo katika kipindi kinachofuata. Mimi pamoja na watendaji wa wizara yangu tunawaahidi ushirikiano wa dhati.

Mhe. Spika, pamoja na shukrani hizo naomba niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mgogoni kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha majukumu yangu ya uwakilishi katika jimbo letu, na kwa kunivumilia wakati wote ninapokosekana jimboni kutokana na majukumu ya kitaifa. Natumai tutaendelea kushirikiana ili kuharakisha maendeleo ya jimbo letu.

HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 7,591,000,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 4,393,130,052.00 zilipangwa kulipia mishahara na stahiki mbali mbali za watumishi na Shilingi 3,197,869,948.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2013 Shilingi 4,909,058,935.00 zilikuwa zimepatikana. Kati ya fedha hizo, Shilingi 3,051,545,020.00 ambazo ni 76%, ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, Shilingi 1,373,038,809.00 (47%) kwa matumizi mengineyo, na 484,475,106.00 (71%) ni ruzuku. Kwa kazi za

maendeleo, Shilingi 6,682,200,000.00 ziliidhinishwa. Kati ya hizo, Shilingi 3,455,000,000.00 ni mchango wa Serikali na Shilingi 3,227,200,000.00 ni msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kufikia Machi 2013, Shilingi 1,657,552,527.00 zilikuwa zimepatikana ambapo Shilingi 1,468,913,527.00 sawa na 43% ni mchango wa Serikali na Shilingi 188,639,000.00 (6%) zilitoka kwa washirika wa maendeleo. Wizara pia ilikadiria kukusanya Shilingi 447,000,000.00 ili kuchangia mapato ya serikali. Hadi Machi 2013, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 288,708,060.00, sawa na asilimia 65%. *Angalia Viambatanisho Nam. 1&3.*

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2012/13

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inatekeleza miradi ya maendeleo ifuatayo:-

(i) Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria;

(ii) Mradi wa Kuimarisha Taasisi za Wizara unaohusisha Utafiti wa Matumizi ya Sheria za Zanzibar, Utafiti kuhusu uwezekano wa kuanzisha Kituo cha Utamaduni cha Kiislamu, na Utayarishaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini;

(iii) Mradi wa Marekebisho ya Mfumo wa Usajili wa Biashara na Uimarishaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali;

(iv) Mradi wa Marekebisho ya Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii;

(v) Mradi wa Mapitio ya Sheria za Zanzibar;

(vi) Mradi wa Matengenezo ya Majengo ya Mahkama;

(vii) Mradi wa Kuanzisha Mahkama ya Biashara;

(viii) Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

(ix) Mradi wa Ujenzi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(x) Mradi wa Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Katiba na Sheria. Utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kazi ya kuandaa mkakati wa mabadiliko katika sekta ya sheria imefikia hatua ya kutayarishwa rasimu ya mwanzo ambayo inatarajiwa kupelekwa kwa wadau. Kazi hii inaratibiwa na Kamati Simamizi

inayohusisha wajumbe 10 kutoka katika baadhi ya taasisi za Sheria Zanzibar. Vile vile Wizara kwa kushirikiana na *UNDP* imo katika hatua za kumpata Mratibu wa Programu ya Mabadiliko katika Sekta ya Sheria, ili kazi ya kukamilisha matayarisho ya mkakati na utekelezaji wake vifanyike kwa ufanisi zaidi. Washirika wengine katika Programu hii ni *UNICEF*, na Jumuiya ya Ulaya.

Mhe. Spika, Utafiti wa Matumizi ya Sheria za Zanzibar umefanyika ili kubainisha Sheria zilizopitwa na wakati miongoni mwa Sheria za Zanzibar. Utafiti huo unafanywa na wataalam wa ndani na rasimu ya mwanzo ya utafiti huo iko tayari na inatarajiwa kujadiliwa na wadau hivi karibuni. Vile vile matayarisho ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini yamefanywa kwa kutumia wataalamu wa ndani. Hatua iliyofikiwa ni kupata ripoti ya mwanzo ambayo tayari imekwishajadiliwa. Mtaalamu bado anaendelea kupokea michango mbali mbali kutoka kwa wahusika ili kujiandaa na kuwasilisha ripoti ya mwisho ya kazi hiyo. Mfumo huu utakapokamilika utarahisisha upatikanaji wa taarifa zitakazowezesha kupima ufanisi wa kiutendaji wa Idara na Taasisi za Wizara. Kwa upande mwengine, Utafiti wa Kuanzisha Kituo cha Utamaduni wa Kiislamu unatarajiwa kuanza wakati wowote zitakapokamilika taratibu za kumpata mtaalamu na fedha.

Mhe. Spika, mradi wa Marekebisho ya Mfumo wa Usajili wa Biashara una lengo la kurekebisha mfumo wa usajili wa taasisi za biashara na tasnia ya mali za ubunifu (*Industrial Property Automation System - IPAS*) na kufanya marekebisho ya sheria zinazosimamia usajili. Sheria zinazohusika ni Sheria ya Kampuni (*Companies Decree Cap*. 153) na Sheria ya Ufilisi (Insolvency Decree Cap. 20). Rasimu ya Sheria mpya ya Kampuni tayari imejadiliwa kwenye vikao vinavyohusika, ikiwemo Baraza la Mapinduzi. Matayarisho ya Rasimu ya Sheria mpya ya Ufilisi yanaendelea. Vile vile, Kanuni za Sheria ya Tasnia za Mali za Ubunifu imekamilika na itawasilishwa kwa Shirika la Kimataifa la Mali za Ubunifu (*World Intellectual Property* Organization (*WIPO*) na Shirika la Mali za Ubunifu la Afrika *(Africa Regional Intellectual Property Organization' (ARIPO*), kwa ajili ya kupata maoni.

Mhe. Spika, mradi wa Uimarishaji Usajili wa Matukio ya Kijamii ulianza mwaka 2010, na unagharamiwa na Serikali pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNFPA*. Chini ya Mradi huu, Mfumo wa Usajili wa Kielektroniki umeanzishwa na matayarisho ya kutunga Sheria ya Usajili wa Matukio ya

Kijamii yanaendelea. Rasimu hiyo imejadiliwa kwenye vikao vinavyohusika ikiwemo Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, mradi wa Matengenezo ya Majengo ya Mahkama, kwa mwaka wa fedha wa 2012/13, ulihusisha kuendelea na matengenezo ya sehemu ya nje ya jengo la Mahkama Kuu Vuga, kazi ambayo inaendelea. Jengo la Mahkama ya Kadhi Mwanakwerekwe limefanyiwa matengenezo kwa kuongezwa urefu wa kuta zake, kuezekwa na kutiwa umeme. Kwa upande mwingine, matengenezo ya Mahkama ya Chake Chake na Makunduchi hayakuweza kufanyika kutokana na upungufu wa fedha.

Mhe. Spika, mradi wa Kuanzisha Mahkama ya Biashara ulihusisha matengenezo ya jengo na kutungwa kwa Sheria. Hadi kufikia sasa Sheria imepitishwa Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, Mahkama ya Biashara haitaweza kuanza kazi katika mwaka wa fedha 2013/14 kutokana na ukosefu wa bajeti. Tunatarajia Mahkama hiyo itasaidia kupunguza mzigo wa kesi kwenye Mahkama za kawaida, na pia kuyashughulikia kwa haraka na umakini zaidi mashauri yanayohusu biashara.

Mhe. Spika, Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka 2012/13 ulikusudia kuwapatia makaazi Waendesha Mashtaka wanaopelekwa kufanya kazi kwenye Mahkama za Wilaya ili wawe karibu na vituo vyao vya kazi. Hivi sasa mradi huo unakamilisha ujenzi wa nyumba iliyopo Madungu Pemba na umeanza ujenzi wa nyumba ya Makunduchi ambayo imefikia hatua ya kuezekwa. Maandalizi ya nyumba ya Mkokotoni yameanza katika hatua ya kupata kiwanja na kutayarisha michoro.

Mhe. Spika, mradi wa Ujenzi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ulikusudia kuipatia Afisi ya Mwanasheria Mkuu jengo jipya kwa ajili ya shughuli za Ofisi. Ujenzi umefikia hatua za kazi za kumalizia, zikiwemo kuweka mifumo ya usalama, udhibiti wa moto na mawasiliano. Matarajio ni kukamilisha ujenzi na kuhamia katika mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara ulianza April 2012 katika eneo la Mazizini Unguja. Mradi huu una lengo la kuiwezesha Wizara kuwa na Jengo la kisasa litakalotosha kwa matumizi ya Ofisi za Wizara na taasisi zake. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Novemba 2013, ikiwa fedha za ujenzi zitapatikana kama tulivyokubaliana. Kama hilo litawezekana jengo hili litakuwa ni moja ya miradi itakayofunguliwa kwenye Sherehe za Mapinduzi yetu matukufu ya 1964 kufikia miaka 50, na kuwa moja ya vielelezo vya mafanikio ya Mapinduzi hayo. Ujenzi huo umefikia ghorofa ya tano na jumla ya Shilingi 2,513,832,424.00 zimetumika kumlipa mjenzi.

UTEKELEZAJI WA IDARA NA TAASISI ZA WIZARA

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa shughuli za Wizara yangu kwa mwaka 2012/13 kwa kuangalia maendeleo ya taasisi moja moja kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu Mipango, Sera na Utafiti, pamoja na kutekeleza shughuli za kila siku. Katika mwaka wa fedha wa 2012/13, Idara imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Idara imeratibu maandalizi ya ripoti na taarifa mbali mbali za utekelezaji na kuziwasilisha kunakohusika. Idara pia imeratibu maandalizi ya bajeti ya Wizara pamoja na maandiko ya miradi sita na kuyawasilisha Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Angalia Kiambatanisho Nam. 4.

Mhe. Spika, miongoni mwa majukumu ya Idara hii ni kuratibu shughuli za *NGOs*. Katika mwaka wa fedha 2012/13 Idara imefanya mapitio ya Sheria ya Jumuiya Zisizo za Serikali (Nam. 6 ya 1995). Rasimu ya Sheria hiyo imejadiliwa kufikia ngazi ya Kamati ya Uongozi ya Wizara. Mapendekezo ya Kamati ya Uongozi yamezingatiwa na sasa rasimu hiyo inatarajiwa kurejeshwa tena kwenye Kamati kwa maamuzi. Aidha, Idara imeanza kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya *NGO's* ya mwaka 2009 kwa kuanza uhakiki wa *NGOs* zilizosajiliwa Zanzibar. Kazi hiyo imefanyika katika Wilaya nne za Unguja ambapo jumla ya *NGOs* 43 zimehakikiwa. Katika mwaka ujao wa fedha, kazi hiyo itaendelea Mkoa wa Mjini/Magharibi na Kisiwani Pemba. Lengo la uhakiki huo ni kujua kwa usahihi Jumuiya zilizo hai ili kuziondoa zile ambazo haziwajibiki ipasavyo kwa mujibu wa sheria, na kuweka mikakati ya kuziimarisha Jumuiya zinazofanya kazi zake vizuri na zinazowajibika kisheria.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imetoa mafunzo kwa njia ya Semina kwa Maafisa Mipango na Wahasibu wa Taasisi za Wizara, ili kuwajengea uwezo katika utengenezaji wa malengo na shabaha za kibajeti. Kwa upande mwengine, katika kujiimarisha, Idara imewapatia mafunzo watumishi wake watatu.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa Shilingi 172,860,000.00. Hadi kufikia Machi 2013, Shilingi 65,244,700.00 zimetumika kwa malipo ya mishahara na stahiki nyengine za watumishi na Shilingi 41,709,200.00 kwa matumizi mengineyo. Shilingi 787,200,000.00 ziliidhinishwa kwa kazi za Maendeleo na hadi kufikia Machi 2013, fedha

zilizopatikana ni Shilingi 237,251,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 48,612,000.00 (30%) ni kutoka Serikalini na Shilingi 188,639,000.00 (30%) kutoka kwa washirika wa maendeleo. *Angalia Kiambatanisho Nam. 1.*

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/14 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha Uratibu wa Sera, Mipango, Miradi ya Maendeleo na Ripoti za Utekelezaji;
ii. Kukamilisha Waraka wa Mkakati wa Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria;
iii. Kufanya utafiti wa taarifa za msingi za sekta ya Sheria (*baseline study*); na
iv. Kutayarisha Sera ya Msaada wa Huduma za Kisheria Zanzibar (*Legal Aid Policy*).

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 184,152,000.00 kwa matumizi ya kawaida, zikiwemo Shilingi 94,596,000.00 za mishahara na Shilingi 89,556,000.00 za matumizi mengineyo. Vile vile, naomba Baraza liidhinishe Shilingi 1,454,313,000.00 kwa kazi za maendeleo, zikiwemo Shilingi 150,000,000.00 kutoka Serikalini.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina dhamana ya kusimamia na kuratibu shughuli zote za Uendeshaji na Utumishi zinazofanywa ndani ya Wizara na Taasisi zake. Katika mwaka wa fedha wa 2012/13, Idara imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kuimarisha uwezo wa kuratibu masuala ya utumishi na kusimamia uendeshaji, Idara imeanzisha Kamati ya Utumishi ya Wizara. Kamati hiyo inajumuisha Maafisa Utumishi na inaendelea kukutana na kuratibu masuala ya kiutumishi, ikiwemo miundo ya utumishi na madaraja ya wafanyakazi, matayarisho ya *nominal roll*, mipango ya mafunzo, uajiri na utunzaji wa kumbukumbu za ofisi na za wafanyakazi.

Mhe. Spika, Idara kupitia kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, imekamilisha ukaguzi katika taasisi zote za Wizara, Unguja na Pemba. Ripoti za Ukaguzi wa Ndani za Julai – Septemba na Oktoba - Disemba 2012/13 zimeshawasilishwa kwenye Kamati ya Ukaguzi ya Wizara. Ripoti ya Januari – Machi 2013 iko kwenye hatua za kukamilishwa.

Mhe. Spika, Idara kupitia Kitengo cha Uhasibu imefanikisha kazi ya kurekebisha vifungu vya matumizi baada ya Marekebisho ya Bajeti ya Wizara; kutoa ufafanuzi wa Hoja za Ukaguzi wa Ndani na Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa Ripoti ya Upatikanaji wa Matumizi ya Fedha kwa vifungu vya Wizara.

Mhe. Spika, Idara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa Wizara kwa kununua vifaa na huduma mbali mbali kwa mujibu wa sheria ya Manunuzi Nam. 9 ya 2005. Aidha, Idara imeendesha mafunzo ya siku mbili kwa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Wizara, kuhusu Sheria na Taratibu za Manunuzi, pamoja na utunzaji na uwekaji Kumbukumbu za Mali za Serikali. Katika kipindi cha Julai 2012 - Machi 2013, Idara imeandaa vikao tisa vya Bodi ya Zabuni.

Mhe. Spika, taratibu za kuanzisha *data base* ya wafanyakazi wa Wizara zimeanza kwa kuhakiki na kupitia mafaili ya wafanyakazi. Kazi ya kuingiza taarifa kwenye *data base* inatarajiwa kuendelea katika mwaka wa fedha wa 2013/14. Aidha, Idara imeanza hatua za kutayarisha Mpango wa Rasilimali Watu wa Wizara (*Human Resource Plan*) kwa kukusanya na kuhakiki taarifa za awali. Matayarisho kamili ya mpango yanasubiri muongozo kutoka Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pamoja na kazi hiyo, Idara inafanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa wizara na tayari imeandaa Mpango wa Mafunzo wa mwaka mmoja.

Mhe. Spika, hali ya watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria inaendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Idara na Taasisi za Wizara. Hivi sasa Wizara ina jumla ya wafanyakazi 797 wakiwemo wanawake 293 na wanaume 504. Idadi ya wafanyakazi wenye elimu ya Stashahada au zaidi ya hapo ni 33% ya wafanyakazi wote. *Angalia Viambatanisho 9a-c.*

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara, Idara imesomesha Wafanyakazi 12; mmoja Shahada ya pili, mmoja shahada ya kwanza, watatu Stashahada ya Uzamili, watano stashahada, na wawili cheti. Kati ya watumishi hao wanawake ni saba na wanaume ni watano. Aidha, Idara imo katika hatua za kukiimarisha Kitengo cha Mawasiliano cha Wizara na kwa kuanzia imeajiri Afisa Mawasiliano atakayefanya kazi za kitengo hicho. Idara pia inaendelea kuimarisha tovuti ya Wizara kwa kuingiza kumbukumbu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 566,653,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 314,343,000.00 zilitengwa kwa malipo ya mishahara na stahiki za

Watumishi na Shilingi 252,310,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2013, zilipatikana Shilingi 228,011,820.00 (73%) kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 116,289,299.00 (46%) kwa matumizi mengineyo. *Angalia Kiambatanisho Nam. 1.*

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha uratibu wa majukumu ya Rasilimali Watu;
ii. Kuimarisha uratibu wa kazi za utawala za Wizara; na
iii. Kuimarisha miundo mbinu ya kutoa huduma.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza majukumu yake, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 591,141,000.00 kwa kazi za kawaida, zikiwemo 338,831,000.00 kwa mishahara na 252,310,000.00 kwa matumizi mengineyo.

MAHKAMA

Mhe. Spika, Mahkama ndicho chombo chenye jukumu la kikatiba la kusimamia utoaji wa haki. Katika kufanikisha jukumu hilo usikilizaji wa kesi za jinai, madai, pamoja na rufaa za jinai na madai ni jambo la msingi. Katika mwaka wa fedha 2012/13 Mahkama imepokea na kusajili kesi 6,039 kutoka Mahkama zote, Unguja na Pemba. *Angalia Viambatanisho 5a&b*.

Mhe. Spika, kutoka Julai 2012 hadi Machi 2013, Mahkama Kuu imepokea mashauri mapya 237, na kuifanya iwe na jumla ya mashauri 492, ukijumuisha na mashauri 255 yaliyopokelewa kabla. Katika kipindi hicho, Mahkama Kuu imetoa uamuzi kwa mashauri 16. Katika Divisheni ya Mahkama ya Kazi, yamepokelewa Mashauri mapya 6 na kuifanya Divisheni hiyo iwe na mashauri 31 kwa kujumuisha na mashauri 25 yaliyosajiliwa kabla. Mahkama hiyo imetoa uamuzi kwa mashauri 2.

Mhe. Spika, katika Mahkama za Mkoa, mashauri mapya 291 yamepokelewa na kufanya Mahkama hizo ziwe na jumla ya mashauri 720, kwa kujumuisha na mashauri mengine 429 yaliyosajiliwa kabla ya kipindi hicho. Katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013, Mahkama za Mikoa zimetolea maamuzi mashauri 21. Wakati huo huo, Mahkama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,927 na kufikisha jumla ya mashauri 2,890, yanapojumuishwa na mashauri 963 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013, Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 875.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013, Mahkama ya Kadhi ya Rufaa imepokea mashauri mapya 63, na kuifanya iwe na jumla ya

mashauri 78, yanapojumuishwa na mashauri 15 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 37 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Vile vile, Mahkama za Kadhi wa Wilaya zilipokea mashauri mapya 1222, na kuwa na jumla ya mashauri 1852, baada ya kujumuishwa na mashauri 630 ya siku za nyuma baina ya Julai 2012 na Machi 2013 Mashauri 311 yametolewa uamuzi.

Mhe. Spika, katika Mahkama za Mwanzo mashauri mapya 2263 yamepokelewa na kufanya Mahkama hizo kuwa na jumla ya mashauri 2711 yanapojumuishwa na mashauri 443 yaliyosajiliwa kabla. Kuanzia Julai 2012 hadi Machi 2013, mashauri 1502 yametolewa uamuzi.

Mhe. Spika, Mahkama ya Rufaa ya Tanzania ilianza mwaka wa fedha 2012/13 ikiwa na idadi ya mashauri 134 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma na kupokea mashauri mapya 5 na hivyo kufanya idadi ya mashauri kufikia 139. Aidha katika kipindi cha Julai 2012 hadi Machi 2013 Mahkama ya Rufaa ya Tanzania imetolea uamuzi mashauri 133.

Mhe. Spika, tathmini hiyo inatuonesha kwamba kwa wastani Mahkama zetu zimeweza kutoa uamuzi kwa kesi 2,897 kati ya kesi 8,913 ambayo ni jumla ya kesi 6,039 zilizofunguliwa katika mwaka wa fedha 2012/13 na kesi 2,874 zilizosajiliwa kabla ya kipindi hicho. Kiwango hiki ni kidogo na hakiridhishi kwa sababu hiyo, Wizara yangu kupitia Mahkama inachukua hatua za kufanya mabadiliko yatakayoongeza ufanisi wa kazi za Mahkama. Miongoni mwa juhudi hizo ni kuharakisha uendeshaji wa kesi ili haki za walalamikaji na walalamikiwa zipatikane kwa wakati, kwani kuichelewesha haki ni kuikataa. Kamati maalum imeundwa kushughulikia uharakishwaji wa kesi na Kamati hiyo imefanya vikao viwili katika mwaka 2012/13, kujadili mbinu zinazoweza kusaidia kupunguza muda wa kuendesha kesi. Hatua nyengine ni kuanzishwa Mahkama za kushughulikia mambo maalum kama ilivyo kwa Mahkama ya Watoto na Mahkama ya Biashara na kuongeza idadi ya mahakimu. Katika mwaka huu wa fedha 2012/13 Mahkama imeajiri wafanyakazi zaidi ya 30, wakiwemo Mahakimu.

Mhe. Spika, Mahkama ya Watoto ilizinduliwa mwezi Februari 2013 kwa ajili ya kushughulikia mashauri yanayohusu watoto. Tangu kuanza kazi Mahkama hiyo imemaliza kesi saba na kuzitolea uamuzi kati ya kesi 56 zilizoanza kusikilizwa.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo, Mahkama imeipitia Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985. Rasimu ya sheria hiyo imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu hivi karibuni. Kupitishwa kwa sheria hiyo kutaleta mabadiliko makubwa ya utendaji wa Mahkama ya Kadhi.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine Mahkama imewajengea uwezo baadhi ya Majaji na Mahakimu kwa kuwawezesha kushiriki katika mikutano, makongamano na semina Tanzania Bara, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Afrika ya Kusini. Aidha, Mahkama imewapatia nafasi ya kuongeza elimu wafanyakazi wa Unguja na Pemba, katika ngazi ya stashahada na cheti kwenye fani za sheria, uongozi na kompyuta.

Mhe. Spika, katika kuelimisha jamii, Mahkama imeendelea kurusha vipindi vya elimu kupitia *ZBC* ambapo vipindi vinne vya televisheni na vitatu vya redio vimetolewa. Vile vile, toleo la kwanza la Jarida la Mahkama limechapishwa na kusambazwa kwa wasomaji. Uzinduzi wa jarida hilo umefanywa kwenye maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar, tarehe 7/2/2013. Aidha, Mahkama imefanya mikutano minne ya hadhara kuzungumza na wananchi katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Mahkama iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 3,145,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 600,000,000.00 kwa kazi za maendeleo kutoka serikalini. Vile vile, jumla ya Shilingi 72,000,000.00 zilikadiriwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2013, Shilingi 1,657,639,000.00 (70%) zilitumika kulipia mishahara na stahiki nyingine za watumishi, na Shilingi 344,843,836.00 (43%) kwa matumizi mengineyo. Kwa kazi za maendeleo, Shilingi 100,000,000.00 (17%) zilipatikana. *Angalia Kiambatanisho Nam. 1&3.*

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/14 Mahkama imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kupunguza mrundikano wa kesi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa haki.
ii. Kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahkama Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ili Mahkama iweze kutekeleza malengo yake mwaka 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 3,583,000,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida, zikiwemo Shilingi 2,350,100,000.00 za mishahara na Shilingi 1,232,900,000.00 za matumizi mengine. Vile vile, naomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 150,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, Mahkama inatarajia kuchangia Serikalini mapato ya Shilingi 90,000,000.00. *Angalia Viambatanisho Nam. 2&3.*

AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Afisi ya Mwanasheria Mkuu (AMM) ni kuishauri Serikali kwa mambo yote ya kisheria. Katika kutekeleza wajibu huo AMM inafanya kazi ya kutayarisha miswada ya sheria, kusimamia kesi na mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa hati na nyaraka za kisheria, kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mikataba ya serikali na kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi za serikali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, AMM imetayarisha miswada 10 ya sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi. *Angalia Kiambatanisho Nam. 6*.

Aidha, AMM imeandaa na kuchapisha matangazo 81 ya kisheria na kanuni 20 za sheria mbali mbali na imesimamia mikataba 23 kwa ajili ya Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali. Wakati huo huo, Afisi inaendelea kusimamia kesi 45 za madai zilizofunguliwa dhidi ya Serikali.

Mhe. Spika, AMM imeandaa mikakati ya uimarishaji wa usimamizi wa kesi za madai za Serikali kwa kukutana na watendaji wakuu wa baadhi ya taasisi za umma kujadili suala hilo. Hatua inayofuata ni kujiimarisha zaidi katika usimamizi wa kesi.

Mhe. Spika, pamoja na kazi hiyo, AMM imepanga kuziweka pamoja na kuzichapisha sheria za Zanzibar. Kazi hivyo imeshaanza siku za nyuma. Kwa mwaka 2013/14, AMM imekusudia kuzishughulikia sheria za mwaka 1980 – 2010. Afisi imekamilisha mazungumzo na kampuni za uchapishaji sheria za *Law Africa* ya Kenya na *Law Publisher* ya India ili kuangalia uwezekano wa kuzichapisha sheria zote katika mfumo wa elekroniki na karatasi. Kazi hiyo ikikamilika Zanzibar itakuwa na toleo jipya la Sheria za Zanzibar. Toleo la mwisho kama hilo lilitoka mwaka 1958.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine, AMM imekamilisha kazi ya upembuzi wa sheria ili kubaini sheria zinazotumika na zisizotumika na sasa imo katika maandalizi ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Zisizotumika. Vile vile, AMM inaendelea kuandaa Sheria mpya kuchukua nafasi ya baadhi ya sheria za zamani za Kiingereza zilizoanza kutumika wakati wa ukoloni na ambazo sasa zimepitwa na wakati. Wataalamu wanaofanya kazi hiyo wamekamilisha hatua za awali. Hatua iliyobaki itakamilika mwaka wa fedha 2013/14. Sheria zinazofanyiwa kazi ni Sheria ya Hati ya Uwakala (*Power of Attorney Act*), Sheria ya Wasimamizi wa Amana na Wasii (*Trustees Act*), na Sheria ya Tafsiri na Masharti ya Jumla Namba 7/84, (*Interpretation and General Clauses Act*) na Sheria ya Kusimamia Hundi *(Bill of Exchange Act).* Aidha,

Afisi inakusanya na kuyaweka pamoja magazeti rasmi ya serikali kutoka 1910 hadi 1963, ili kuzihifadhi kumbukumbu muhimu zilizomo kama vile kumbu kumbu za vikao vya Baraza la Kutunga Sheria za wakati huo (*LEGCO*).

Mhe. Spika, ili kuimarisha utaratibu wa kazi ya kuandaa Miswada ya Sheria, AMM imeandaa Muongozo wa Uandaaji wa Miswada. Muongozo huo ambao uko katika hatua za mwisho kukamilishwa, utaweka bayana taratibu za kuandaa miswada. Aidha, muongozo utaweka mfumo mmoja wa uandishi wa miswada, kulingana na aina za miswada.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, AMM imetimiza moja kati ya malengo muhimu kwa kukamilisha Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo ilipitishwa na Baraza hili kwa kauli moja. Utekelezaji wa sheria hiyo utaanza baada ya taratibu zinazohusika kukamilika. Afisi tayari inayo dira na mpango kazi wa utekelezaji wa sheria hiyo.

Mhe. Spika, katika kujenga uwezo kiutendaji, AMM imeajiri wafanyakazi 12 wakiwemo wanasheria wapya sita na wengine wanne wamepatikana kutoka taasisi nyengine za Serikali ili kuongeza ufanisi. Vile vile Afisi imewapatia nafasi za masomo wafanyakazi wawili katika ngazi ya Shahada na mmoja ngazi ya Stashahada. Aidha, wafanyakazi watatu wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi kuhusu Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi na watano wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi Afirika ya Kusini, juu ya udhibiti wa fedha haramu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13 AMM iliidhinishiwa jumla ya shillingi 802,000,000.00 zikiwemo Shilingi 197,000,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 605,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kufikia Machi 2013, jumla ya Shilingi 170,885,550.00 (87%) zilipatikana kwa ajili ya mishahara na Shilingi 264,545,421.00 (44%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, kwa kazi za maendeleo, ziliidhinishwa jumla ya shilingi 1,800,000,000.00 na kupatikana shilingi 844,289,230.00 (47%). *Angalia Kiambatanisho Nam. 1*.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/14, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha utekelezaji wa mpango mpya wa Afisi chini ya Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu;
ii. Kutekeleza Mikakati ya Utekelezaji wa Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu;
iii. Kukamilisha Matayarisho ya Toleo jipya la Sheria za Zanzibar na kulichapisha;

iv. Kuimarisha Uwezo wa Watendaji; na
v. Kukamilisha ujenzi na kuhamia kwenye Jengo Jipya la Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, ili AMM iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 919,000,000.00 kwa kazi za kawaida zikiwemo Shilingi 245,400,000.00 za mishahara na 673,600,000.00 za matumizi mengine.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria (TKS) Zanzibar ina jukumu la kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yake. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume inatekeleza shughuli mbali mbali ikiwemo kufanya utafiti unaowashirikisha wananchi katika mchakato wa kupitia Sheria. Aidha, Tume inatoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Zanzibar ili kuwaongezea uelewa. Lengo la kupitia hatua hizo ni kutunga sheria ambazo zinahusisha wananchi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Tume imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida kwa kuzipitia sheria nne zifuatazo:- Sheria ya Vileo Sura 163, Sheria ya Mifugo Na. 11/1999, Sheria ya Mikataba Sura 149/1917 na Sheria ya Usafirishaji Bidhaa kwa njia ya Bahari Sura 155/1926. Kufikia sasa, kazi ya kuipitia Sheria ya Vileo imekamilika na kazi ya kupitia Sheria ya Usafirishaji Bidhaa kwa Njia ya Bahari na Sheria ya Mikataba inaendelea.

Mhe. Spika, pamoja na kazi hiyo, tume inaendelea kufanya uchambuzi kwa ajili ya kubaini Sheria zinazohitaji kufanyiwa mapitio ili kuisaidia Tume katika kuandaa Mpango Kazi na kuiwezesha Serikali kujua mahitaji yaliyopo ya kazi ya kupitia sheria, na kusaidia upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika kwa kazi hiyo.

Mhe. Spika, ili kuzitekeleza vyema kazi zake, TKS imeendelea kuimarisha mashirikiano na taasisi zenye majukumu sawa ndani na nje ya nchi. Katika kufanikisha suala hilo, Tume imefanya mawasiliano na Tume za Kurekebisha Sheria katika baadhi ya nchi za Afrika na taasisi za kimataifa zinazojumuisha Tume za Kutunga Sheria. Katika harakati hizo, Tume imejiunga na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Afrika Mashariki na Kati (*Association of Law Reform Agencies of Eastern and Southern Africa - ALRAESA*), na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Jumuiya ya Madola (*Commonweath Association of Law Reform Agencies - CALRAs).* Kupitia taasisi hizo, Tume

inapata uzoefu na kujifunza mbinu mpya za kufanyia kazi na kuongeza ufanisi na uwiano katika utendaji.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, Tume imefanya mapitio ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria. Hatua hiyo imechukuliwa ili kuleta mabadiliko ya msingi katika Muundo na shughuli za Tume. Rasimu ya Sheria hiyo imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa Wizarani kwa hatua zaidi. Vile vile, ili kuwajengea uwezo watendaji, Tume imewapatia wafanyakazi watatu (3) mafunzo ya muda mfupi kuhusu "*Computer Crime*", na Uandishi wa Sheria nchini Afrika ya Kusini, India na Korea. Aidha, wafanyakazi wawili (2) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, Afisi imetoa mafunzo kwa umma kuhusu matumizi ya Sheria za Zanzibar. Jumla ya vipindi vinane vya televisheni na 12 vya redio vimerushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) na Semina kuhusu mapitio ya Sheria zimefanywa kwa wadau wakiwemo Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Walimu, Wanafunzi, Madaktari, Polisi, Masheha, Wanasheria wa kujitegemea, Wanasheria wa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS), na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (*ZLSC*) pamoja na wanajamii.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, TKS iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 271,000,000.00 kwa matumizi yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi 94,000,000.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 177,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Fedha zilizopatikana hadi kufikia Machi 2013 ni Shilingi 101,233,200 kwa ajili ya kulipa mishahara na stahiki nyengine za watumishi na Shilingi 98,538,620.00 kwa matumizi mengineyo. Vile vile, jumla ya Shilingi 145,000,000.00 ziliidhinishwa kwa kazi za maendeleo kutoka Serikalini. Kufikia Machi 2013 Shilingi 73,280,000.00 (50.5%) zilipatikana. *Angalia Kiambatanisho Nam. 1.*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo;

i. Kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar zifuatazo; *Limitation Decree Cap 12/1917, The Penal Decree Cap 13/1934, The Legal Practitioners Decree Cap 28 1941, The Notaries Public Decree Cap 29/1948;*

ii. Kutoa elimu kwa Umma*;*

iii. Kuimarisha Utendaji wa Kazi za Tume; na

iv. Kuimarisha Ushirikiano na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume za ndani na za kimataifa.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2013/14, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 483,000,000.00 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 147,000,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 336,000,000.00 kwa matumizi mengine.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ndio msimamizi mkuu wa mashtaka yote ya jinai Zanzibar kwa ajili ya upatikanaji wa haki kwa raia. Afisi imeendelea kusimamia kesi zinazoendelea kusikilizwa mahakamani, kufungua kesi mpya na kutoa ushauri juu ya masuala yanayohusu mashtaka na haki za jinai.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imetekeleza kazi za kawaida kwa ufanisi. Afisi imeendelea kusimamia kesi za jinai na kutoa ushauri wa kiufundi kwa Jeshi la Polisi na taasisi mbali mbali za Serikali pamoja na raia. Jumla ya kesi za jinai 2,051 zimefunguliwa katika Mahkama za Zanzibar katika ngazi tofauti na majalada ya uchunguzi wa jinai 409 kutoka kwa Jeshi la Polisi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Vile vile, jumla ya wananchi 576 waliokuwa wakihitaji huduma ya ushauri wa haki ya jinai wamehudumiwa.

Mhe. Spika, Afisi imeendelea kujenga mashirikiano baina ya vyombo vinavyosimamia masuala ya jinai ili kuongeza ufanisi. Mikutano 13 kati ya waendesha mashtaka na wapelelezi imefanyika. Mikutano hiyo imesaidia kujenga ukaribu baina ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na taasisi zinazohusika na uendeshaji wa mashtaka, zikiwemo Jeshi la Polisi, Mahkama, Mawakili wa Utetezi na jamii kwa jumla. Vile vile, Afisi imeandaa mikutano minane ya wadau wa jinai, zikiwemo baadhi ya taasisi za umma kama vile Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) na Baraza la Manispaa ya Zanzibar. Aidha, Afisi imetoa mafunzo kwa wadau mahsusi, yaani Halmashauri za Wilaya, Mahkama za Mwanzo na Masheha.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/13 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilikusudia kukamilisha kazi ya kuweka mfumo wa uendeshaji mashtaka kiraia katika Wilaya ambazo bado Polisi wanaendesha mashtaka. Katika kutekeleza jukumu hilo, Afisi imeajiri wanasheria wapya watano ili kuwapeleka kwenye Wilaya hizo. Mpaka sasa uendeshaji wa mashtaka kiraia unafanyika katika Mahkama nne za Wilaya ambazo ni Mjini, Magharibi, Chake Chake na Mkoani. Tunatarajia kuwa uendeshaji mashtaka kiraia utafanyika kwenye Wilaya zilizobakia, Unguja na Pemba. Afisi imeanza kutayarisha makaazi

kwa ajili ya kuwaweka Waendesha Mashtaka watakaopangiwa kufanya kazi kwenye vituo vya Makunduchi na Mkokotoni.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeanza kazi ya kufanya utafiti wa sheria zinazohusu makosa ya jinai. Pamoja na kazi hiyo, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeanza kuupitia muongozo wa mashtaka ili kuufanyia marekebisho uendane na mahitaji yaliyopo. Wakati huo huo, Afisi imo katika hatua ya kusambaza Kanuni za Maadili ya Waendesha Mashtaka.

Mhe. Spika, Afisi kupitia Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria inaendelea kutoa mafunzo ya usimamizi wa sheria kwa watendaji mbali mbali wakiwemo wanasheria na watendaji wengine wa Serikali na taasisi binafsi. Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa na kituo hicho ni Uandishi wa Sheria (*Legislative Drafting*), Usimamizi wa Sheria za Kazi (*Labour laws Implementation Training*), Uandishi wa Miradi (*Project Write-up*) na ufundi maalum wa Uandishi wa Mikataba *(Contract Drafting and Negotiation Skills*). Chuo kiko katika hatua za awali za kuanzisha mashirikiano na taasisi za kimataifa ili kujenga na kuimarisha uwezo wake. Baraza la Uongozi wa Chuo tayari limezinduliwa na limeanza kazi kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, wafanyakazi 35 wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamepatiwa mafunzo katika nyanja mbali mbali zikiwemo Sheria, Utawala na uwekaji kumbukumbu; kati yao wanaume ni 28 na wanawake ni 7. Aidha, baadhi ya wanasheria wameshiriki katika semina mbali mbali na mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, katika kuelimisha jamii kuhusu haki za jinai, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeandaa na kurusha hewani vipindi tisa kwa njia ya redio, na jarida la Shahidi limeendelea kutolewa na kusambazwa kwa wadau.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,229,000,000.00/= kwa matumizi mbali mbali. Kati ya hizo shilingi 411,000,000.00/= zilitengwa kwa ajili ya mishahara na maslahi mengine ya watumishi, shilingi 468,000,000.00/= kwa matumizi mengineyo, shilingi 250,000,000.00/= kwa kazi za maendeleo na shilingi 100,000,000.00/= za ruzuku.

Hadi kufikia Machi 2013, fedha zilizopatikana ni shilingi 434,418,950.00/= (106%) kwa mishahara na stahiki za watumishi; shilingi 277,164,290.00/= sawa na asilimia (59%) kwa matumizi mengineyo; shilingi 100,000,000.00/= (40%) kwa matumizi ya kazi za maendeleo na shilingi 43,900,000.00/= (44%)

ni ruzuku kwa ajili ya kuendeshea shughuli za chuo. Angalia Kiambatanisho Nam. 1.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imejiwekea malengo yafuatayo kwa mwaka wa fedha 2013/14:-

i. Kukuza uwezo wa Afisi;
ii. Kukuza na kuimarisha kazi za uendeshaji mashtaka;
iii. Kukuza uwezo wa raslimali watu; na
iv. Kuendeleza uendeshaji mashtaka kiraia.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,103,000,000.00/= kwa kazi za kawaida, zikiwemo shilingi 612,000,000.00/= za mishahara na shilingi 491,000,000.00/= za matumizi mengineyo, shilingi 150,000,000.00/= kwa kazi za Maendeleo, na ruzuku ya shilingi 80,000,000.00/= kwa ajili ya kuendeshea Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria.

AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Ofisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhima kisheria ya kutoa miongozo kuhusu masuala ya kidini kwa Zanzibar. Ofisi ya Mufti katika mwaka wa fedha wa 2012/13, imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa malengo yake ya kibajeti, yakiwemo kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu kama vile mikutano ya Baraza la Ulamaa, Mikutano ya Kamati ya Kuandama kwa Mwezi, Ziara za Misikiti na Madrassa; na kutatua migogoro na kushajiisha amani na utulivu.

Mhe. Spika, katika utekelezaji Ofisi ya Mufti imesimamia uzinduzi wa Baraza la Ulamaa uliofanyika Januari 2013. Baraza hilo limefanya mikutano miwili. Vile vile, Ofisi ya Mufti imeandaa na kusimamia vikao vya Kamati ya kuthibitisha kuandama kwa mwezi na kutoa taarifa kwa umma. Jumla ya vikao sita vimefanyika.

Kazi nyengine ambayo Ofisi ya Mufti imeifanya ni kuzitembelea madrassa na Misikiti. Jumla ya madrassa 83 na Misikiti 43 imetembelewa Unguja na Pemba. Kwenye ziara hizo ushauri na maelekezo mbali mbali yametolewa kwa viongozi wa Misikiti na madrassa. Katika jitihada zake za kuwa na takwimu sahihi za madrassa na Misikiti, Ofisi ya Mufti imesajili jumla ya madrassa 210 kati ya madrassa 2431 na Misikiti 254 kati ya Misikiti 2017 iliyopo Zanzibar. Kazi hii itaendelea kwa mwaka 2013/14.

Mhe. Spika, katika jitihada za kudumisha amani, Ofisi ya Mufti imefanya mikutano kadhaa na Jumuiya zinazohusishwa na matukio ya uvunjifu wa amani. Vile vile, Ofisi imepokea migogoro 51 ya ndoa na mmoja wa Msikiti. Migogoro 43 ya ndoa kati ya hiyo iliyopokelewa imepatiwa ufumbuzi, mitano imepelekwa Mahakamani na minne inafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, katika kujenga mahusiano baina ya taasisi za kidini nchini, Ofisi ya Mufti imefanya mikutano na baadhi ya Jumuiya za Kiislamu Unguja na Pemba. Masuala kadhaa yalijadiliwa kwenye mikutano hiyo likiwemo suala la kupiga vita vitendo vya hujuma dhidi ya viongozi wa kidini.

Aidha, Ofisi ya Mufti kwa mashirikiano na Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu, imefanya matembezi ya hiyari kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Jumuiya zenye vituo vya kuwatibu watumiaji wa madawa ya kulevya *Sober Houses*, na kuvitembelea mara nne vituo hivyo ili kutoa mawaidha kwa vijana wanaopata huduma ya vituo hivyo.

Mhe Spika, Ofisi ya Mufti imeendelea na utaratibu wake wa kudumisha uhusiano wa kimataifa. Ofisi imepokea wageni kutoka nchi mbali mbali, wakiwemo Sheikh kutoka Misri na viongozi wa dini kutoka Iran, Iraq, Marekani, Ujerumani, Newzeland, Ufaransa, Uturuki na Kenya. Vile vile, kwa kushirikiana na Ubalozi wa Saudi Arabia, Ofisi ya Mufti inaratibu msaada wa ujenzi wa Misikiti minne kisiwani Pemba. Ofisi pia imepata msaada wa mafunzo kuhusu njia bora za kulingania dini ambapo vijana 14 wa Zanzibar watapatiwa mafunzo hayo nchini Misri na India.
Mhe Spika, Ofisi ya Mufti imeendelea na utamaduni wake wa kutoa elimu kwa umma kwa njia ya redio. Vipindi vya masuala na majibu vimeendelea kutolewa ambapo jumla ya masuala 210 yamejibiwa kupitia vyombo vya habari (*ZBC*). Aidha, Ofisi imepokea watu 378 waliofika kutaka ufafanuzi wa mambo mbali mbali ya kisheria. Mbali na hatua hiyo, vipindi 14 vya nasaha na mawaidha ya dini vimetolewa kuhusu mambo yanayoiathiri jamii wakati huu, yakiwemo ubaya wa rushwa na riba. Aidha, muongozo wa kusheherekea sikukuu za Kiislamu umetolewa kupitia vipindi hivyo.

Mhe. Spika, katika kuimarisha nyenzo za taaluma, Ofisi imeanzisha Maktaba ya Kiislam na sasa imo katika jitihada za kutafuta vitabu zaidi kuimarisha maktaba hiyo. Katika hatua nyengine, Ofisi ya Mufti imeendelea kutekeleza mpango wa kutoa elimu ya kupambana na UKIMWI kwa mbinu za Kiislamu. Ofisi imefanya semina ya kuwaelimisha zaidi wafanyakazi wake kuhusu njia za udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI. Katika kuwajengea uwezo watendaji wake kitaaluma, Ofisi imempatia fursa ya kujiendeleza mfanyakazi mmoja katika ngazi ya Stashahada.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi ya Mufti wa Zanzibar iliidhinishiwa jumla ya shilingi 338,324,000.00/=. Kati ya hizo, shilingi 235,298,000.00/= zilitengwa kwa malipo ya mishahara na stahiki nyengine za watumishi, na shilingi 103,026,000.00/= kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2013, zilipatikana shilingi 159,786,000.00/= (68%) kwa kulipa mishahara na shilingi 40,562,700.00/= (39%) kwa matumizi mengineyo. Angalia Kiambatanisho Nam. 1.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Ofisi ya Mufti imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha uratibu wa shughuli za dini; na
(ii) Kuongeza uwezo wa Afisi kiutendaji

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Mufti wa Zanzibar itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 485,666,000.00 kwa kazi za kawaida, zikiwemo Shilingi 302,639,000.00 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 183,027,000.00 kwa matumizi mengineyo.

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI

Mhe. Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (*The Business and Property Registration Agency - BPRA*) ndio yenye jukumu la kusimamia masuala ya usajili unaohusu taasisi za biashara, tasnia ya mali za ubunifu, pamoja na usajili wa nyaraka mbali mbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar. Ofisi hii mpya imeasisiwa baada ya kupitishwa kwa sheria ya Kuanzishwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar Na. 13 ya 2012, ambayo imefuta Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine, *BPRA* imeendelea na kazi za usajili. Katika kipindi cha miezi tisa katika mwaka wa fedha 2012/13, *BPRA* imesajili jumla ya kampuni 105, majina ya biashara 281, alama za biashara 513, *NGO's* 82 na nyaraka za aina mbali mbali 608.

Mhe. Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imefanya mikutano na wadau mbali mbali wakiwemo *ZRB, ZIPA, TRA*, Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Kamisheni ya Utalii Zanzibar, kujadili hali ya mifumo ya usajili, na jinsi inavyoweza kusaidia taasisi hizo katika kufanikisha shughuli zake.

Aidha, katika mwezi wa Novemba *2012 BPRA* iliandaa mkutano wa Baraza la Utawala (*Administrative Council)* la *ARIPO*. Zaidi ya nchi 25 na mashirika kutoka ndani na nje ya Afrika zilishiriki mkutano huo. Wakala wa Usajili wa

Biashara na Mali pia ilishiriki mikutano mbali mbali ya kiutendaji iliyofanyika nchini Tanzania, Norway na Switzerland pamoja na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mikutano hiyo ilijadili mambo mbali mbali ikiwemo usajili na kubadilishana taarifa za makampuni baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, katika kujenga uwezo wa kiutendaji, wakala imefanya semina elekezi kwa wafanyakazi wake na kuandaa mikutano ya wadau kwa ajili ya kuitambulisha sheria mpya ya wakala pamoja na sheria nyengine zinazoongoza shughuli za usajili Unguja na Pemba. Vile vile, wakala imewasomesha wafanyakazi watano, katika kiwango cha Shahada ya Kwanza ya Sheria, Stashahada ya Utunzaji Nyaraka, na watatu mafunzo ya muda mfupi ya udereva, kompyuta (*Oracle database Administrator)* na Usimamizi wa Tasnia za Mali Ubunifu.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, wakati huo ikiitwa Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya shilingi 265,673,000.00/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 115,674,000.00/= zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 149,999,000.00/= kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2013 zimepatikana shilingi 94,646,950.00/= (82%) kwa ajili ya mishahara na shilingi 75,777,000.00/= (51%) kwa matumizi mengineyo.

Aidha, shilingi 100,000,000.00/= ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kutoka serikalini. Kati ya hizo zimepatikana shilingi 40,000,000.00/= (40%). Vile vile, Ofisi ilikadiria kukusanya shilingi 195,000,000.00/=. Kufikia Machi 2013, zimekusanywa shilingi 102,554,010.00/= (53%). Angalia Viambatanisho Nam. 1,3 na 7.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa ajili ya kutoa huduma bora;
ii. Kuandaa kanuni za sheria za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, Usajili kwa Taasisi za Biashara pamoja na Usajili wa Dhamana za Mali zinazohamishika; na
iii. Kuendeleza uwekaji wa mifumo ya kisasa ya usajili na utoaji huduma.

Mhe. Spika**,** ili kuiwezesha Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 289,006,000.00/= kwa kazi za kawaida zikiwemo shilingi 139,008,000.00/= za mishahara na shilingi 149,998,000.00/= za matumizi mengineyo na shilingi

100,000,000.00/= kwa kazi za maendeleo. Aidha, Afisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali inakadiria kukusanya mapato ya shilingi 125,700,000.00/=. Angalia Viambatanisho Nam. 2 na 3.

AFISI YA MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO:
Mhe. Spika, Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, kisheria ina majukumu ya kusajili Vizazi na Vifo na kutunza kumbukumbu zitokanazo na usajili huo. Mbali na hayo, Ofisi ina jukumu la kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Usajili wa Vizazi na Vifo, kuelimisha jamii na kutoa mafunzo kuhusu usajili kwa watendaji na mawakala wa usajili, wakiwemo watendaji wa Afya, Masheha na viongozi wa dini.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/13 imesajili jumla ya vizazi 31,540 wakiwemo wanaume 15,930 na wanawake 15,610, Unguja na Pemba. Vile vile, Afisi imesajili vifo 1,885 vikiwemo vya wanaume 1,072 na wanawake 813, Unguja na Pemba. Takwimu hizo zinabainisha vifo kuandikishwa kwa idadi ndogo. Tatizo hilo linasababishwa na mwamko mdogo wa jamii na ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuandikisha vifo.

Wizara yangu kwa mwaka 2013/14 imepanga kutoa elimu kwa jamii ili kuhamasisha uandikishaji wa vizazi na vifo. Kwa kuanzia napenda kutoa wito kwa Wajumbe wa Baraza lako walichukulie suala la uandikishaji wa vizazi na vifo kwa usawa na umuhimu mkubwa, na wasaidie kuwaelimisha wananchi katika maeneo yao juu ya umuhimu huo.

Mhe. Spika, usajili wa vizazi na vifo umekuwa na matatizo mengi kwa muda mrefu na unaleta usumbufu wa mara kwa mara kwa watu wanaohitaji huduma ya vyeti vya kuzaliwa. Ukosefu wa magamba ya kuchapishia vyeti, uwezo mdogo wa uchapaji na ukosefu wa fedha ndiyo matatizo ya msingi yanayosababisha hali hiyo. Hata hivyo, Wizara yangu imefanya jitihada za kulipunguza tatizo hilo kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali, kama vile Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali.

Mhe. Spika, pamoja na hatua hizo, Wizara yangu imeanza kutekeleza mpango wa muda mrefu wa kuondokana na tatizo hilo kwa kufanya marekebisho ya mfumo wa usajili kwa kutumia kompyuta. Majaribio ya mfumo huo yamepangwa kufanyika katika mwaka 2013/14 kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi ili kuuwezesha mfumo huo kufanya kazi, hatua kadhaa zimefikiwa.

Rasimu ya Sheria ya Usajili wa Matukio ya Kijamii imekamilika na imefikia hatua ya kujadiliwa Baraza la Mapinduzi. Hatua nyegine ni kutoa mafunzo

kwa Mawakala wa Usajili Wilaya za Mjini na Magharibi, na kuingiza taarifa za miaka ya nyuma kwenye kompyuta ili kusaidia uwekaji kumbukumbu na upatikanaji wa vyeti kwa haraka. Hatua itakayofuata ni kutoa mafunzo kwa mawakala wa usajili kwenye Wilaya zilizobakia, kutoa elimu kwa umma, kuweka miundombinu ya mfumo wa mawasiliano na kuajiri maafisa usajili wa Wilaya.

Mhe. Spika, katika maandalizi ya mfumo mpya wa usajili Wilayani, AMVV imeanza kazi ya matengenezo na marekebisho ya Ofisi za Usajili za Wilaya. Matengenezo hayo yamekamilika katika Ofisi za Wilaya ya Kusini, Kati, Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B' Unguja. Matengenezo kama hayo yataendelea kwa Wilaya zilizobaki. Aidha, chumba kimoja kwenye Ofisi Kuu, Forodhani, kimefanyiwa matengenezo makubwa ili kuweka '*server computer'* ambayo itakuwa ndiyo kituo kikuu cha taarifa zote za vizazi, vifo, ndoa na talaka.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13, Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 305,159,000.00/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 134,222,000.00/= zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 170,937,000.00/= kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, fedha zilizopatikana ni shilingi 79,559,600.00/= (59%) kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 72,124,492.00/= (42%) kwa matumizi mengineyo.

Aidha, jumla ya shilingi 400,000,000.00/= ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo kutoka serikalini na zilipatikana jumla ya shilingi 262,732,297.00/= (66%). Ofisi pia ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 180,000,000.00/= na kufikia Machi 2013, shilingi 105,333,550.00/= (59%) zilikusanywa. Angalia Kiambatanisho Nam. 1 na 3.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma;
ii. Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji; na
iii. Kufanya mageuzi ya mfumo wa usajili na utoaji wa vyeti.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 353,460,000.00/= kwa matumizi ya kawaida; kati ya hizo shilingi 145,221,000.00/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 208,239,000.00/=, kwa matumizi mengineyo. Vile vile, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya shilingi 300,000,000.00/= kwa kazi za maendeleo na

makusanyo ya shilingi 219,300,000.00 kuchangia mfuko mkuu wa Hazina. Angalia Viambatanisho Nam. 2 na 3.

AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

Mhe. Spika, Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar ina dhima kisheria ya kuhakikisha hali, hadhi na maslahi ya wabunifu wa Zanzibar yanaimarika kwa kuthaminiwa na kupatiwa malipo yanayotokana na matumizi ya kazi zao kibiashara. Vile vile, Ofisi ya Hakimiliki inahusika na usimamizi na utendaji kisheria wa mfumo wa hakimiliki kitaifa na kimataifa. Jukumu hilo linatekelezwa kwa kusajili kazi za hakimiliki, kutoa leseni kwa matumizi halali ya kazi hizo kibiashara, pamoja na kukusanya na kugawa mirabaha kwa wabunifu waliosajili kazi zao.

Mhe. Spika, Ofisi ya Hakimiliki ni Wakala wa Wenye Hakimiliki zilizosajiliwa. Mojawapo ya kazi zake muhimu ni kukukusanya na kugawa mirabaha. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, jumla ya shilingi 37,648,000.00/= zilikusanywa. Utaratibu wa kugawa mirabaha kwa wabunifu 726 wa muziki, kasida, mawaidha na filamu waliosajiliwa na Ofisi zimekamilika na ugawaji utafanyika hivi karibuni.

Mhe. Spika, katika kutekeleza lengo lake la kupunguza uharamia wa kazi za hakimiliki, Afisi imeimarisha uwezo wa kiutendaji kwa Dawati la Hakimiliki la Jeshi la Polisi na Waendesha Mashtaka. Mafunzo juu ya masuala ya Hakimiliki yametolewa kwa Kikundikazi cha Askari Polisi wa Mikoa, Waendesha Mashtaka na Maafisa Kodi. Pia kwa kushirikiana na Shirika la Milki Ubunifu Ulimwenguni (*WIPO*) yalifanyika mafunzo ya utambuzi wa jinai za hakimiliki kwa Jeshi la Polisi, mahakimu na maofisa kodi.

Mhe. Spika, Ofisi pia inatoa taaluma kwa wabunifu, watumiaji wa kazi za hakimiliki, pamoja na kutoa taarifa za kitaalamu kwa umma, taasisi za umma na taasisi binafsi kuhusiana na masuala ya hakimiliki. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2013, jumla ya vipindi 28 vya redio na 31 vya televisheni vilirushwa hewani. Pia, Ofisi imetoa elimu ya ana kwa ana kwa watu 22, wakiwemo wanafunzi wa sekondari 15 na wanafunzi saba wa vyuo ambao wanafanya utafiti.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki imewapatia mafunzo watendaji watatu. Mfanyakazi mmoja anasoma Shahada ya pili katika fani ya "*Development Policy*", Morogoro, mmoja amehudhuria mafunzo ya "*Cyber Crime*" nchini Korea, mmoja amehudhuria mafunzo Dar es Salaam kuhusu *"Practical Approaches to Intellectual Property Utilisation and Protection in Africa".*

Mhe. Spika, ili kujiimarisha kiutendaji, Ofisi ya Usajili wa Hakimiliki inaipitia Sheria ya Hakimiliki Namba 14 ya mwaka 2003, kwa ajili ya kuifanyia marekebisho. Rasimu ya mwanzo imekamilika na sasa imeanza kujadiliwa na Wataalamu wa Shirika la Milki Ubunifu (*WIPO)* na baadae itajadiliwa na wadau wa Hakimiliki wa ndani ya nchi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iliidhinishiwa ruzuku ya shilingi 120,000,000.00/=; shilingi 39,548,800.00/= kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 80,452,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2013, fedha zilizopatikana ni shilingi 50,747,850.00/= (128%) kwa ajili ya mishahara na Shilingi 32,187,000.00 (40%) kwa matumizi mengineyo. Angalia Kiambatanisho Nam. 1.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Afisi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Hakimiliki;
(ii) Kupunguza uharamia wa kazi za hakimiliki; na
(iii) Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Hakimiliki iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 140,000,000.00/= kwa matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi 63,347,000.00/= kwa mishahara na shilingi 76,653,000.00/= kwa matumizi mengineyo.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina jukumu la kusimamia masuala yote yanayohusu mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Idd Kitaifa, Hijja, Zakka na Misaada ya Kheri.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu hayo Kamisheni iliweka lengo la kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji na ugawaji wa Zakka katika mwaka 2012/13. Katika kufanikisha suala hilo elimu ya zakka imetolewa kupitia semina nne kwa mikoa ya Unguja, ziara za vikundi 118 na wajasiriamali 20 Unguja na Pemba, na vipindi vitatu vya TV.

Aidha, vitabu 135 vya muongozo wa zakka na vipeperushi 200 vimegaiwa. Ofisi imefanya na kukamilisha uchambuzi wa mahitaji ya utendaji na uimarishaji wa kumbukumbu za zakka. Jumla ya shilingi 321,807,200.00/= za zakka zimegaiwa na shilingi 2,100,000.00/= zilikusanywa. Aidha, misaada ya

kheri yenye thamani ya shilingi 930,000.00/= kutoka *Baitulmali* na wachangiaji mbali mbali imetolewa. *Angalia* Kiambatanisho Nam. 8a.

Mhe. Spika, katika kuendeleza mfumo bora wa usimamizi wa Mali za Wakfu na Amana, Kamisheni imeandaa Muongozo wa Wakfu; imefanya vikao 33 vya uelimishaji na uhamasishaji, na kutoa vipindi viwili vya TV, kipindi kimoja cha Radio na makala mbili katika gazeti. Vile vile, Kamisheni imo katika hatua za awali za kuanzisha *database.*

Mhe. Spika, Kamisheni imeendeleza utafiti, uhakiki na utekelezaji wa nyasia na wakfu, pamoja na ukusanyaji wa kodi za wakfu, amana na ada. Matokeo ya kazi hizo ni kupatikana kwa nyaraka 40; kutekelezwa kwa nyasia 20 kwa jumla ya shilingi 46,215,344.90/=; na kusajiliwa kwa nyakfu tisa mpya. Aidha, jumla ya shilingi 217,325,360.00/= zimekusanywa kutokana na kodi ya nyumba za Wakfu, shilingi 27,074,000.00/= kutokana na Mali za Amana; shilingi 3,688,000.00/= mashamba; na shilingi 790,000.00/= kwa ada za mikataba 79.

Mhe. Spika, katika kufanya ukaguzi, hifadhi na uendelezaji wa nyumba na mashamba ya Wakfu na Amana, jumla ya nyumba 157 na mashamba tisa yamekaguliwa, nyumba 10 na Msikiti mmoja zimefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 65,502,000.00/=, na miche 100 ya minazi imepandwa katika mashamba ya Wakfu.

Mhe. Spika, katika kutekeleza huduma za mirathi, jumla ya majalada 389 yalifunguliwa, majalada 342 yenye mali ya thamani ya shilingi 2,219,262,573.00/= yalifungwa Unguja na Pemba, na mapitio ya majalada ya 2005 yamefanyika. Aidha, nyaraka 29 zikiwemo 23 za urithi na sita za mauzo zimetolewa. Vile vile, mizozo 12 inayohusu mirathi imeshughulikiwa na mengine 13 inaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2012/13, Kamisheni imesimamia vyema shughuli za Hijja na kuimarisha huduma za Mahujaji. Jumla ya Mahujaji 2,146 walitekeleza ibada hiyo. Mahujaji 1,255 kati ya hao walisafiri kupitia vikundi vya Zanzibar na vikao tisa vimefanyika ndani na nje ya nchi kuratibu shughuli za Hijja. Vile vile, Kamisheni imeendelea kusimamia kwa ufanisi shughuli za Sala na Mabaraza ya Idd kitaifa. Angalia Kiambatanisho Nam. 8b.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2012/13 Kamisheni imeanzisha uhusiano na Wizara ya Wakfu ya Oman,

Qatar, Taasisi ya Al-Rahma ya Falme za Kiarabu *UAE* na Shirika la *Danmission la Denmark*.

Mhe. Spika, katika kutayarisha nyenzo za kufanyia kazi, Kamisheni imo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Hiba na Wakfu, Wasia na Mirathi, Huduma, Ada na Malipo. Aidha, kazi ya kukamilisha Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana zinaendelea sambamba na ukamilishaji wa Muundo wa Kamisheni. Katika kuwajengea uwezo watendaji, Kamisheni imesomesha wafanyakazi wawili ngazi ya Shahada, wanne Stashahada na wawili mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Kamisheni imetoa mafunzo ya ndani kuwajenga wafanyakazi ili kutoa huduma bora zaidi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/13 Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 460,000,000.00/= za ruzuku zikiwemo shilingi 291,280,000.00/= za mishahara, shilingi 168,720,000.00/= za matumizi mengine na shilingi 179,000,000.00/= za makusanyo ya ndani. Hadi kufikia Machi 2013, fedha zilizoingizwa ni shilingi 184,789,875.00/= (63%) zilizotumika kulipia mishahara na shilingi 172,850,381.00/= (102%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 136,561,865.00/= (76%) zilikusanywa kutokana na mapato ya ndani na zilichangia uendeshaji wa ofisi. Angalia Kiambatanisho Nam. 1.

Mhe. Spika, katika mwaka ujao wa fedha Kamisheni imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za Zakka na Wakfu;
ii. Kuimarisha Uwezo wa Afisi kiutendaji; na
iii. Kuimarisha shughuli za Uratibu na Uendeshaji.

Mhe. Spika, ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya shilingi 510,000,000.00/= zikiwemo shilingi 303,745,000.00/= za mishahara, na shilingi 206,255,000.00/= za matumizi mengine.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za utendaji wa Wizara Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Afisi Kuu Pemba imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba imefanya ziara tano za kutembelea Idara na Taasisi za Wizara na kufanya mikutano mitatu ya robo mwaka. Aidha, Ofisi

imefanya mkutano mmoja wa wafanyakazi kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji. Vile vile, Ofisi Kuu Pemba imeratibu maandalizi ya ripoti na taarifa za utekelezaji na maandalizi ya bajeti ya Wizara ya 2013/14 na kuziwasilisha Wizarani kwa hatua zaidi.

Mhe. Spika, mbali na majukumu hayo Afisi Kuu Pemba imeshiriki vikao mbali mbali vilivyojadili ripoti na bajeti ili kupata miongozo ya pamoja. Aidha, Afisi imeratibu kazi zinazohusiana na marekebisho ya utumishi wa umma yanayohusisha kuhakiki na kupitia mafaili ya wafanyakazi, kutayarisha *norminal roll* na madaraja ya wafanyakazi *(Scheme of Service)* wa wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, miongoni mwa kazi za Afisi Kuu Pemba ni kuratibu shughuli za Jumuiya zisizo za Kiserikali (*NGOs*). Katika mwaka wa fedha unaomalizika, Afisi Kuu Pemba imezitembelea Jumuiya zilizoko Pemba kwa lengo la kutathmini utendaji na kuwepo kwake. Jumla ya Jumuiya 26 zimetembelewa kati ya 36 zilizopangwa.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo watendaji wake, Afisi imeandaa mafunzo ya wafanyakazi yanayohusu Sheria ya Utumishi wa Umma kwa watumishi wa wizara. Afisi pia imeendelea kulipa gharama za mafunzo kwa watumishi watatu wa Afisi Kuu, mmoja katika ngazi ya stashahada na wawili mafunzo ya muda mfupi katika fani ya uchunguzi wa hesabu za ndani na utunzaji wa kumbukumbu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Afisi Kuu Pemba ilikadiria kutumia Shilingi 165,331,000.00 kwa kazi za kawaida zikiwemo Shilingi 80,159,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 85,172,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kufikia Machi 2013 jumla ya shilingi 60,119,250.00 (75%) zimetumika kwa kulipia mishahara na shilingi 41,483,951.00 (49%) kwa matumizi mengineyo. *Angalia Kiambatanisho Nam. 1.*

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/14, Afisi Kuu Pemba inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

iv. Kuendelea kuratibu shughuli za Wizara Pemba;

v. Kuwaendeleza wafanyakazi kielimu; na

vi. Kulifanyia matengenezo jengo la wizara Pemba.

Mhe. Spika, ili Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika mwaka wa fedha 2013/14, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe

jumla ya shilingi 196,575,000.00 kwa matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi 105,704,000.00 za mishahara na Shilingi 90,871,000.00 za matumizi mengineyo.

Rasimu ya Katiba

Mhe. Spika, sote tunaelewa kuwa rasimu ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imeshatolewa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Napenda kutanabahisha kuwa kazi iliyopo mbele ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni kubwa. Kwanza ni sisi wenyewe kujua tunataka Muungano upi na Katiba ipi. Baada ya kujua hayo, itatulazimu tuwaelimishe wananchi wetu ili waijadili rasimu hii iliyopo na kutoa maoni yao kupitia Wawakilishi wao, Mabaraza ya Katiba na, hatimaye, Bunge la Katiba.

Mhe. Spika, ninachowaomba wananchi na kwa kweli kwa kupitia Wawakilishi wao, ni kutazama na kujadili rasimu hiyo na kuona kama kweli inakidhi haja ya kuleta maendeleo kwa Zanzibar; maisha mazuri kwa vizazi vya Wazanzibari; na haki za Wazanzibari; na kwamba Katiba itakayopatikana itaweza kuhimili misukosuko ya kisiasa na kibinadamu na kuweza kuishi kwa miaka mingi ijayo bila ya mtikisiko wa vishindo vyovyote. Tuhakikishe kuwa Katiba hiyo inafufua matarajio ya Wazanzibari kwa Zanzibar yetu ya leo na ya siku za usoni.

Mhe. Spika, ni lazima tuelewe kuwa Katiba tuitakayo Wazanzibari itabadilisha sana taifa letu, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Baadhi ya mabadiliko hayo yatakuwa ya karibuni na tuwe tayari kuyaunga mkono. Lakini baadhi ya mabadiliko yatachukua muda, ni lazima pia tuwe imara na wenye uzingativu kwa kujibidiisha kulingana na mabadiliko hayo.
Mhe. Spika, kwa upande wa serikali, napenda nichukue nafasi hii tena kwa kuwahakikishia Wazanzibari kuwa tutasimama na matakwa ya Wazanzibari na tutawatetea na kuwasimamia kwa yale yote mtakayokubaliana katika Mabaraza ya Katiba katika kuleta maslahi ya Zanzibar.

Shukrani

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuiwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Aidha, napenda kuwashukuru wale wote waliotoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara yangu.
Vile vile, natoa shukurani kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu, bila kuwasahau watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza kazi za Wizara na kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Mwisho, natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza hili, kwa michango yao yenye manufaa kwa Wizara na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba uniruhusu niwashukuru wadau mbali mbali wa maendeleo ambao wamefanya kazi kwa mashirikiano makubwa na Wizara yangu. Wadau hao ni *UNDP, UNICEF, UNFPA*, Shirika la Kimataifa la Mali za Ubunifu (*WIPO*), Shirika la Mali Bunifu la Afrika (ARIPO), Benki ya Dunia, Jumuiya ya Ulaya, *African Muslim Agency*, Benki ya Maendeleo ya Kiislam (*IDB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), *Save the Children*, Wizara za Wakfu za Oman na Qatar, Taasisi ya Al-Rahma ya Falme za Kiarabu (*UAE*) na Shirikia la *Danmission* la Denmark; Saud Arabia, Oman, na Egypt; Chama cha Wanasheria Zanzibar (*ZLS*) na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (*ZLSC*), na Chama cha Wanasheria Wanawake (*ZAFELA*); Vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano zikiwemo Mahkama, Tume ya Kurekebisha Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, na Jeshi la Polisi; Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji, Jumuiya na Taasisi mbali mbali za kidini na Masheha na Wanajamii wote wa Zanzibar kwa jumla. Hao wote tunathamini ushirikiano na misaada yao ya hali na mali, na kwa niaba ya wizara yangu na serikali kwa jumla hatuna zaidi cha kuwalipa isipokuwa kuwambia ahsante sana na Mungu awabariki.

Hitimisho

Mhe. Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza malengo yake vyema, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye tunaomba waidhinishe Shilingi 8,188,000,000.00 kwa matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha wa 2013/14 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 4,480,499,000.00 zitumike kulipia mishahara na Shilingi 3,707,501,000.00 kwa matumizi mengine.

Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi 2,154,313,000.00 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, 850,000,000.00 ni kutoka serikalini na Shilingi 1,304,313,000.00 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Vile vile, naliomba Baraza lako liidhinishe Ruzuku ya Shilingi 730,000,000.00. Naomba pia Baraza lako liikubalie Wizara yangu ichangie Shilingi 435,000,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *Angalia Viambatanisho Nam. 2&3.*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria naomba kuwasilisha muhtasari wa hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara ya Katiba na Sheria Mwaka 2013/14

Mhe. Spika, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya na tukaweza kukutana hapa kwa ajili ya kutekeleza wajibu wa kulijenga taifa letu. Aidha napenda kuchukua nafasi hii pia kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Abubakar Khamis Bakari pamoja na watendaji wa Wizara hii wote kwa mashirkiano yao ya dhati waliyoipatia Kamati yetu katika kutekeleza kazi zake za msingi kama ilivyoelekezwa katika kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kazi yetu ya kupitia bajeti ya wizara hii isingekamilika bila ya mashirikiano ya hali ya juu ya wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao walifanya kazi hii kwa kujitolea na kujifungia siku nzima bila ya malipo kabla ya siku iliyopangwa kukutana na wizara na kukipitia kifungu kwa kifungu kwa lengo la kuchambua kwa umakini bajeti hii.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii ndogo kuwatambua wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala huku nikithamini mchango wao mkubwa uliofanikisha Kamati hii kuwasilisha muhtasari huu wa hotuba, naomba tena niwataje kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ussi Jecha Simai Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salim Ali Mjumbe
5. Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mjumbe
6. Mhe. Mansoor Yussuf Himid Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis Mjumbe
8. Ndg. Aziza Wazir Kheir Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji Katibu

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo sehemu ya kielelezo cha utawala wa nchi, bila ya uwepo wake nchi ingekuwa na utaratibu mbovu wa taratibu na sheria. Wizara hii ndiyo inayoratibu uendeshaji wa moja ya mihimili mitatu ya dola ambao ni Mahakama, kutokana na jambo hilo ndiyo maana nikatangulia kusema kuwa wizara hii ni sehemu ya kielelezo cha utawala wa nchi kutokana na umuhimu wake huu.

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ni miongoni mwa Wizara za serikali ambazo zinatoa huduma moja kwa moja kwa wananchi na kukusanya mapato mbali mbali yanayotokana na huduma hizo kwa wananchi. Mwaka uliopita

wa bajeti, Wizara ya Katiba na Sheria ilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. Milioni 447 katika vyanzo vyake vya mapato.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2013, jumla ya Tsh. 288,708,060, zilikusanywa na kuingizwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali ambazo ni sawa na asilimia 65% ya makadirio. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja alieleze Baraza lako ni kwa nini Wizara yake haikufikia malengo ya ukusanyaji ingawa imevuka malengo hayo.

Mhe. Spika, kamati yangu inapendekeza njia mbadala za kukusanya mapato ya huduma zinazotolewa na Wizara kupitia taasisi zake mbali mbali, yalipwe kwa utaratibu mwengine kama vile kupitia benki badala ya malipo kufanywa mikononi mwa watu.

Mhe. Spika, naeleza hivyo kutokana na ukweli kwamba Baraza lako tukufu ambalo lilielezwa kuwa mapato yaliyokadiriwa kupatikana katika bajeti ya mwaka wa fedha unaomalizika kutoka kodi za Mawizarani ni Tsh. Bilioni 20, lakini kwa bahati mbaya kabla ya robo ya mwisho ya bajeti hiyo kumalizika ni Tsh. 8.8 bilioni tu ndizo zilizokusanywa. Kamati yangu haitaki kuamini kuwa makadirio hayo hayawezi kufikiwa lengo. Kamati inaamini kuwa makadirio hayo ili yaweze kufikiwa ni vyema utaratibu wa makusanyo ukabadilika na kuwa wa kibenki.

Mhe. Spika, kwenye miradi ya maendeleo Wizara ya Katiba na Sheria bado inasuasua na inakwenda taratibu mno, jambo ambalo limesababishwa na kusita kwa baadhi ya miradi yake kama vile mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Makampuni na Kuimarisha Afisi chini ya mpango wa kuimarisha mazingira ya Biashara, mradi huu ulitarajiwa kufadhiliwa na Benki ya Dunia kwa bahati mbaya hadi hivi sasa fedha hazikupatikana.

Mhe. Spika, miradi mengine ambayo ilianza vizuri lakini sasa hivi inakwenda kwa kusuasua ni pamoja na ujenzi wa jengo la Afisi ya Mwanasheria Mkuu, inasikitisha kuona hatua iliyofikiwa ya ujenzi ule imekwama njiani, kamati yangu inaiomba serikali kurekebisha mipango na kuhakikisha kuwa inatafuta fedha za kumalizia ujenzi wa jengo lile.

Mahakama

Mhe. Spika, kamati imebahatika kufanya ziara katika baadhi ya majengo ya mahakama za Wilaya na kujionea hali mbaya ya baadhi ya majengo ya Mahakama hizo ambayo ndiyo taswira ya eneo la kutolea uamuzi wa mashauri mbali mbali yanayofikishwa hapo. Mfano wa majengo ya mahakama ambayo hali yake haiwezi kusubiri bajeti yetu itoshe ndiyo

yafanyiwe kazi ni jengo la mahakama ya Mwanakwerekwe, Mfenesini na Makunduchi.

Mhe. Spika, Mahakama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe hali yake ni mbaya sana, chumba wanachotumia waendesha mashitika na polisi kwa ajili ya kutayarisha ushahidi na mashahidi hakipo katika mazingira mazuri hata kidogo ya kuendesha shughuli hizo. Ni chumba kidogo cha futi 19, watu zaidi ya 20 wanakitumia, vielelezo vya ushahidi kama chupa za mikojo, kemikali, madumu ya ulevi wa kienyeji, mabati, nondo nakadhalika, vyote vimejumuishwa na binadamu wanaofanya kazi hapo.

Aidha chumba hicho ni mazalia mazuri ya wadudu waharibifu kama vile panya ambapo wadudu hao huzaliana kutokana vitu nilivyovitaja hapo juu vikiwekwa kama ushahidi lakini kutokana na ufinyu wa sehemu hiyo na vitu hivyo hukaa muda mrefu husababisha ushahidi huo kugeuka na kuwa taka taka ambazo zina athari kwa afya ya binadamu. Vile vile katika Mahakama hiyo Kamati ilipata bahati ya kuoneshwa chumba cha kuwekea mahabusu ambacho ni kidogo sana na kimekuwa na msongamano mkubwa baadhi ya wakati.

Mhe. Spika, hali siyo hiyo tu, kamati yangu ilitembelea Mahakama ya Wilaya ya Makunduchi, kwa kweli hali ni mbaya sana na inasikitisha kuona kuwa sehemu ambayo mwananchi anategemea kupata haki zake za msingi kisheria ipo kama jinsi tulivyolikuta ambapo hivi sasa jinsi lilivyo nathubutu kusema ni kama gofu la zamani ambalo linavuja, halina dari, sakafu yake imechimbika, hali ya hewa ya vumbi na ukungu ndani ya jengo. Kutokana na hali hiyo napata nguvu ya kusema kuwa jengo hilo halifai kutumika kutokana na mazingira halisi ya jengo hilo huenda kinyume na mazingira ambayo binadamu yeyote yule angependa kukaa na kufanya kazi zake kwa utulivu.

Mhe. Spika, kutokana na ufinyu wa muda, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, haikuweza kutembelea majengo mengine ya Mahakama za Wilaya, lakini imepata taarifa za uhakika kuwa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mfenesini halina hata chumba cha waendesha mashtaka na badala yake waendesha mashitaka wanatayarisha mashahidi wakiwa kwenye gari.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba na Sheria imeamua kuyaweka wazi mambo iliyoyaona katika kipindi kifupi tu tokea kuundwa kwa kutaka Baraza lako lielewe kuwa tunapotoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri kwa kufanya kazi vizuri, tusisahau kuwapa pole watendaji wanaoumia kwa kufanya kazi kwenye mazingira magumu huku tukiwategemea wafanye hivyo kwa ufanisi. Licha ya yote hayo, kamati yangu imesikitishwa sana na kasma ndogo ya

fedha za maendeleo iliyopewa Mahakama katika bajeti ya mwaka huu 2013/2014 kwa ajili ya matengenezo ya majengo yake.

Mhe. Spika, kamati yangu imesikitishwa sana wakati ilipokuwa ikipitia bajeti kwa kugundua utofauti wa fedha katika fungu la 36 la fedha za maendeleo ambapo kulijitokeza kasma mbili tofauti, moja ikiwa ni shilingi milioni 300 na ya pili ni milioni 150 na baada ya kutaka maelezo Kamati ilielezwa kuwa kasma ya shilingi milioni 150 ndio sahihi.

Mhe. Spika, kamati inaona kuna haja kwa Wizara ya Fedha kuwa makini katika uwekaji wa fedha katika bajeti ili kuepuka utata kwa Wajumbe hali ambayo inaweza kusababisha mzozo ndani ya Baraza hasa ukizingatia bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ni ndogo katika maeneo ya Mahakama ambapo Kamati yangu haikuridhishwa na fedha zilizotengwa hasa tukizingatia kuwa kuna changamoto nyingi tulizozieleza.

Mwanasheria Mkuu

Mhe. Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeongezewa majukumu kwa kupewa jukumu la kuwasimamia wanasheria wote wa Serikali, kuwajengea uwezo na kuratibu utendaji kazi wao uwe wa ufanisi. Kamati yangu ina mashaka na utekelezaji wa azma hiyo kwa kuwa bajeti ya mwaka huu ya Tsh. 919 milioni ni ndogo mno ambayo haikidhi utekelezaji wa majukumu hayo ya ziada.

Mhe. Spika, kamati inakumbusha tena wasi wasi wake wa kusita kwa ujenzi wa jengo la Afisi za Mwanasheria Mkuu ujenzi ambao ulianza vizuri lakini hivi sasa umesimama. Kamati inaiomba serikali kukata pua na kuunga wajihi, kwa kutafuta fedha na kupunguza matumizi mengine yasiyokuwa ya lazima ili waweze kusaidia jengo lile limalizike ili liweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

Tume ya Kurekebisha Sheria

Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria ni miongoni mwa Taasisi nyeti zilizopo hapa nchini kutokana na ukweli kwamba chombo hiki kina jukumu la kuhakikisha kuwa kinatafsiri sheria hizo katika lugha nyepesi na kuzifanya zieleweke kwa wananchi. Kazi hii sio nyepesi hata kidogo, inahitaji utulivu na wataalamu wa kada tofauti zinazohusu sheria husika. Sambamba na hilo elimu kubwa kwa wananchi inatakiwa itolewe ili kuwawezesha wananchi hao kushirikina na Tume katika kuzifanyia marekebisho sheria zetu wakati wowote wananchi watakapohisi utekelezaji wa sheria hizo ni mgumu.

Mhe. Spika, kwa kuona umuhimu huo, kamati inaishauri serikali kutatua changamoto ya ukosefu wa Ofisi ya Tume kwa kuwa na Afisi za kudumu

badala ya kuhama hama na kukodi majengo kwa gharama kubwa. Aidha Kamati imeona jinsi Tume hii inavyotumia fedha nyingi za kulipia kodi ya Ofisi ambapo fedha hizo hizo kama zingetumika kidogo kidogo kujenga jengo la Ofisi za Tume lingekuwa katika hatua nzuri kwa sasa.

Afisi ya Wakala wa Usajili wa Makampuni
Mhe. Spika, Afisi ya Wakala wa Usajili wa Makampuni inahitaji kuimarishwa kwa kuhakikisha inakuwa na watendaji wenye uwezo na utaalamu mkubwa. Kamati imepata wasi wasi wa kukimbia kwa wataalamu wa Afisi ya wakala wa Usajili wa makampuni hasa katika fani za mawasiliano na kompyuta. Mhe. Spika, uondokaji huu unaelezwa kusababishwa na maslahi madogo wanayolipwa wataalamu wa fani hizo adimu.

Mhe. Spika, kamati inapendekeza kuwa katika kuifanya Afisi ya Wakala wa Usajili wa Makampuni kutatua baadhi ya changamoto zake basi iwezeshwe kubakisha asilimia maalum ya makusanyo ya fedha za huduma wanazozitoa. Hatua hii inaweza kupunguza utegemezi wa Afisi na kujiendesha yenyewe bila ya mwega wa Serikali.

Afisi ya Msajili wa Hakimiliki
Mhe. Spika, Afisi ya Msajili wa Haki Miliki tumeibebesha dhima ya kusimamia haki za wasanii, kutokana na jukumu hilo kubwa tuliyoibebesha Afisi hii ni lazima tukumbuke kuwa ni lazima watendaji wa Afisi hii wapatiwe vitendea kazi vitakavyowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Miongoni mwa vitendea kazi muhimu ni pamoja na usafiri ambao utaisaidia ofisi na kurahisisha kazi za kila kila siku. Kutokana na kilio cha muda mrefu kilichokuwepo katika taasisi hii, tunapenda kutoa pongeza kwa serikali katika bajeti ya mwaka huu kulizingatia suala hilo kwa kuweka kasma kwa ajili ya ununuzi wa gari.

Aidha kamati ilipotembelea katika taasisi hii ilipewa taarifa kuwa baadhi ya wataalamu wake wanahamia katika taasisi nyengine kutokana na mishahara midogo wanayolipwa, kutona na hali hiyo, Kamati inaiomba serikali ilifikirie suala hilo ili wataalamu hao wanaosomeshwa na serikali waweze kuzitumikia taasisi zinazowagharamia katika masomo yao.

Mhe. Spika, mwaka huu wa fedha 2013/14, Afsi ya Msajili wa Hakimiliki imekadiriwa jumla ya Tsh.140 milioni zikiwa ni ruzuku ya mishahara na shughuli nyengine za uendeshaji. Hata hivyo Kamati ina mashaka makubwa na kiasi hicho cha fedha kilichotengwa kutokana na ukweli kuwa fedha hizo ni kidogo na tunahisi kuwa fedha hizo huenda zisikidhi mahitaji katika uendeshaji wa shughuli za Afisi hiyo kutokana na majukumu mazito

yaliyokuwepo. Aidha, wasi wasi mkubwa wa Kamati yetu unakuja kutokana na Afisi hii kukosa jengo la ofisi na wataalamu.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali kudhibiti upotevu na wizi wa kazi za wasanii kwa kuiwezesha Afisi hii kufanya marekebisho ya sheria yake ambayo ingeweka sharti la kutorejesha leseni kwa vituo vya utangazaji ambavyo havilipi mirahaba.

Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo

Mhe. Spika, kamati wakati inachunguza fungu 36 la Wizara ya Katiba na Sheria kwenye kifungu 0901 cha Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo haikuridhika na maelezo iliyopewa kuhusiana na kifungu hicho. Kutokana na kutoridhika huko kamati imeagiza marekebisho yafanyike kwa baadhi ya vifungu ambavyo kasma zake zimewekwa kwenye vifungu visivyoombewa matumizi. Marekebisho hayo yamefanyika kama kamati ilivyoagiza kama ifuatavyo kijifungu 220408 gharama za umeme zilikuwa sifuri, hivi sasa kijifungu hicho kimewekewa fedha zilizokuwa katika kijifungu 220302 cha safari za nje ambazo ni Tsh. 4,535,000. Kijifungu 311203 cha fedha za Ununuzi wa vyombo vya Usafiri, kimepunguzwa Tsh. 1.5 milioni ambazo zimeongezwa kwenye kifungu 220301 cha safari za ndani na hivi sasa kimewekewa Tsh. 7,500,000 kutoka 600,000 za awali.

Mhe. Spika, kamati inaiomba serikali kuisadia Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kwa kuitafutia wafadhili kusaidia utoaji wa taaluma kwa wananchi hasa katika kukabiliana na changamoto ya kughushi vyeti vya kuzaliwa. Aidha, kamati inaiagiza Idara hii kukutana na Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari kueleweshana kuhusu nani hasa mwenye dhamana ya kuthibitisha uhalali wa cheti cha kuzaliwa.

Mhe. Spika, kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Afisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kutokana na ukarabati wa vituo vya Wilaya ya Kaskazini "A" kwa kituo cha Gamba, Wilaya ya Kaskazini "B" kwa kituo cha Mahonda, kituo cha Wilaya ya Kati kilichopo Dunga na kituo cha Wilaya ya Kusini kilichopo Makunduchi, Kamati iliridhika na ukarabati uliofanyika na inaiomba Ofisi hii iendelee na juhudi za kuvikarabati vituo vyake vyote vilivyopo nchini.

Aidha kamati inaiomba serikali ilizingatie suala la wafanyakazi wa Ofisi za Vizazi na Vifo hasa wale walioko katika vituo mbali mbali ambao inaonekana wanafanya kazi katika Wizara mbili, hasa linapokuja suala la posho la wafanyakazi hao ambapo tatizo linajitokeza la kuijua ni Wizara ipi inayohusika na malipo ya posho za wafanyakazi hao. Hivyo Kamati inaomba

suala hilo lizingatiwe na Wizara zote kwa kukaa pamoja na kuamua nani atawajibika kwa wafanyakazi hao.

Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana

Mhe. Spika, wakati wa kuwasilishwa bajeti ya mwaka unaomalizika wa fedha, 2012/13, Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana ilikuwa kati kati ya mijadala mizito ya Wajumbe wa Baraza hili, hasa katika suala la nyumba za amana za Michenzani zilizo chini ya amana ya Kamisheni ambazo zilizokuwa mikononi mwa Idara ya Nyumba. Kwa mujibu wa maelezo tuliyopatiwa ni kuwa Kamisheni inashindwa kuzifuatilia suala hili kutokana na kukosa "*Appointment"* na wahusika wa Idara ya Nyumba. Aidha kwa majibu wa maelezo hayo inaonekana kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Nyumba anawakwepa watu wa wakfu kwa ajili ya kukaa na kulizungumzia suala hili na hatimaye makabidhiano ya nyumba hizo yaweze kufanyika. Kutokana na hali hiyo Kamati inaiomba Wizara kuwasiliana na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi suala hilo na hatimaye nyumba hizo zikabidhiwe kwa wahusika ambao ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Spika, suala hilo bado halijamalizika na kamati haitapenda lijitokeze tena katika mijadala ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2013/14. Kamati imeshatoa agizo kwa Kamisheni ya Wakf kukutana haraka na Idara ya Nyumba kulimaliza suala hili.

Mhe. Spika, kamati inaguswa na suala la malipo ya kodi za nyumba za Wakf ambapo kodi hizo zinalipwa kwa kiwango kidogo na wapangaji. Wapangaji wengi wa nyumba hizo wanapangishwa kwa fedha kidogo chini ya Tsh. 50,000/= huku wao wakizipangisha kwa bei ya juu ambayo ni zaidi ya Tsh. 200,000/= Mhe. Spika, hii ni dhuluma hasa ukizingatia mazingira ya nyumba zenyewe.

Mhe. Spika, kamati inashauri Kamisheni kuandaa mikataba mipya itakayokuwa na vipengele visivyoruhusu mikataba mengine kwa wanaopangishwa *(sub letting).*

Afisi ya Mufti

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba na Sheria inatambua mchango wa Afisi ya Mufti katika kuimarisha mshikamano na ustawi wa maadili mema ya jamii yetu. Kama tunavyojua kuwa jamii yetu hivi sasa imekumbwa na janga kubwa la mporomoko wa maadili na vitendo viovu hasa vya udhalilishaji wa watoto na wanawake kijinsia katika maeneo ya utoaji wa taaluma kama vile skuli, madrassa, majumbani pamoja na meneo mengine.

Kutokana na hali hiyo, kamati inaiomba serikali kushirikiana na Afisi ya Mufti kwa kuipatia fedha za kufanya kampeni na kutoa elimu ya mwamko wa jamii kupambana na vitendo hivyo. Aidha, kamati inapendekeza Afisi ya Mufti kuandaa utaratibu mpya wa kuhakiki madrassa na kutayarisha leseni maalumu kwa ajili ya walimu wa madrassa hizo, ili kubaini baadhi ya watu waovu wanaojipenyeza katika madrassa kwa nia mbaya na kudhalilisha watoto kijinsia.

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka

Mhe. Spika, kamati inachukua fursa hii kuipongeza Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka katika kuimarisha mpango wake wa kueneza uendeshaji wa mashitaka kiraia katika Wilaya zote. Mpango huo utawezesha Mahakama nyengine za Wilaya ambazo hazijafikiwa na waendesha mashitaka wa serikali kuanza kuutumia utaratibu huo.

Mhe. Spika, kamati inasikitika sana kuona juhudi hizo zinarudishwa nyuma kutokana na hizo fedha kidogo zinazotengwa katika bajeti kutopatikana kwa wakati. Hivyo Kamati inaiomba serikali kuhakikisha kuwa fedha hizo kidogo zinazokuwa zimetengwa zinapatikana kwa wakati ili yale malengo ya ndani ya taasisi husika yaweze kutekelezeka. Aidha ukosefu huo wa fedha au ucheleweshaji huo huleta athari kubwa ya kiutendaji ktika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mhe. Spika, mpango wa uendeshaji wa mashitaka kiraia unapokwama maana yake tunaendelea kuruhusu uendeshaji wa kesi katika Wilaya kwa kutumia Polisi ambao ni hao hao wanafanya upelelezi wa kesi na wakati mwengine kukosa ufanisi wa uendeshaji wa kesi zenyewe na hatimaye watuhumiwa wa uhalifu wanaachiwa pengine kwa kukosa ufanisi wa kuendesha kesi tu na wala sio ushahidi.

Mhe. Spika, mwaka wa fedha unaomalizika 2013/14, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ilikadiriwa kupata kiasi cha Tsh.. 250 milioni, fedha za maendeleo ambazo hadi mwezi Machi, 2013 ni Tsh. 100 milioni tu ndizo walizopatiwa kati ya fedha hizo. Kamati imeridhika jinsi fedha hizo kidogo zilivyotumika katika ujenzi ya nyumba ya Mwendesha Mashitika Mkoa wa Kusini Unguja, Kuimarishwa kwa Afisi ya Pemba na Kununuliwa Kiwanja cha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, Kamati yangu hairidhishwi na fedha za maendeleo ilizopatiwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mshitiaka katika mwaka huu wa fedha 2013/14 ni Tsh. 100 milioni ambazo kamati imeshindwa kujua zitatumika vipi mwaka huu wakati Afisi imebakisha njiani malengo ya mwaka jana ambayo yanahitaji zaidi yaTsh.150 kuyakamilisha.

Mhe. Spika, hali hiyo inamaanisha kuwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mshtaka kwa mwaka huu wa fedha haitaweza kukamilisha mipango yake, hii ni kutokana na kutokamilika kwa mipango ya mwaka wa fedha uliopita ambayo pia inahitaji kukamilishwa kabla ya utekelezaji wa mipango ya mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, hali hii inasikitisha na inaipa changamoto kubwa Kamati ya kujiuliza endapo ni kweli tunapanga mipango yetu kwa uhalisia kwa kuweka vizuri vipaumbele vyetu? Kutokana na hali hii Kamati inaisisitiza Serikali kuitazama jicho la pekee Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ambayo imebebeshwa majukumu mazito na yenye hatari, huku maslahi ya wafanyakazi wake yakiwa madogo. Kwa mwaka huu wa fedha kifungu cha posho la mazingira magumu cha Afisi hii kina kasma sifuri, licha ya mazingira ya hatari wanayofanyakazi wafanyakazi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mhe. Spika, mazingira ya kazi ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mshitaka yana changamoto nyingi ambazo zinahitaji uwezo wa kifedha ambao utasaidia kuzipunguza changamoto hizo. Mhe. Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Afisi hii lakini bado kuna tatizo la uelewa wa wananchi katika kutoa mashirikiano na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, hasa katika suala la kutoa ushahidi. Kesi nyingi zinashindwa kuendelea kutokana na wananchi kushindwa kutoa mashirikiano na Afisi na hatimaye kesi kufutwa, tatizo hili linahitaji kampeni na elimu kubwa kwa umma ambayo kamati inashauri Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ipatiwe fedha za kufanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, hakuna hatia bila ya Ushahidi, hiyo ni kauli mbiu ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ambayo kamati inakubaliana nayo. Ukosefu wa kukusanya ushahidi kwa njia za kisasa unasababisha kazi ya Waendesha Mashitaka kuwa ngumu. Kamati inakumbusha ahadi ya Serikali ya kupatikana kwa kifaa cha *DNA* ambacho kitasaidia sana ushahidi wa kitaalamu badala ya kutegemea ushahidi wa kiramli wa kuona peke yake hasa katika kesi zinazohusu udhalilishaji wa kijinsia.

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii na kunivumilia muda wote kutoa hotuba hii kwa niaba ya kamati. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Baraza kwa utulivu na ukimya wao wakati nikiwasilisha maoni haya ya kamati. Ni imani yangu wataipokea, kuichangia na hatimae kuipitisha bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria na kumsaidia Waziri kurejeshewa mafungu yake yaliyopunguzwa katika baadhi ya taasisi zake.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Bismillahi Rahmani Rahim Mhe. Spika, Wizara hii leo kubwa sana hasa ikiambatana na kina Mufti na kuna Katibu wetu wa Wakf na Mali na Amana lazima tuanze kwa jina kubwa ili Mwenyezi Mungu atuongoze vizuri katika utendaji wetu huu na panapo haki tupeleke haki ipasavyo kwa mujibu wa sheria na Katiba na Kanuni zetu.

Mhe. Spika, mimi nichangie katika sehemu ya Idara ya Mipango na Sera, ningemuomba Mhe. Waziri kifungu cha 23 amenambia kuna semina ambazo zilifanyika hapa angenifafanulia semina ngapi na katika semina hiyo anambie kuwa katika uelewa hao waliopewa semina hizo wamefika *percentage* ngapi katika kufahamu lile ambalo lililokusudiwa humu katika utafiti huo ambao walioutoa wao kwenye mafunzo hayo.

Lakini nikenda katika ukurasa mwengine wa Mahkama Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hapa wote wanasheria hao lakini hasa ningesema kuwa Waziri atanisaidia kwa uelewa wake wa sheria, kwa sababu sheria ina mapana mengi sana na ina tafsiri nyingi lugha moja unaweza ukatafsiri mara tatu mpaka nne.

Lakini vile vile nimuelekee Mwanasheria ninamuomba sana na yeye katika mchango wangu huu hapa kwenye Mahakama na yeye ambaye ni mtaalamu wa kufafanua zaidi hii Katiba aweze kunisaidia ili niweze kufanikisha. Mhe. Spika, mimi hupata tabu sana katika kichwa changu hiki na hasa katika neno Katiba. Mhe. Spika, mimi ninakuwa naheshimu sana Katiba tena ninaiogopa katika kuongeza neno au kutengua neno. Lakini Mhe. Spika, Mahakama zetu hizi katika Katiba yetu hii inanambia ina Tume yake, lakini nashangaa sana kwa kuwa Mahkama ina Tume, halafu leo wanakuwa fursa zao hasa za marupurupu za s*cheme of service* zinakuwa hazitambulikani zinakwenda katika Tume nyengine ambazo na hapa ningemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri nyote wanasheria, hebu nambieni hasa koseo liko wapi Katiba inaeleza hivyo? Lakini huku huku tulipitisha tena Kamisheni ya Utumishi katika wizara nyengine, niambie mamlaka yao hapa yakoje. Kwa sababu Mhe. Spika, ili nende sambamba na wao ningeomba sana waje kunisaidia kuwa hii ya Katiba tuifute au hiyo nyengine tuifute au anambie Mhe. Waziri ataleta marekebisho ili tuende sambamba, ningeomba hivyo aweze kunisaidia.

Mhe. Spika, tuna Majaji wetu Wakuu, wengine sijui mpaka leo Mhe. Waziri sasa hivi nchi za wenzetu niseme kuna mihimili mengine hasa huko nje akiambiwa tu mtu huyu ni Jaji au Hakimu au ni Jaji Mkuu basi tayari yule mtu anatetemeka *automatical*, kwa sababu ni mtu mkubwa sana kwa wenzetu.

Lakini tuna Majaji sijui kama mpaka leo Mhe. Waziri utanieleza kama hapa tumewateua hivi karibuni wana ulinzi wa kutosha, haki yao Mhe. Spika, na sidhani kama mpaka leo ulinzi huo upo. Ningemuomba Mhe. Waziri hili aje kunambia kama tayari hawa Majaji wetu ni tayari na wao wamo kwenye muhimili na hawa. Sasa na wao ni watu wa kutumia *VIP* hawa lakini wanakosa ulinzi na pale tunawapa kesi kubwa kubwa, sasa sijui Mhe. Waziri atawalinda vipi hawa watu ambao tuliowachagua kwa mujibu wa Katiba yetu.

Mhe. Spika, nakumbuka kumbukumbu za mwaka jana tulipitisha *ceiling* ya shilingi milioni mia tatu kwa malengo mazuri tu, lakini Wizara ya Fedha ninasikitika sana huwa wanapenda kupunguza kiasi ambacho vile wanavyoona wao na kuona fedha zile wanazowatilia hawa Mahakama hii kwa shughuli zao wanaona kama itakuwa ni nafuu kwa kazi zao lakini si kweli, Mhe. Spika, tunawaonea kuwapa milioni mia moja na hamsini, hiyo ni sawa sawa na kutokuwapa fedha. Kwa kweli hili suala linatia unyonge mkubwa sana, angekuwepo Mhe. Waziri wa Fedha kwa nini tunawabena sana hawa Mahakama, kwa sababu ni chombo kikubwa nacho wamo ndani ya Katiba muhimili ambao tunautegemea.

Mhe. Spika, kusema kweli hili suala linasikitisha kwa sababu utakuta Mahakama yetu Kuu mpaka leo sijui atanieleza Mhe. Waziri kama bado anazo pesa za kuendeleza kulijenga lile jengo kulimalizia au kulikarabati na isitoshe Mahakama zetu nyengine ni chache tu zilizokuwa tayari zinakwenda na wakati. Ukenda Mfenesini haitambulikani, mbele na nyuma ukenda na sehemu nyengine. Mhe.Spika, tufumbe macho Mhe. Waziri angekuwepo wa Fedha awachie awape zile fedha kwa mujibu wa utaratibu.

Lakini vile vile tuangalie na hizi heshima za *VIP* za wakubwa wetu. Mimi mtazamo tu kwa kuwa Mhe. Spika, niseme na Mhe. Jaji Mkuu kwa mujibu wa Katiba na wao ni wakubwa katika viongozi wakubwa katika nchi hii. Lakini sina uhakika niseme hivyo Mhe. Waziri kuna mambo mengine Jaji Mkuu anayakosa hasa masuala ya *VIP*, na sijui ile sheria inasema vipi pengine Mhe. Spika, kidogo imenipita, *VIP* tunaambiwa kuna kitu kuna *services charges* pale unatakiwa ulipe lakini ninajua kwamba Mheshimiwa wangu Spika, atakuwa halipi sasa na kwa nini huyu Jaji Mkuu alipe na hiyo hebu tuangalie nayo kama ipo hiyo Mhe. Waziri unieleze kama Jaji Mkuu na yeye kwa mujibu wa sheria hana haki ya kulipa kama anavyokuwa Mhe. Spika wetu. Kama ni hivyo kama analipa Mhe. Spika *fine*, lazima na yeye itabidi alipe, sasa hebu tuangalie mazingira hayo halisi ambayo tunayokwenda nayo.

Lakini Mhe. Spika, twende katika masuala ya mishahara. Hili suala nilipigia kelele sana kuna mambo tukiwasaidia watu wenye dhamana kubwa tukawawekea katika mishahara yao isilinganishwe na sehemu ya Idara

nyengine ambayo iliyokuwa si muhimili au mengine yanakuwa ni muhimili, lakini tuangalie na zile *level* zenyewe zilivyo. Mhe. Spika, kusema la ukweli utakuta wale Majaji wetu hawa wanapata mishahara sawa sawa na Makatibu Wakuu. Mhe. Spika, kwa kweli niseme kuwa unajua mtu ukimuingilia katika suala lake ataona mbona huyu anataka kuniweka *level* moja na Jaji Mkuu au na Majaji, lakini ndio sheria ya Katiba ilivyoeleza humu. Mhe. Spika, imeeleza kwa ufasaha kabisa kuwa lazima kutakuwa na Majaji wetu kutakuwa na Jaji Mkuu kwa mujibu wa Katiba yetu. Mimi ningeomba na hili suala la mishahara hasa inayohusiana na *scheme of service* zao. Hatuoni Mheshimiwa kumuweka na Katibu Mkuu hawa watu hatuoni kama ni kupingana na Katiba yetu na kuwadharau hawa majaji wetu wakuu kwa mujibu wa sheria na Katiba? Ningeomba hilo hebu niweke sawa na wao tuwa-*favour* na wao tuwape haki yao kwa mujibu wa Katiba kwa sababu tunachokizungumzia ni Katiba. Mimi nazungumzia leo ni Katiba tu Mhe. Spika, na ndio maana nikasema kuwa anisaidie sana Mwanasheria Mkuu kwa suala hili ili tuekane sawa kutokana na ile Tume ambayo iliyokuwa imo ndani ya mamlaka ya Mahkama yenyewe ya kuweza kupanga mambo yao. Halafu nimekuta kifungu kimoja naomba nikinukuu hapa kidogo kifungu (b) masharti ya kazi, tizama sasa hapo kidogo nitasaidiwa nimekirukia hiki kwa mantiki yangu masharti ya kazi na marupurupu ya kiinua mgongo cha Jaji kwa mkataba ambao kwa kipindi maalum, huyo mtu wa mkataba yataamuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama.

Sasa Mhe. Spika, naomba hapa ndio maana ukaona nieleze hii ieleweke vizuri kuwatizama halafu utakuta hii Tume itashauriana na Mhe. Rais katika masuala ya kuteua Jaji Mkuu na masuala mengine. Kwa hivyo Mhe. Spika, bado tuuwekee heshima muhimili huu. Tuwape haki yao ambayo inayostahiki ili waweze kupewa na nilimsikia Mhe. Waziri siku moja alisema kuwa mishahara yao atawahakikishia na kuwasimamia wanapata basi isipokuwa moja tu ninamshukuru alisema ukweli *area* atakuwa hana uwezo wa kulipa. Kama nimekosea Mhe. Spika, Waziri atakuja kunisahihisha, hilo alilisema na akasema pengine aliona kuwa halipwi yeye zile akaweza akawalipa wao ndio mantiki yake. Sasa kashindwa hiyo kuji-*commit* lakini kwenye mishahara alisema atahakikisha watakwenda kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na hiyo Kamisheni ya Utumishi jinsi gani ambavyo *scheme of service* zitavyotolewa. Lakini mpaka leo hatujaona, sijasikia naomba nielimishwe kama haya mambo yameshakaa sawa, mishahara yao iko juu na niweze kuipongeza wizara hii.

Mhe. Spika, kwa kuendelea haraka haraka niseme kuwa Ofisi ya Mwanasheria lakini hapa hebu angalia fungu la Mwanasheria kama nimekosea linakuwa ni kubwa kuliko la Mahkama yenyewe. Sasa nini kilichojitokeza hapa ikawa hivyo utajaribu kunielekeza vizuri ili niweze

kufahamu, fungu kubwa liwe kwa Mwanasheria kwa kuwa kuna kazi zaidi kuliko Mahkama, naomba hilo nifahamishwe. Lakini Mwanasheria sasa kidogo ni mtaalam wangu mzuri sana hasa katika masuala ya Katiba, naomba sana uje kunisaidia ili nisije nikapotea *steps,* kwa mara nyengine nimeangalia sana humu hawa Manaibu Mawaziri jinsi ya shughuli zao, lakini naona bado sijapata ufafanuzi. Mwanasheria hebu nambie zaidi katika Kanuni hii yetu ya Baraza wewe utakuwa muhusika zaidi au uko katika *control* ya kuweza kufuatilia kutengeneza hii kidogo. Ningeomba na hili Mwanasheria wangu uje kunisaidia. Sasa nataka uje kunipa jibu kwa Naibu Waziri atakuwa na uwezo wa kunijibu mimi hoja au atakuwa na uwezo wa kuchangia kwa mujibu wa Katiba hii, naomba unieleweshe vizuri ili Katiba iende vizuri, naomba sana Mwanasheria hilo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, jitahidi sana katika hizi kesi ambazo zinawajibika kwa mujibu wa sheria ya serikali, ningeomba sana usiende *speed* kuzitengeneza hizi zina-*delay time*, hasa kuna mambo mengine ambayo yanatakiwa yatolewe hukumu haraka sana ili yasiathiri katika masuala mengine. Lakini niingie ukurasa wa 22 kwenye Tume ya Marekebisho ya Sheria hapa kidogo niipongeze sana na aendelee na jitihada zake za haraka haraka hasa kila panapoona sheria sasa hivi inataka kubadilika ili waweze kukaa pamoja waweze kutubadilishia ili kutuletea na tuweze kuipitisha hapa kwa mujibu wa taratibu tulivyojiwekea sisi wenyewe.

Niingie katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Spika, hapa niwapongeze sana kwa jitihada zao nzuri lakini vile vile niwaambie katika kamati imesema sasa hivi kuna tatizo hilo, kweli nakubaliana ili mtu atiwe hatiani lazima kuwe na sababu ambayo wanaoiona wao ili aweze kutiwa hatiani. Naomba sana Mhe. Spika, hili wasichukue muda mkubwa ili kesi zikaanza kurundikana au watu wakapata kujijua uamuzi wao. Napenda sana kwa uamuzi wao ambao wa haraka haraka na lile wanaloliona halistahiki kumtia hatiani wanakuwa *sharp* sana kulirembea huko na kulitolea uamuzi. Naomba sana wajitahidi sana ili jitihada zifike kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Spika, kwa kuendelea ukingoni namalizia kwa kuwa Wizara hii kubwa sana leo nimeianzia kwa jina la Mwenyezi Mungu. Hivyo niseme kwenye Mrajis wa Vifo na Vizazi Mhe. Spika, humu wametajwa mpaka Masheha wahusika katika kifungu hiki Mhe. Spika, ningeomba katika kuwaelimisha zaidi hawa Masheha wafahamu utaratibu ambao unaohusika na wao katika suala hili ili kuweza kukamilisha masuala hayo kwa usajili.

Kuna Masheha wengine hiki kifungu cha mwanzo hapa ambacho cha Mrajis vizazi na vifo hapa, wengine sijui hawajui mantiki yao, sijui hawajui umuhimu wao, wanakuwa hawatoi *certificate* zile ambazo zinazohusika kwa

mujibu wa sheria kumpa mtu au karatasi za kwenda kumpa mtu ambaye ende kule kunakohusika. Mhe. Spika, nalo hili mimi nalipigia kelele sana lakini niseme juzi tu nimshukuru mheshimiwa wangu Dr. Mwinyi ameniona kuwa Masheha waliokuwa wadhaifu atawaondoa ili wapate utaratibu ambao ule uliowekwa na zile taaluma kwa sababu hawa wanasomeshwa fedha za wanyonge na wafahamu ile taaluma, ndio maana nikawa na wasi wasi hizi taaluma zinawafika. Mhe. Spika, nimshukuru sana Dr. Mwinyi namwambia atimize wajibu wake huyu mtu ahakikishe ameondoka mara moja Sheha wa Kwaalinatu.

Lakini Mhe. Spika, niendelee katika mambo ya usajili wa hati miliki, nishukuru sana kwa sababu ni kweli wasanii wetu hawa na nimshukuru Mkurugenzi muhusika kwa jitihada yake kwa kutishwa kwake lakini hakutetereka alifika pahali kukamilisha kwa mujibu wa sheria kumlinda yule mtu ambaye mwenye hati miliki wa lile suala ambalo kwa mujibu wa sheria tulilopitisha hapa. Hakutetereka amefanya kazi kwa mujibu wake wa sheria na amefika pahali pazuri sana na ninamuomba sana aendelee hivyo hivyo kuwalinda watu kuwagomboa kuwaondoa kwenye umaskini kwa kupitia utajiri kwa kupata hati miliki na kumlindia ile haki ya mali yake ambayo iliyokubalika kwa mujibu wa sheria kufanya *registration*.

Mhe. Spika, nimalizie sasa hapo kwa kumalizia nakuja kwenye Kamisheni, nikitoka hapa ndio naingia kwenye kumalizia, bado muda ninao. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Mhe. Spika, na wao niwashukuru sana lakini nitoe na tahadhari hapa namuomba Katibu wangu na watendaji wao hapa pana dhamana kubwa sana na dhamana yake katika masuala hasa yale ya kutithishiwa.

Mhe. Spika, suala la kurithishwa mtu hasa ya mali ya marehemu, tuogope sana hapa tuwe waadilifu sana, msikubali mashindikizo ya Wakuu wa Wilaya au Wakuu wa Mikoa wanakuwa wengine wana jambo pale ndani yake, wana *interest* ya kitu hawaangalii sheria, wanaangalia *interest* yao, hili suala litamfikisha mtu pabaya, sio pabaya katika serikali hata kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu umedhulumu mwenye haki ya kupewa anakuwa hapewi, anapewa mtu ambaye aliyekuwa hana haki. Kwa kuwa Mkuu wa Wilaya yuko kafuatilia au Mkuu wa Mkoa, ninamuomba sana Katibu wangu mzuri, mtu mahiri na nimeona mtu *standard* kabisa kwa hilo hakubali nalo lakini natoa *attention* tu kuwa afahamu yasitokezee na mengine aendelee na huo huo ukaidi wake wa kutokukubali hafla jambo akiletewa na watendaji wake.

Inawezekana kuwa mtendaji kwa kuwa anakatiwa kitu kidogo tu kwa sababu siku hizi unajua mishahara yenyewe midogo Mhe. Spika, leo kishapewa donge nene hajapata kuona shilingi milioni tatu *dafari* moja, unafikiri Mhe.

Spika, atapinda tu atalihalalisha lile lililokuwa haramu. Atahalalisha lile lililokuwa haram wakati halali lipo halifanyi lile Mheshimwia. Hapa mimi naomba sana jamani waache tamaa hizi si mchezo mali ya yatima kuliwa si kitu cha masihara na tuogope sana na hasa ingewezekana Mhe. Waziri kama kungekuwa kuna jambo katika Wizara yako, hebu tupeni *offer* Baraza la Wawakilishi wote twendeni Makka ikiwezekana kama ipo tupeni sadaka hiyo ya kwenda Makka, lakini hamupigi kofi kwa sababu kwenda Makka hamjawa tayari Wawakilishi wenzangu kwenda Makka. Mhe.Spika, Wawakilishi wako hawajawa tayari kwenda Makka mimi niko tayari kwenda Makka wakati wowote nikipata *offer* hiyo mimi nataka niende mheshimiwa. Sasa kusema la ukweli hili suala ambalo ninamuomba sana Katibu wangu awe mahiri sana kuliangalia.

Nakwenda kwenye suala hili la rasimu ya Katiba. Mhe. Spika, unajua kuna watu wengine huwa wana kumbukumbu za *hansard*. Namalizia Mhe. Spika, hapa sasa hivi mbele yetu tuna rasimu hiyo hapo inakuja ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kabla sijaanza kuchangia hapa naomba sana ninukuu *hansard* zilizopita nyuma ambazo zitakuwa kielelezo chetu sisi hasa watu wa *back benchers* kwa sababu huyo uliosema ni mkubwa zaidi, simsemi lakini miongoni mwetu tumo ndani ya *back bencher*. Mhe. Spika, naomba hivi sisi tunavyojua na mpaka katika vikao vyetu vya kero za muungano tunasema Zanzibar tunahisi ndani ya *BOT* wenzetu mpaka leo wanashindwa kuleta *documents* za vikao vitatu, yaani hawamuheshimu hata yule Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kaitisha vikao vile. Sasa leo suala dogo tu la hisa yetu ambayo kila mtu anaijua tunayo lakini *document* ile ya kuthibitisha mpaka sasa hivi hatujakuwa nayo. Sijui Mhe. Waziri utanieleza nini suala hili. Naomba sana Mhe. Spika.

Lakini nikiendelea kifungu chengine, hivyo Mhe. Spika, wajumbe ambao wana hofu kwamba sijui nani ataitwa, nani atakwita kwa wakati atakayetuita ni huyu ambaye ametupa hiyo kazi, kwa maana hiyo hakuna wa kuitwa na wala tusiogope isipokuwa tujenge hoja ambazo ni za msingi zitakazowasaidia Wazanzibari na Watanzania kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba sana wajumbe wenzangu tusiogope ikifika wakati twende kwenye mabaraza yetu, mwenye kutaka serikali mbili atatoa hoja nzuri, mwenye kutaka serikali tatu atatoa hoja nzuri, mwenye kutaka serikali ya mkataba atatoa hoja nzuri. La msingi hapa tuwe na hoja tujenge hoja kwa lile mtu analolitaka. Naomba tuwe wazi, naomba tusiogope tuijenge Zanzibar yetu kwa maslahi ya nchi yetu. Rasimu imetuongoza kuna masuala mengine yametuweka sawa, kwa hivyo tunastahiki na sisi tuweze kuchangia kwa mujibu wa sheria. Haya maelezo ni ya *hansard* sio ya Mshimba.

Mhe. Spika, niyaeleze hayo ili niweze kuaidia katika muongozo wa kuchangia vizuri katika hao watu wetu. Mhe. Spika, nikushukuru sana na niseme hii kwa mara ya kwanza nitaunga hoja mkono kwa sababu sina mambo mengine yaliyokuwa mazito ya humu niliyoyaweka, mimi mwenyewe isipokuwa baadhi ya mambo tu tutaweza kuyasaidia. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalla kwa kuendelea kuturuzuku neema zake za uhai na uzima tukaendelea na shughuli zetu katika Baraza hili tukufu. Nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji wa pili leo katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Lakini Mhe. Spika, nimpongeze sana Waziri wa Katiba na Sheria kwanza kwa kivazi chake alichokuja nacho leo kuwasilisha bajeti yake. Maana Mhe. Spika, imekuwa kawaida kila mmoja hutafuta suti iliyokuwa nzuri zaidi katika kabati, leo kaamua kutafuta kanzu iliyokuwa inapendeza zaidi halafu akamechisha suruali, kanzu, koti mpaka kofia. Sasa tulikuwa tunaulizana Mhe. Spika, kwamba jana tuliona wazee wa Kitumbatu wanaingia hapa bajeti ikapita kidogo sivyo ilivyotarajiwa. Sijui kama na Mhe. Abubakar naye kanzu na koti hii katika maelekezo ya Mgogoni au vipi, lakini kwa yote ninampongeza kwa namna alivyokuja na inshaalla itakuwa dalili ya kupita vizuri bajeti yake.

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria nilibahatika kwamba ni moja kati ya Wizara nilizokuwa nikizifanyia kazi katika kamati uliyonichagua iliyopita. Moja katika sifa zake mimi nataka niipe haki yake hata sisi tunaopenda kuchokonoa chokonoa vifungu ilikuwa tabu sana kupata vifungu vile ukaweza kuvihoji kwamba labda vimekuzwa sana ama vipi na mara nyingi unakuwa umejiandaa vizuri na maelezo ya kila kifungu ambacho umekiweka. Kwa hivyo kwa hilo ninampongeza hata mara hii nimeangalia angalia sikuona kubwa sana.

Mhe. Spika, katika mchango wangu kwanza naomba nimpe pole Mhe. Waziri kwa mkasa uliomkumba katika wa Mufti Sheikh Fadhil Soraga, ni kitendo cha kinyama, cha kishenzi ambacho kinapaswa kulaaniwa na watu wote wanaopenda amani na wanaothamini utu na ubinadamu kwa mwenzetu.

Mhe. Spika, nakumbuka siku tuliyokwenda kumtizama tuligongana mimi na wewe pale kwake ulitokezea huku na mimi nikatokezea inasikitisha sana. Si kitendo ambacho binadamu yeyote anayejua utu anaweza kumfanyia binadamu mwenzake kwa sababu yoyote ile. Kwa hivyo nimpe pole Mhe. Waziri lakini nimuombe tu, najua serikali inajitahidi lakini niendelee kumuombea tena kwamba wawe karibu naye na huduma zake za kiafya wazipe umuhimu mkubwa ili afya ya Fadhil Soraga irudi katika hali ya

kawaida. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu amrejeshee afya yake ampe uzima, aendelee kujumuika na sisi kama alivyokuwa akijumuika huko nyuma.

Mhe. Spika, kwa sababu nimenza na suala la Ofisi ya Mufti naomba nimalizie hapo hapo machache tu yanayohusu *fee*, nimpongeze vile vile Mhe. Waziri kwa kufanya kazi ambayo tulikuwa tukiizungumza katika kamati iliyopita ya kuhakikisha kwamba anampatia gari Mufti wetu. Kwa sababu ilikuwa haipendezi Mufti katika nchi kama yetu kwa utamaduni wake ni mtu mkubwa kwamba iwe gari yake ni ya kushikilia shikilia tu. Kwa hivyo ninampongeza kwamba kafanikisha suala hilo lakini nimkumbushe tena haidhuru alishatwambia kwamba si lake tena, lakini huko ambapo limepelekwa bado halijapewa kauli mpaka leo. Mhe. Jaku mara nyingi sana alikuja hapa na suala la kuuliza Serikali kwamba nchi kama yetu lini tutayarishe utaratibu wa kusherehekea kuanza kwa mwaka mpya wa Kiislamu *Hijria*.

Mhe. Spika, Waziri alituambia kwamba mwenye uwezo wa kuchagua siku hizi na kuzipendekeza ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini tumeona limechukua muda mrefu halipati jibu, kwa hivyo nilikuwa naomba nilikumbushie hili kwa kupitia kwake au kwa sababu Serikali inawajibika kwa pamoja Ofisi ya Makamu wa Pili atakuja kutujibu na kutuambia hili suala limekwamia wapi mpaka leo. Nikiondoka katika Ofisi ya Mufti naomba nizungumzie Idara ya Mahakama.

Mhe. Spika, hapa vile vile nianze kwanza kwa kupongeza hatua iliyofanyika kubwa ya kuimarisha jengo la Mahakama Kuu pale Vuga ambalo liko katika Jimbo langu la Mji Mkongwe. Mhe. Spika, lile jengo si tu kwamba ni kielelezo cha utoaji haki katika nchi, lakini zaidi ni jengo la kihistoria linaloweka haiba ya mji wetu, lilikuwa katika hali mbaya sana, matengenezo makubwa yamefanyika ndani na sasa hivi wanafanya matengenezo nje naipongeza hatua hiyo. Lakini nilikuwa ninataka nimuulize Mhe. Waziri katika fedha za maendeleo nimeona kwamba matengenezo ya mradi huu kumetengwa 150,000,000/=. Sasa nilitaka anisaidie kwamba je hili ni kwa ajili ya jengo lile tu au na majengo mengine ya Mahakama mbali mbali ambayo tulikuwa tukiyatembelea ambayo yalikuwa haidhirishi, kuna Mahakama ya Mfenesini, Makunduchi tulitembelea katika kamati ile iliyopita na nyengine, hata Pemba kule sijui kiasi gani bajeti hii inategemea itasaidia uimarishaji wa majengo ya Mahakama zile.

Mhe. Spika, katika Idara ya Mahakama vile vile naomba nieleze masikitiko yangu kwamba bado suala la wananchi kulalamikia kwamba Mahakama zetu zimezongwa na rushwa bado lipo. Mhe. Spika, Mahakama ndipo pahala pa mwisho ambapo mnyonge anakimbilia kutegemea kupata haki na Serikali yetu imefanya kubwa sana ya kuimarisha maslahi ya Mahakimu na watendaji

wengine wa Mahakama ili kuondosha tashwishi za rushwa ili haki iweze kutendeka, lakini bado wananchi wana malalamiko. Kwa hivyo hili ninamuomba Waziri akalitazama.

Mhe. Spika, katika hili ninataka nimkumbushe tena Waziri kama nilivyomkumbusha mwaka jana hasa aangalie kwenye Mahakama za Kadhi vile vile. Tumekuwa tukipiga kelele sana Mhe. Spika, kwamba Mahakama za Kadhi ambapo ungetegemea ingekuwa ndio ni kielelezo cha utoaji haki, kwa kwa sababu pale panazungumzwa kutimizwa sheria ya Mwenyezi Mungu lakini wananchi wanapiga kelele sana, talaka zinakuwa zinatoka kama vile njugu, lakini kuna watu wanatuhumu vile vile kwamba hata namna ya uwekaji wa kumbukumbu za ndoa vile vile, kwamba mara nyengine talaka haziko vizuri, watu wanaozeshwa ambao bado kisheria pengine watakuwa hawajaachika, kuna matatizo mengi sana, nilikuwa naomba hili alitazame.

Mhe. Spika, katika hili ninataka nimkumbushe Waziri juu ya kadhia moja. Mwaka jana nilimwambia akaniambia kwamba wanalijua na wanalifuatilia. Nilitaja Mhe. Spika, kadhia ya Kadhi mmoja ambaye alikuwa anasikiliza kesi, ikaonekana kwamba alikuwa na mawasiliano si ya kawaida kwa upande mmoja anaosikiliza kesi na suala lile likafikishwa mpaka Polisi kwa ajili ya kuchunguzwa. Si vizuri Mhe. Spika, kuanza kutaja majina ya Makadhi wetu na Mahakimu wetu lakini mwenyewe analikumbuka kwa sababu mwaka jana alilitolea kauli akasema anaijua, nataka akija aje aniambie suala lile limefikia wapi kwa sababu Mhe. Spika, kama hatuoni kwamba hatua zinachukuliwa hakuweza kuna na nguvu nyengine kuweza kuacha vitendo kama hivi, na kwa sababu mtu kaaminiwa kusimamia uadilifu na utoaji wa haki, halafu akawa anatumia nafasi yake kwamba kapatiwa gari huko pembani akawa anaminya haki ya mtu mwengine, hilo si suala ambalo linaweza kupendeza katika nchi inayofuata utawala wa sheria. Kwa hivyo nilikuwa naomba na hili Mhe. Spika, akija anisaidie.

Mhe. Spika, bado katika Mahakama za Kadhi kuna malalamiko makubwa sana na mara nyengine wale waliokuwa waadilifu wananyang'anywa kesi kwa sababu tu wamekataa hongo au rushwa, kupendelea upande fulani wakahamishwa kuwapa wengine ambao wanaonekana matajiri wanakuwa na sauti kubwa zaidi huko, nilikuwa naomba nipate maelezo.

Mhe. Spika, nije katika Kamisheni ya Wakf. Mimi kidogo natofautiana na iliyokuwa Kamati yangu, sasa hivi siko tena, wamesema kwamba wameangalia upande mmoja zaidi katika suala la nyumba za Wakf kwamba bei zake za kodi ziko chini sana, kwa hivyo Serikali kupitia Kamisheni ya Wakf ziangalie tena. Mhe. Spika, naelewa kwamba nyumba za Wakf si nyumba za Serikali, ni nyumba ambazo zimewekwa na wenyewe

kushughulikia yale mambo ambayo yamewekwa katika wasia uliokuwemo katika ule Wakf wao. Lakini tumesema lazima mambo pia yazingatiwe katika nchi yetu ikiwemo vipato vya wananchi wetu.

Niliwahi kusema Mhe. Spika, kwamba Mji Mkongwe wale waliopewa hizi nyumba za Wakf wakae sio ule Mji Mkongwe waliokuwa wakikaa Ibn Kinana na Ibn Ghuzaima sio ule kuna wananchi wengi wanyonge bado wako pale. Hili nilikuwa nisiliseme lakini kwa sababu Kamati nimesikia imelizungumza nikaona kwa sababu hili nimelifuatilia binafsi kulikuwa na malalamiko, wananchi wale katika Jimbo langu la Mji Mkongwe wakaunda kamati yao tumelifuatilia Mhe. Waziri anajua mpaka tumefika kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, tukafanya kikao cha pamoja lakini ninamshukuru Mhe. Waziri kawa ukweli na uadilifu na muaminifu mpaka tumefanya kikao katika ya uongozi wa wizara yake, Kamisheni ya Wakf, mimi mwenyewe na wananchi wale ambao wanakaa katika nyumba za Wakf tukafanya kikao. Na kulikuwa na makubaliano yalikuwa yamewekwa yanatakelezwa. Nimuombe tu Waziri asije akakubali kushawishika na mapendekezo ya Kamati akayaacha yale makubaliano yetu, ndio nilikuwa nataka kumkumbusha hilo tu katika Baraza hili.

Lakini Mhe. Spika, la pili ambalo Kamati imelisema hili nakubaliana nalo, lile linalohusu nyumba za Wakf kwa maana ya nyumba ambazo zilikuweko katika jumba la Michenzani Na. 10, nyumba ambazo aliyekuwa Rais, Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume, siku anazizundua tulialikwa baadhi yetu pale, alisema kuna watu ambao wamekufa watafutwe warejeshewe haki zao. Sasa tunasikia wakubwa wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati walichukua nyumba zile wakagawana wao, nyumba ambazo ni haki ya watu, ilikuwa kama wenyewe hawajajitokeza zibakie katika amana chini ya Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana mpaka wapatikane wenyewe. Suala hili tumelipigia kelele tangu mimi mjumbe wa kamati mpaka leo nimestaajabu kwamba mpaka leo Kamati inakuja kuikumbusha kwamba bado hazijarejeshwa, kuna nini. Kwa hivyo Mhe. Waziri, hili nataka kauli utuambie Kamisheni ya Wakf iko chini ya dhamana ya Serikali, Wizara ya Ardhi iko chini ya Serikali hiyo hiyo, kuna tatizo gani kwa kauli ambayo imeshatolewa ndani ya Baraza hili kwamba nyumba zile zitarejeshwa kwa aliyekuwa Waziri, samahani Waziri wa sasa hivi Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alitoa ahadi humu ndani kwamba analijua hilo suala wanalifanyia kazi zirejeshwe, kuna uzito gani nyumba zile kurejeshwa kwa wenyewe. Jamani hizi ni haki za watu tutakwenda kuadhibiwa mpaka kesho kama tutaendelea kuzichukua. Nilikuwa nataka kauli katika hilo.

Mhe. Spika, vile vile katika Wakf kuna suala ambalo niliwahi kulizungumza huko nyuma suala la nyumba iliyokuwa ikitumika kama Makao Makuu ya

Wizara ya Mawasiliano ya Uchukuzi, ile nyumba wa Wakf na mpaka mwaka jana nakumbuka ilikuwa inadaiwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano ilikuwa inadaiwa 80,000,000/=. Hebu Waziri akija anisaidie wamelipa, maana isiwe tunawabana wananchi tu huku lakini Serikali inatumia mali za watu ikawa hazilipwi na kuna Wakf ule wa mwenyewe ameweka masharti yake nakumbuka niliuona mimi, kwa sababu muhisika ni katika wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe, hebu akija Mhe. Waziri anisaidie kwamba Wizara ya Mawasiliano imelipa lile deni.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Haki Miliki au Msajili wa Haki Miliki. Kwanza Mhe. Spika, naomba nimpongeza yule mama ambaye anayeongeza pale, wanaposema kwamba wanawake wakikabidhiwa dhamana wanaziweza basi sio Mhe. Fatma Fereji tu mwanamke jasiri, lakini Bi.Mtumwa aliyepewa kuongoza Wakf hii anafanya kazi nzuri sana. Lakini bahati mbaya Mhe. Spika, mimi naona kama vile hatujaipa kipaumbele inayostahiki. Kwa maana ya bajeti ya watumishi, hebu Mhe. Waziri aitupie jicho tena Ofisi hii ya Haki Miliki, sitaki kusema zaidi nafikiri kanifahamu naomba akija aje aniambie, wanachukua hatua gani kuimarisha kwa sababu pale pana haki za watu wetu. Siku hizi watu wengi wanaanza kupata uelewa wa kwenda kusajili kazi zao mbali mbali ambazo zinataka kutunzwa chini ya misingi ya Haki Miliki. Kwa hivyo nasema hebu Mhe. Waziri akija anisaidie ana mpango gani ya kuiendeleza ile ofisi kwa maana ya watumishi lakini hata kwa maana ya bajeti ili kuweza kufanya kazi vizuri, kuwajengea uwezo, kuwapa mafunzo na vitu vyengine kama hivyo.

Mhe. Spika, kuna suala nataka kulizungumza hili si kwa nia ya kuiambia Wizara moja kwa moja lakini kuiambia Serikali. Tulipata fununu Mhe. Spika, na juzi zikanifanya niziamini baada ya mchango mmoja uliotoka humu ndani ya Baraza kuhusiana na Msajili wa Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, kuna malalamiko mengi ya watu kuendelea kupata tabu katika kuthibitishwa vizazi vyao, hasa vizazi kuliko hivyo vifo kwa sababu vifo bado hakujakuwa na hamasa kubwa na nchi yetu kuelimika kwenda kuandikisha, lakini vizazi sababu haki zako nyingi huzipati kama hujapata cheti cha kuzaliwa, kuna kukwamishwa kutoka kwa Masheha huko na watu wengine.

Lakini Mhe. Spika, hata juzi tulijadili kwa urefu hapa kwamba kitambulisho cha Mzanzibari ili ukipate unaanzia na kupata cheti cha kuzaliwa. Sasa juzi hapa palitoka hoja kwamba mambo haya mawili yaunganishwe pamoja, mimi siungi mkono lakini nimeamua niseme hapa kwa sababu tulishaanza kupata mapema sisi wengine kwamba kuna mkakati wa wale wanaopenda kuzuia haki za watu wengine wanaona bado kuna uzito kwa ofisi kubakia katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu wananchi wanakuwa wakipata vyeti vya kuzaliwa tofauti na ilivyokuwa mwanzo. Kwa hivyo inataka ing'olewe

katika Wizara hii ipelekwe kwengine ili wananchi wanyimwe vyeti vya kuzaliwa, wanyimwe pia na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Sasa Waziri akija aniambie sana analijua hili yeye na hao wanaolisukuma hili wana ajenda gani kwa vijana na wananchi wa Zanzibar ambao wanalilia haki zao.

Mhe. Spika, nipongeze vile vile kazi kubwa inayofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali. Ule mradi wa kutaka kuzipa *brand* karafuu za Zanzibar. Nakumbuka mimi nilisikia kupitia kwa wakala huyu, wakati ule ilikuwa bado ni ofisi ya jumla ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Sasa hapa nilikuwa na sababu moja mbali ya pongezi ni kwamba nikiangalia mradi ule wa kuimarisha mazingira ya biadhara una shs.100,000,000/= katika fedha za maendeleo, wakati kuna kazi kubwa sana ilikuwa imepangwa. Nilitaka Mhe. Waziri aje aniambie kwamba hizi ndio alizopewa ama ndio zinatosheleza kufanya mradi huu muhimu ambao ukifanya kazi utajenga mazingira mazuri ya biashara na kukuza uchumi wetu, hebu naomba Waziri akija hili anisaidie.

Mhe. Spika, sasa niende katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwanza nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika ofisi hii na katika sehemu mbali mbali. Mhe. Mwanasheria Mkuu ni kielelezo kwa sisi wengine kwa mtu anavyopaswa kuwajibika. Lakini vile vile uweledi na umahiri wake katika suala hili Mheshimiwa unaonekana. Nataka nimpongeze mahususi kwa maoni yake binafsi aliyoyaandika kuipelekea Tume ya Warioba kuhusiana na mchakato wa Katiba unaoendelea. Mimi niiombe Serikali itumie sana maoni yale katika kufikiria nini kinapaswa kwa haki za Zanzibar katika *process* hii inayoendelea.

Mhe.Spika, vile vile nimevutiwa zaidi kwamba katika hotuba hii ya Mhe. Waziri, katika sehemu ya Mwanasheria Mkuu kakikumbuka na chombo hichi kwa njia nyengine cha Baraza la Wawakilishi. Aliopokumbusha haja ya kuzitunza kumbukumbu za iliyokuwa Baraza la Kutunga Sheria (*Legislative Council*). Mhe. Spika, watu wasiojitambua hawawezi kuwa na thamani mbele ya mtu mwengine na historia ni kielelezo muhimu sana cha binadamu, tunapokwenda katika Mabunge ya wenzetu tunaona jinsi wanavyotunga sheria zao.

Mhe. Spika, mimi na Mhe. Ali Mzee tulialikwa katika ziara ya kwenda kujifunza juu ya suala la haki a kupata habari katika nchi ya India kupitia Baraza la Habari (*Media Council*). Moja katika jambo lililonivutia katika Bunge la India ni kiasi gani wameweka hii *Museum*, Makumbusho hasa ya jinsi historia ya Kibunge na utungaji wa sheria na Katiba ulivyoibuka India. Sisi kwetu hapa hatutungi na hapa nilikuwa naomba, ilikuwa nilisimamie siku ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini nikasema aah! niliache, lakini leo

limenigusa hili kwa sababu Mhe. Hamza jana alizungumza kuhusu kuutunza ule ukumbi uliokuwa wa *LEGICO* pale *Victoria Garden*. Mhe. Mwanasheria Mkuu yeye kazungumzia nyaraka kuanzia mwaka 1910 mpaka 1963, mimi nasema na ule ukumbi wenyewe urejeshwe katika hali yake mtu akija aone kwamba hivi ndio ulivyokuwa.

Mhe. Spika, lakini hata lile Baraza la Wawakilishi la zamani tulilokuwa tukitumia pale Mnazi Mmoja nimeona hata mapato yake ya kukodishwa ukumbi yanaingia katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, wakati lilikuwa lilitumiwa na Baraza la Wawakilishi ile historia mtu akiambiwa Baraza la Wawakilishi leo limefika hadhi hii alijue lilikotokea Chombo cha Kutungia Sheria katika nchi. Kwa hivyo tunapaswa kutunza kumbukumbu. Nampongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba kalifikiria hili na najua anafanya kazi kubwa ya kuzikusanya sheria zote kuanzia miaka ya nyuma ambapo mara ya mwisho ilikuwa mwaka 1958 ndio vilivyochapishwa vitabu vya sheria vya Zanzibar, sasa anataka kuzitayarisha upya, nimpongeze kwa mpango wake wa kuipitia upya sheria ya tafsiri ya sheria.

Mhe. Spika, hapa niombe kwamba sheria hii nadhani ni muhimu sana Waheshimiwa Wawakilishi kuijua na kuifahamu vilivyo. Niombe hasa lile pendekezo alilolitoa Mhe. Mwanasheria Mkuu katika semina kwamba Wawakilishi wapewe semina juu ya sheria hii hasa na pengine kuchapishwa katika vitabu kila mtu awe nayo Mwakilishi hasa ni miongozo wanapotafsiri sheria au kutafsiri Katiba ajue kwamba kisaidizi kile nafikiri muhimu kipatikane.

Mhe. Spika, nina mapendekezo mawili katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Niliyasema siku ambayo tulikuwa tukijadili muswada ule wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Nilikuwa naomba katika muundo wake bado azingatie suala la kuwa na kitengo cha kusimamia mikataba kwa sababu mambo mengi tunaona madudu yanaibuliwa katika Baraza la Wawakilishi ni matatizo ya mikataba katika kukubaliana katika masuala ya majadiliano *negotiation*, lakini baadae namna ya kuiandika mikataba yenyewe. Kwa hiyo nadhani ni muhimu kuwa na kitabu kile ili kama ile sheria inavyotaka kama sasa mambo ya mikataba yote yasikamilike kabla ya kupita katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, jengine ni kuwa na kitengo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kinachoshughulikia masuala ya sheria yanayohusu mafuta ya gesi. Huko tunapokwenda Mhe. Spika, mafuta na gesi kwa Zanzibar zitakuwa ndio muhimili mkubwa wa uchumi wa Zanzibar. Kwa hivyo nilikuwa nadhani kuna haja ya kuwa navyo lakini nataka nimalizie katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kumkumbusha lile ambalo jana Mhe. Mtando alilipigia kelele

sana. Yeye alizungumzia kanuni ya sheria ya utumishi wa umma, lakini tuna tatizo kubwa sana la kutokuwa na kanuni katika sheria nyingi sana ambazo tumezipitisha hapa, kuna sheria nyengine zina miaka mitano kama si kumi chengine ambazo hazijatungiwa kanuni mpaka leo na nyengine ni sheria muhimu sana Mhe. Spika. Sheria ya utumishi wa umma ni muhimu lakini hata sheria kwa mfano ile ya usafiri baharini, ili ifanye kazi vizuri maana tumeshakumbana na ajali hapa, kanuni zake ni muhimu zimekaa muda mrefu tumeambiwa sasa zinafanyiwa kazi, lakini ni muhimu sana karibu zote zikapitiwa tukajua katika sheria mbali mbali kanuni gani zinakosekana zile muhimu ziweze kutungwa, na pengine si vibaya kukawa na kitengo maalum katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kama hakipo ambacho kinafanya hiyo tu ya kupitia sheria mbali mbali na kujua kanuni zake ambazo zinapaswa ziwepo.

Mhe. Spika, haraka haraka niende katika ofisi ya *DPP*. Mimi niipongeze vile vile ofisi hii na ofisi hii imepata bahati ilianzishwa na Mwanasheria Mahiri Mhe. Othman Masoud ambaye sasa hivi ni Mwanasheria Mkuu wetu na sasa amempokeza kijiti Mwanasheria mwengine vile vile makini na mahiri Mhe. Ibrahim Mzee Ibrahim ambaye alikuwa Katibu wetu wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, ile hatua ya kuanzisha kituo cha mafunzo na utafiti wa sheria ni hatua ya kupongezwa kabisa, inatusaidia sana hivi sasa. Nilikuwa najiuliza kazi hii nzuri nzito, kazi ya kusimamia kwamba masuala ya mashtaka sasa yasimamiwe kiraia mbona haiendani na namna ya kulinda masuala yao watu wa ofisi hii.

Mhe. Spika, tunapozungumzia kuimarisha utoaji wa haki kwa kuzuia rushwa Mahakamani kwa kutengeneza maslahi yao basi pia tutizame vile vile kwamba wanaoendesha mashtaka nao pia wasije wakawa wakaingia na vishawishi vya rushwa, kwa hivyo maslahi yao yanapaswa yawe mazuri. Lakini sio hilo tu hawa ndio wanaoendesha mashtaka wanaweza kujenga uadui na watu wengi huko nje hasa kwa sababu tunaambiwa zaidi ya asilimia 80 ya kesi zinazoshughulikiwa bado kama si tisini ni kesi zinazohusiana na masuala ya jinai, kwa hiyo maslahi yao lazima yawe mazuri.

Mhe. Spika, nimejaribu kufanya utafiti mdogo kwamba kwenye Mahakimu kule si vizuri kutaja viwango vya mishahara hapa lakini wameongezewa viwango vikubwa tu, sitaki kuvitaja kwa sababu nalinda ile haki ya *privacy* ya mtu na mshahara wake. Lakini ukija ukilinganisha na viwango vya mishahara vya waendesha mashtaka bado viko chini sana. Mhe. Spika, hili nitalitaja kwa sababu hivi navitetea kwamba leo bado tunawalipa Ma-*DPP* wetu mshahara wa 400,000/= huku kuna milioni na kitu huyu anapewa 400,000/=, maslahi yao yameboreshwa au yamefanywa kuwa mazuri zaidi kwa kuongezewa posho. Mhe. Spika, hata posho yenyewe hailingani na posho wanayopewa

watu wengine, hawa kwa mfano katika Idara ya Mahakama lakini tatizo linakuja kwamba posho haitamsaidia wakati wa mwisho akistaafu huyu, kwa hiyo naona hili ni muhimu sana tukalitazama na atakapokuja Waziri naomba anisaidie hili kwamba wanafanya kazi kiasi gani kuweza kufikia hili.

Lakini jengine katika *DPP* Mhe. Spika, ofisi muhimu kama hii ina wafanyakazi muhimu wa utoaji wa haki siridhiki na uingizaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, nimeulizia gharama za matumizi mengine *OC*, ilikisiwa bajeti yao wapate shs.351,000,000/= fedha za *OC* mwaka jana lakini mpaka Juni wamefunga hesabu wameingiziwa shs.261,564,840/=, kuna upungufu wa shs.98,435,160/=, hizi ni fedha nyingi kwa ofisi kama hii. Mimi nadhani katika kuipa kipa umbele inapaswa itizamwe ofisi hii ambayo inagusa maisha ya watu na utoaji wa haki. Mhe. Spika, nilikuwa nadhani hili niliseme hili ni muhimu sana kwa maslahi yao na nitaomba Waziri akija anipe maelezo.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, la rasimu ya Katiba. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake katuambia kwamba rasimu imetoka na naam imetoka na sisi tumepata nakala na wananchi wengine wanazo nakala zao huko. Mimi niungane mkono na maelezo aliyoyazungumza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Spika, tumepiga kelele siku nyingi Zanzibar, hatimae fursa hii imekuja baada ya miaka 50, tukiichezea itapita miaka mengine pengine hamsini kama si mia kuipata fursa kama hii. Hofu yangu ni kwamba bado Zanzibar tunaongozwa sana na utashi wa kisiasa katika kujadili masuala kama haya.

Mhe. Spika, si vibaya kutoa mfano. Tukizungumzia sera ya Chama cha Mapinduzi inasema ni serikali mbili, wengine wanasema kuelekea moja huko nyuma iliwahi kuzungumzwa hivyo mwaka 1994 wakati wa mjadala wa G55. Sera ya CUF, Chama chengine ambacho hapa Barazani kimo ni Serikali tatu, lakini wananchi wa Zanzibar tunaojadili wengi wamezungumza masuala yaayohusu haki zetu na katika hili Mhe. Spika, nikupongeze na wewe vile vile na Kamati yako ya Uongozi wa Baraza hili, mlipopeleka maoni mlikwepa kuhusishwa na vyama vya siasa na sera zake na mkakataa kuzungumzia msimamo fulani wa muundo utawakwaza wajumbe fulani na ukawafurahisha, mkachukua misingi ambayo mnataka izingatiwe katika rasimu ile na kwa kiasi fulani misingi ile imezingatiwa lakini bado haijatimia.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nadhani nitoe wito hapa kwa wananchi wa Zanzibar mpaka sisi Wawakilishi, wananchi wa Zanzibar kama kuna chombo wanakiamini zaidi katika kusimamia haki zao basi ni chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. Sasa Mhe. Spika, nasema ile *spirit* tuliyoionesha mwaka jana

wakati tunajadili hapa, nakumbuka alipochangia Mhe. Salmin Awadh mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi lakini tulikuwa tukimshangiria sote, kwa sababu gani hakuzungumza utashi wowote na mwaka jana nilipokuwa nikijadili hapa tuliweka upande zile sera zetu. Mimi nilikuwa nadhani ni muhimu Mhe. Spika, kuangalia maslahi yetu kuliko sera zetu. Mimi nimeipitia sana rasimu hii, bado kuna maeneo yamejirekebisha lakini bado kuna maeneo mengi ambayo ni muhimu Zanzibar kukamata wenyewe mamlaka yake.

Mhe. Spika, tumeona tunavyokwazwa kiuchumi hatuwezi kusonga mbele kama hatujapata baadhi ya mamlaka. Suala la sarafu na Benki Kuu kuendelea kuwa la muungano, mimi binafsi nadhani kwamba itakuwa bado Zanzibar haijafanya kitu. Suala la Mambo ya Nje kwamba bado linadhibitiwa na muungano bado Zanzibar itakuwa haijafanya kitu, ile kupewa ushirikiano wa kimataifa Mhe. Spika, tusidanganyane kwamba tumeweze kufaidi haki zile, kwa sababu utapoambiwa unaweza kujiunga na Jumuiya za Kimataifa kwa mambo yasiyokuwa ya muungano inategemea sheria au kanuni inayoongoza hiyo Jumuiya ya Kimataifa. Leo tuchukue mfano mdogo tu. Michezo si suala la muungano, tumetaka kujiunga *FIFA* leo miaka mingapi Mhe. Spika, tumeshindwa kujiunga na *FIFA*, kwa sababu sheria na kanuni za *FIFA* zinataka ili ujiunge uwe na mamlaka kamili na ndivyo hivyo hivyo itakavyokuwa kwa afya huwezi kuwa mwanachama wa Shirika la Afya Duniani (*WHO)* ikiwa nchi yako haina mamlaka kamili na hivyo hivyo itakuwa katika jumuiya nyengine kwa mfano katika kilimo ya *FAO* na nyenginezo, lakini hata suala la uraia na uhamiaji.

Mhe. Spika, sisi ni kisiwa huwezi kulinganisha na ukubwa wa Tanganyika. Tuna suala la haki zetu za kiraia hapa, suala la ardhi lakini hata udhibiti wa uhamiaji katika kisiwa chetu au visiwa vyetu. Nilikuwa nasema masuala haya matatu. Sarafu-Benki Kuu, Mambo ya Nje, Uraia na Uhamiaji bado inatakiwa tuangalie kwa umakini sana tunapoijadili rasimu hii katika kuzingatia kwamba Zanzibar inapaswa irejeshe mamlaka yake ambayo itaweza kujikwamua kiuchumi na kusonga mbele.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema tena nampongeza Mhe. Waziri kwa kazi nzuri, zile hoja ambazo nimezitolea maelezo nitaomba akija anisaidie, na baada ya kusema hayo nasema naiunga mkono hoja kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe walionituma kuja hapa kwa asilimia 100. Nakushuru sana.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ambayo iko mbele yetu. Ili nisipoteze muda naomba nianze moja kwa moja na nitaanza na ukurasa wa 36 kwenye Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Spika, afisi hii ni muhimu sana kutokana na kazi zake inazofanya. Kwa sababu chemchemu ya kujua idadi ya watu wengi kama ingekuwa ofisi hii inafanya kazi zake vizuri, inawezeshwa namna ya kufanya kazi zake vizuri na ikawa wananchi wana taaluma ya kutosha basi ingekuwa hatuna kazi ya kufanya sensa ya kupita kuhesabiana huko majumbani. Ilikuwa twende pale tuvute *register* lile la vizazi, tuvute *register* la vifo tujue tu kuna watu wangapi wamezaliwa, wangapi wamekufa, takwimu iweze kupatikana. Lakini kinachokwaza kwanza ni uwezo wa ofisi ile kufanya kazi zake vizuri na hata mazingira ya kufanyia kazi.

Kwa sababu ukienda pale ofisi kuu kipindi cha mvua na wewe umo katika jengo lile ni afadhali uwe chini ya mti utakuwa huroi kuliko kukaa katika ofisi ile pale, jambo ambalo kwa kweli linatutia mashaka ya hata zile kumbukumbu zilizomo pale. Mimi nadhani serikali ingejitahidi kwa ofisi muhimu kama hii wakatafuta jengo ambalo lina uhifadhi mzuri sana wa kumbukumbu za vizazi na vifo ni mambo muhimu sana.

Lakini la pili changamoto nyengine ambayo imo katika ofisi ile taaluma za watu wetu, hii hasa imekuja kuonekana wakati huu wa kutafuta vitambulisho vya kupigia kura na vya Mzanzibari. Tumekuja kugundua kwamba kumbe kuna watu wengi sana hawana taaluma ya kusajili vizazi vyao, lakini pia kuna watu wengi hawana taaluma ya kusajili ndoa zao, talaka zao, vifo vyao. Kwa hivyo, nadhani kuna tatizo kubwa sana la taaluma na nilikuwa nafikiria mimi ofisi hii ingewezeshwa ikatoa taaluma ya kutosha. Na katika ulimwengu wetu huu wa sasa tusitamanie sana jamani kutumia vipindi vya redio, maana ukiwauliza mmetoa taaluma wanasema ndio, tumerusha vipindi vingapi, kuna watu hawasikilizi redio katika nchi hii, kuna watu hawana hata ile faragha ya kuangalia televisheni. Mimi nadhani waandae *program* za kushuka huko kwenye masheha chini huko, ili masheha wakusanye watu wao. Watu wa mrajis waweze kutoa taaluma zao kule kuliko kutamania mambo haya. Mimi binafsi naweza kukaa siku tatu au nne sijatizama TV wala sisikilizi redio.

Jambo jengine labda niwashukuru kidogo kwa kuimarisha ofisi zao za wilayani. Wamejitahidi hicho kidogo walichokipata lakini wameweza kutengeneza ofisi nzuri za kuweza kusajili vizazi na vifo kule mawilayani. Katika hili Mhe. Spika, nilitaka niseme ni jambo zuri sana kwa sababu linarahisisha wananchi kuweza kupata huduma kwa wale ambao wamezinduka wanataka kusajili vizazi vyao kupata huduma yao kwa karibu zaidi na kwa urahisi. Lakini sasa katika hili nataka nitahadharishe jambo moja, lazima kuwe na uratibu wa karibu sana wa mrajis mwenyewe.

Kwa sababu Mhe. Spika, kunanuka harufu mbaya mawilayani mwetu. Wanatumia fursa hii ya kuweza kutayarisha vyeti vibaya, wanatumia fursa vibaya. Sasa nilikuwa nadhani Mrajis atayarishe utaratibu utakaomuwezesha yeye kupata taarifa za vizazi ambavyo vimesajiliwa katika kila wilaya na ikiwezekana yeye mwenyewe ndio awe *authority* wa mwisho, kama kuna saini yake, kama muhuri wake, kama jambo gani lakini yeye awe ni mtu wa mwisho wa kukitambua kile kizazi kilichozaliwa au cheti kilichoandikishwa. Vyenginevyo akianza kuwaachia tu watu wa wilayani wanaweza wakasajili watu wasiokuwepo, wanaweza wakasajili watu wasiostahiki mambo ambayo siku zote yanatuletea matatizo katika maisha yetu ya kila siku.

Sasa nilikuwa namuomba sana Mrajis hilo aliangalie na ikiwezekana kuwe na utaratibu maalum ambao mwenyewe ataujua, lakini ahakikise kama kila kinachoandikishwa kule wilayani basi yeye kama Mrajis taarifa anazo na yeye ndio anayetoa amri ya mwisho.

Mhe. Spika, nikiacha hapo haraka haraka niende kwenye Mahkama. Mahkama imeelezwa katika ukurasa wa 14. Katika hili mimi nina masikitiko tu kwamba kwa kweli Mahkama zetu hazijatupiwa jicho la rehma, Mahakimu wanafanya kazi katika miundombinu mibovu sana.

Hivi karibuni Mhe. Spika, Kamati yako ya Katiba, Sheria na Utawala tulifanya ziara katika baadhi ya Mahkama hizi za wilaya, lakini tulipofika Mwanakwerekwe tulikamata mikono kichwani. Kuna kijichumba kidogo humo humo polisi wanakaa, waendesha mashtaka wanakaa humo, mashahidi wanakaa humo, chumba kidogo, *exhibit* zile mizigo ya kuni, nondo, pombe za kienyeji zilizokamatwa kamatwa zote ziko humo; yaani hatari kubwa, ukienda pale wewe kama afya yako inaweza kuathirika kwa muda mfupi basi unaweza siku ile ile ukapata mafua mle. Mimi nashangaa sijui wanafanya kazi vipi.

Sasa kwa kweli ule si ubinadamu na sasa hili Mhe. Spika, ukilioanisha na fungu lao la pesa za maendeleo walizopewa kwa kweli unaweza ukaona huruma sana. Kwa sababu mwaka uliopita huu waliidhinishiwa kupata shilingi 600 milioni fedha za maendeleo, lakini hadi kufikia mwezi wa Machi

walizopewa ni shilingi milioni mia moja. Sasa shilingi milioni mia moja hata ukiwa hamjengi, hamtengenezi, utakuwa mnawaonea bure pesa hawakupewa.

Mimi nilikua nadhani Wizara ya Fedha mambo kama haya au sijui wanaichukia hii Mahkama, mimi sidhani kama ni wasia mzuri. Kwa sababu tusifikirie tu kama kule Mahkamani au jela hatukutengenezi kwa sababu wanaokwenda kule ni watu wakorofi, watu wahuni, siku nyengine Mhe. Spika, wanaweza kwenda watu na heshima zao kule na wakajisikia vibaya, hao ambao wanaidhinisha pesa siku nyengine wanaweza wakaishia kule kule. Sasa mimi nadhani tusiifanyie vibaya Mahkama tujitahidi kutoa pesa hizi kama ambavyo zinaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi na hatimaye waweze kutengeneza mazingira mazuri ya kuweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, Mahkama ni chombo muhimu sana na kama Mahkama itaweza kufanya kazi vizuri ni nyezo muhimu sana ya kulinda amani na utulivu wa nchi yetu. Na ikiteleza Mahkama kufanya kazi vizuri basi kinachoweza kutokea ni balaa katika nchi. Sasa nadhani wangetizamwa kwa jicho zuri.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, nataka nizungumze ukurasa wa 30 kwenye Ofisi ya Mufti. Mhe. Spika, mimi nasikitishwa sana na serikali yetu, kwamba hii Ofisi ya Mufti haijawezeshwa kufanya kazi na Mhe. Spika, mimi nataka niseme kuna ofisi muhimu sana katika nchi yetu ofisi ambayo kwa upande mwengine inaweza ikasaidia sana kulinda amani ya nchi yetu basi ni ofisi hii ya Mufti. Hii ina wataalamu wa dini wakubwa sana na ikiwezeshwa ikapanua wigo wa wataalamu wake na wakaweza kuwafikia watu, basi nchi yetu inaweza kuepukana na mambo mengi mabaya mabaya. Sasa tatizo lake imewekwa pale kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kama nembo tu ya kuonesha kama ndani ya nchi hii kuna kijiofisi kinachoshughulikia mambo ya dini, lakini kwa kweli haiwezeshwi na haiwezi kufanya majukumu yake ipasavyo hata siku moja kwa pesa ambazo zinawekwa.

Mhe. Spika, nchi hii ya Zanzibar ina Waislamu asilimia 99, sasa ukishakuwa na Waislamu wa namna hiyo unapaswa sasa kufanya uratibu wa shughuli za Kiislamu, wala mimi siungi mkono hata siku moja ile kauli ambayo tumezowea kuambiwa kuwa serikali haina dini.

Mhe. Spika, serikali ni watu, watu wenyewe wanayo dini, sasa ukisema serikali haina dini mimi nadhani kuna tatizo la ufahamu wa hii sentensi kuwa serikali haina dini. Mimi nadhani waliosema hivi kama walikusudia kwamba serikali haitapendelea dini yoyote ni sawa, lakini kwamba serikali haina dini ni kwamba iache shughuli za dini kushughulikia hii si kweli. Serikali inaunga taasisi kwa mujibu wa *activity* za watu katika nchi.

Kule Saudia kuna wizara nzima ya kushughulikia Msikiti wa Makka na Madina tu, kwa sababu ya umuhimu wa zile *activities* za ile misikiti miwili. Hapa Waislamu asilimia 99 wanaswali, wanajenga misikiti, wanajenga madrasa, wanaunda taasisi za zakka, taasisi za hijja, halafu useme maana yeka uache tu hivi hivi kufanya uratibu. Mimi nadhani si sahihi, si sahihi kabisa. Ofisi ya Muft ina kazi kubwa sana ya kufanya katika nchi hii. Kwa mujibu wa takwimu hizi ambazo nimeziona kwenye kitabu kuna misikiti 217 nchi nzima na hii inawezekana sana ikawa zaidi ya hii, lakini kuna madrasa 2431 ambazo zinafundisha watoto. Sasa zote hizi ziko chini ya majukumu ya Ofisi ya Mufti kuzipitia kuangalia uratibu wake zinatekeleza vipi shughuli hizo. Sasa kijiofisi kile kina watu wachache hakina vifaa vya kufanyia kazi, hakuna ile nguvu kazi ya watu. Mimi nadhani tuangalie tena Mhe. Spika, kwa sababu ofisi hii ina mambo mengi ya kufanya.

Kwa mfano, siku hizi kuna wimbi kubwa sana la wahuni, mimi nawaita wahuni ambao wanafungua *asbaab* za madrasa za Qur-an lakini kumbe si walimu wa Qur-an walio na nia safi ya kusomesha Qur-an. Lakini wanafungua madrasa, wanakusanya watoto wa watu halafu wanawafanyia vitendo vya kishenzi. Wanafanya vitendo vya kishenzi Mhe. Spika, kwa kweli hili wimbi sasa ni kubwa na linatishia amani ya jamii yetu. Hii ni kazi ya Mufti kufuatilia, na mimi nilikuwa nakiri Mhe. Spika, sasa hivi lazima Mufti akaze buti sawa sawa, akaze buti afanye uratibu wa madrasa moja moja na ikiwezekana kila madrasa aweke mtu maalum wa kufuatilia nyendo maalum za madrasa ile, tusipoangalia Mhe. Spika, kwa *rate* inavyokwenda sasa hivi baada ya miaka fulani ijayo tutakuwa na jamii ya watu goi goi ambao *mushkel*, jambo ambalo ni hatari sana katika maisha yetu.

Hii mimi nimejenga mashaka sana kwamba sijui kama hakuna mkakati wa makusudi, nina wasi wasi mkubwa, nimo katika kufanya utafiti na kuna siku nitakuja kutoa matokeo ya utafiti wangu. Lakini nina wasi wasi mkubwa kama kuna mkakati makusudi wa kuharibu watoto wetu. Sasa mimi naomba sana Ofisi ya Mufti sasa iwezeshwe tena, iwezeshwe hasa si mchezo!

Mhe. Spika, inasikitisha sana kuona ofisi hii inapewa pesa mwaka jana walizoziomba kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa shilingi 103 milioni na 26 elfu. Lakini walichokipata mpaka kufikia mwezi wa Machi ilikuwa ni shilingi 40,562,700, hiyo ni asilimia 39. Sasa hebu na tuangalie pesa hizi zitamuwezeshaje Mufti kupita kila kona, kila kijiji cha nchi hii maana kila kijiji kuna msikiti, kila kijiji kina madrasa si moja wala si mbili, watawezaje kufanya shughuli kwa namna hii?

Sasa mwaka huu naanza kusema mimi kwamba ikiwa *rate* itakuwa ni hii kwa sababu hata mwaka huu shilingi yao hii hapa nimeiona, shilingi 183 milioni,

sasa ikiwa *rate* ni hii mimi mwakani natangaza kabisa kama nitakuwa hai bajeti kuu ya serikali mimi Abdalla Juma sitoipitisha mpaka anihakikishie fungu la Mufti limeongezwa pesa za kutosha kabisa kufanyia kazi kwa ajili ya kurekebisha jamii yetu. Hilo nalitangaza toka mwaka huu kabisa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na nataka niseme kwamba ofisi hii kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa ina bahati ya kupata watu wazuri. Tulianza na Mwanasheria Mkuu ambaye ni muasisi hasa wa ofisi hii, alifanya kazi kubwa sana kwa mafanikio makubwa na hatimaye ikapata Mkurugenzi mwengine ambaye pia kwa kiwango kikubwa naye ni mtu makini na mtu ambaye ni *committed* sana kwa kazi zake.

Mhe. Spika, ofisi hii ni katika ofisi zinazobanwabanwa sana kwa *ceiling* na tukitaka tusitake hii ofisi bado ni changa inahitaji kukua ili kuenea nchi nzima, mpaka leo hawajaweza kueneza wanasheria katika nchi nzima. Sasa mimi nadhani mpango huu wa kubinya pesa hatuwezi kuendelea, kwa sababu tuna changamoto nyingi sana katika mwenendo mzima wa kesi zetu katika nchi. Kesi zinakuwa zinachelewa sana, wakati mwengine kesi zilisimamiwa na watu wasiokuwa na taaluma ya kisheria ya kutosha. Kwa hivyo, nadhani ofisi hii ni muhimu iangaliwe katika *priority* ya kuhakikisha kama nayo inaweza kufanya kazi na kufanikisha mwenendo mzima wa kesi.

Wanasheria wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanafanya kazi katika mazingira ya hatari. Kwa sababu katika kusimamia kesi wanaoshinda ni watu wawili, sasa kadiri utakavyosimamia akipata haki mmoja mmoja huwa hapendezi, na kwa sababu hapendezi atakuona wewe mbaya mara nyengine anatishia maisha yako. Kwa hivyo, kuna haja ya kupata lile posho maalum ambalo litawafanya hawa wawe na moyo wa kufanya kazi, vyenginevyo Mkurugenzi wa Mashtaka ataendelea kushtaki kila siku kwamba wataalamu wake wa sheria wanamkimbia. Kwa sababu mtu yeyote yule Mhe. Spika, hayuko tayari kujiona anahatarisha maisha yake katika kiwango hiki.

Mwaka jana hawa tuliidhinisha shilingi 250 milioni kwa ajili ya *issue* zao za maendeleo. Lakini mpaka kufikia mwezi wa Machi walipewa shilingi milioni 100, 50 wakazitumia Unguja na 50 wakatumia Pemba. Shughuli walizokusudia kuzipanga hazikufanyika kwa ukamilifu, matokeo yake pesa ambazo tutawaidhinishia mwaka huu inabidi waanze kulipa vile viporo vilivyopita kuliko mipango yao ya mara hii waliyokusudia.

Lakini pamoja na sifa ambazo nimezitoa Mhe. Spika, kwa ofisi hii kuna jambo moja mimi linanipa mashaka kidogo na hili nilisema niliseme kwa makusudi. Unajua katika kusimamia haki unatakiwa ufuate *principle* na

kanuni za haki, na katika hilo mawazo ya mtu binafsi hayana nafasi. Sasa Mhe. Spika, mimi sifurahishwi hata kidogo na watu kuwaweka ndani bila ya kuwapatia dhamana kwa muda mrefu na hili jambo bado lipo, sitaki kusema ni akina nani lakini kuna watu wako ndani kwa muda mrefu kitu ambacho kiko kinyume na kanuni zile za kuweka watu ndani.

Nilikuwa najiuliza kwa nini kesi zao haziendeshwi? Maana kuna watu maalum sheria zinasema kwamba huyu asipewe dhamana, mwenye sifa hii na hii asipewe dhamana, lakini walioko nje ya sifa hizo wana haki ya kupewa dhamana, kwa nini hawapewi dhamana mpaka leo. Mimi nadhani hii si nzuri, lazima niseme kwamba kwa kweli hapa ofisi yetu ambayo tunaisifu kila siku hapa haijafanya vizuri kabisa.

Kwa hivyo, kwa ushauri wangu mimi nadhani wapewe dhamana halafu watu waendelee na kesi zao mpaka zitakapomalizika wasinyimwe dhamana kabisa.

Mhe. Spika, jambo la mwisho kabisa najua muda ushakwenda sana ambalo nataka kusema ni suala la Rasimu ya Katiba. Nitakuwa sijatenda haki kama nitakaa kitako bila ya kuzungumza lolote. Mhe. Spika, rasimu ya katiba ipo na sasa imo katika utaratibu wa kupelekwa kwenye Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na hatimaye kutakuwa na Bunge la Katiba ambalo hilo litakuwa linatushirikisha sisi Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Spika, hii ni fursa muhimu sana ya kumaliza matatizo yetu ya Muungano. Tunapaswa Wazanzibari kuwa makini sana lakini hasa sisi Wawakilishi tunapaswa kuwa makini zaidi. Kwa sababu kila unayemuona humu kaaminiwa na watu zaidi ya 7000 huko nyuma, kwa hivyo kabeba mawazo ya watu 7000. Sasa mimi nadhani tuitumie nafasi hii kwa maslahi ya watu wetu, wala tusijaribu hata kidogo kuangalia mimi nikisema hivi itakuwa nini hili si muhimu, muhimu ni kuhakikisha kwamba yale mawazo ambayo watu wetu wanayo ndio tuyafanyie kazi.

Nataka niseme Mhe. Spika, tuna bahati moja kubwa sana Zanzibar, Wazanzibari mpaka watoto wadogo akili zao hasa kisiasa zime-*mature* sana, hata useme nini watajua kwamba huyu anakusudia kusema nini. Kwa hivyo, mimi niwatahadharishe wenzangu kwamba sisi tumeletwa hapa kwa imani za watu na miongoni mwa walilotuletea ni kuwalindia haki zao, tukija kufanya vyengine basi watu watatuhukumu huo ndio ukweli.

Kwa hivyo, tuwe macho tufanye kazi kwa makini, rasimu tuipitie ile, na siku ikifika Bunge likiitishwa twende tukapeleke yale ambayo watu wanayadai.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi na kwa niaba ya watu wa Jimbo la Chonga naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametulaza na kutuamsha salama akatufikisha hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa na afya njema. Pia nimpongeze Mhe. Waziri jinsi ya uwasilishaji wake wa hotuba yake kwa umakini mkubwa wa hali ya juu.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze ukurasa wa 37 kwenye matatizo ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Bado suala hili tutaendelea kulipigania na kulizungumza kila mtu, kwa sababu ni haki ya kila mmoja wetu. Katika suala hili Mhe. Spika, nitazungumzia ndani ya Wilaya yangu ya Wete, ndani ya wilaya yangu bado kuna matatizo makubwa ya watu kupata vyeti vya kuzaliwa.

Zamani Mhe. Spika, hao tunaowapigia kelele hivi sasa ni watu ambao walikuwa hawajaibuka na kutafuta vyeti vya kuzaliwa yaani wazazi wetu, lakini vizazi vya sasa kila mmoja anapojifungua tu, tayari anaanza kupeleka vitambulisho vyake kwa ajili ya kupata vyeti vya kuzaliwa kwa ajili ya mtoto wake. Lakini kwa bahati mbaya sana kuna watu tokea unapeleka kirisiti kile cha kutafuta cheti cha kuzaliwa mpaka anakaribia kwenda *nursery* cheti bado hakijapatikana.

Mhe. Spika, sizungumzi hili kwa sababu ya kutilia shaka hili ni jambo ambalo naliona mwenyewe binafsi, nina mtoto ambaye kazaliwa toka mwaka 2010 mpaka sasa hivi mwaka 2013 cheti chake bado kimeshindikana kupatikana. Sasa najitolea mfano mimi mwenyewe, mimi mwenyewe kwa sababu nafanya kazi jirani na Ofisi ya Vizazi na Vifo pale Wete, sasa kila siku ninayokwenda Wete nafuatilia kile cheti. Sasa ninawatizama wengine masikini za Mungu waliokuwa wao pale Wete wanaweza wakakaa zaidi ya mwezi hawajaenda na kila siku ukienda utaambiwa njoo baada ya wiki mbili, baada ya wiki tatu, njoo wiki nne. Sasa hili ni tatizo na linawapa watu usumbufu masikini za Mungu mpaka mtu anakata tamaa na cheti kinapotea.

Mhe. Spika, nina hofu ya watu katika mtiririko huu na ugumu uliopo katika kupata cheti cha kuzaliwa yakaja yakawakuta vizazi vyetu yanayotukuta sasa katika kutafuta kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, sababu kubwa ni cheti cha kuzaliwa. Wengine baada ya kwishapeleka kile kirisiti kwa Sheha kinachukua muda, sheha ndiye anayechukua kile kirisiti na buku kulipeleka wilayani, na wilayani litakaa na ukienda mara nyengine unaambiwa cheti chako hakipo kabisa. Yeye Mhe. Waziri hapa katika kitabu chake

kazungumzia mambo ya upungufu wa magamba na mambo mengine, lakini mimi naona mbali na hayo bado kuna na tatizo jengine.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri aliangalie sana hili kuhusu upatikanaji wa cheti. Sasa kwa hili naomba kusikia kauli ya Mhe. Waziri kwa nini katika Wilaya yangu ya Wete kukawa na usumbufu mkubwa wa upatikanaji wa cheti cha kuzaliwa? Hapa naomba Mhe. Waziri anipe maelezo sahihi yatakayonifurahisha na kama hayajanifurahisha basi kwa hapa mimi naona nitaondoa shilingi katika kifungu hiki.

Mhe. Spika, eneo jengine nitakuja kwenye Jengo la Mahkama. Jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba pia ni bovu ni jengo la muda mrefu na kongwe, linahitaji matengenezo makubwa. Sasa namuomba Mhe. Waziri katika hili aliangalie kwa umakini sana na ikiwezekana katika mwaka huu wa fedha angalau lifanyiwe chochote lile jengo limeshazeeka ni la muda mrefu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 33 kuna Taasisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali. Kwa hakika taasisi hii ni muhimu sana, lakini sasa bado wananchi wetu hawajaifahamu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aandae angalau vipindi vya redio na televisheni kuwaelimisha jamii ili waweze kuitumia hii taasisi.

Mhe. Spika, eneo jengine nataka niingie katika kesi za udhalilishaji. Kesi za udhalilishaji wa kijinsia Mhe. Spika, imekuwa ni kero kubwa, imekuwa ni balaa halisi, halitabiriki hatujui hata tulielewe vipi.

Mhe. Spika, katika hili maana mimi sijui niseme vipi na sijui hata kuzungumza watoto wetu wanaharibika, wanaharibiwa, wanaowaharibu ni watu wazima na akili zao, na hawachagui mwanamke wala mwanamme ilimradi tumeingiwa na janga kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika hili inafika wakati katika mahakama yenyewe unapeleka zile kesi ule ucheleweshaji wa zile kesi kwa masuala haya zikichukua muda mrefu wale watu wanakata tamaa hasa ukizingatia kina mama wanaona tabu muda umeshakuwa mrefu hawana uwezo halafu wanaona aibu inafika, wakati wanasameheana wenyewe kwa wenyewe na kesi zile zinahukumiwa nje ya mahakama.

Mhe. Spika, hili ni tatizo tena kubwa kwa sababu unapohukumu kesi hizi nje ya mahakama basi hili haliondoi tatizo ila linaongeza tatizo. Kwa sababu watu wanaonekana ni mazoea kila mtu anakuhumiwa nje hivi hivi basi na yeye atafanya.
Sasa naomba Mhe. Waziri katika hili kwa sababu baada ya kwishadhalilishwa hawa watoto na kesi hizi huhukumiwa nje ya mahakama yule mtu

aliyetendewa lile tendo anakuwa hana umadhubuti masikini wa hatima yake, ni mtihani kila mmoja anamuoneshea kidole. Sasa kiukweli hili ni tatizo.

Sasa matatizo haya yanaongezeka baada ya kupungua, je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kuandaa na kuratibu ili kuondosha tatizo ambalo kila siku linakuwa na kuendelea ndani ya nchi yetu na kututilia aibu na kutudhalilishia watoto wetu?

Mhe. Spika, pia nataka nielewe katika Mahakama ya Ardhi hapa kidogo. Nataka kuelewa shughuli za Mahakama ya Ardhi zinaripotiwa wapi Wizara ya Ardhi au Wizara ya Katiba na Sheria? Kama ni katika Wizara ya Katiba na Sheria sijaona maelezo yanayohusiana na Mahakama hizi za Mashamba na Ardhi, kwa hiyo hapa kidogo naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi ili nipate kufahamu zaidi.

Mhe. Spika, nataka niende katika ukurasa wa 67 kwenye kiambatanisho namba 8(a) kuna ugawaji wa Zakka katika Wilaya. Hapa nimeona kuna Wilaya kuna vikundi kuna watu kuna na kima cha pesa. Sasa kidogo namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wanatumia kigezo gani katika kugawa hizi Zakka ili nipate kufahamu zaidi na kwa faida ya wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, pia naomba kwa kumalizia niendelee katika sehemu ya mwisho ya hili lilioko mbele yetu. Mbele yetu tumekabiliwa na masuala ya Katiba. Kila mtu anazungumza lakini kwa jambo lilivyo na umuhimu wake Mhe. Spika, lazima kila mmoja atilie mkazo.

Suala la Katiba liko mbele yetu sasa hivi tunatarajia mabaraza ya Katiba ya mawilaya kufanya shughuli muhimu ambayo kuwa ni nafasi yetu kubwa, na nathubutu kusema ni nafasi yetu ya mwisho tukiachia nafasi hii kupotea Wazanzibari kweli tutakuwa na mtihani mpaka Mwenyezi Mungu atatuhukumu mbele ya haki.

Sasa namuomba Mhe. Waziri katika hili aangalie sana na aandae utaratibu maalum wa kuwahamasisha watu wetu akawaelekeza na kuwafahamisha nini kinachotakiwa. Sisi Wawakilishi tuna majukumu yetu na Serikali pia ina majukumu yake katika hili. Pia tusije tukaona kwamba tunamlaani mwana siasa *CUF* au CCM, hili ni suala la Wazanzibari ni maslahi ya nchi yetu tutizame tulikotoka, tulipo na tunakokwenda.
Kwa kumalizia Mhe. Spika, nitaunga mkono hoja asilimia mia moja baada ya Mhe. Waziri kunithibitishia mambo mawili makubwa hasa katika Vyeti vya Kuzaliwa na katika Kesi za Udhalilishaji. Ahsante Mhe. Spika. Nakushukuru.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhanahu wataala* kwa kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Lakini pia nachukua nafasi hii kukushurukuru wewe kunipa nafasi ya kuweza kutoa na mimi mchango wangu japo mdogo sana katika hotuba hii ilioko mbele yetu.

Lakini pia nachukua nafasi kumpongeza Mhe. Waziri, kwa kuwasilisha hotuba yake ya Wizara yake ya Katiba na Sheria kwa ufasaha na kwa vizuri zaidi. Lakini pia nitakuwa mchache wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Wanu Hafidh Ameir aliyesoma hotuba hii kwa niaba ya Kamati yake kwa ufasaha vizuri sana.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nachukua nafasi hii kumuombea dua sheikh wetu Fadhil Soraga Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na apowe ili aendelee na majukumu yake ya kijamii, ya kifamilia na ya dini. Mhe. Fadhil Soraga ni mtu muhimu sana katika visiwa vyetu vya Zanzibar hasa katika kipindi hichi cha mwezi wa Ramadhani ambao uko mbele yetu hutoa taarifa ya miandamo ya miezi kutokana na utaalamu ule ambao Mwenyezi Mungu amempa, naomba Mwenyezi Mungu amjalie afya njema.

Mhe. Spika, naanza mchango wangu kwenye kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 3 Paragrafu ya 8 maneno ya mwisho hapa yanasema:

'Wizara pia ilikadiria kukusanya shilingi 447,000,000.00 ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi fedha zilizokusanywa ni milioni 288,708,060.00 sawa na asilimia 65.'
Mhe. Spika, hapa naomba nimuulize Mhe. Waziri nimuombe atutajie vianzio vyake vya mapato ni vipi? Na suali la pili kwa nini hawakufikia lengo lile ambalo walikusudia?

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende moja kwa moja katika Ofisi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ukurasa wa 42, 43.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni moja katika Kamisheni muhimu sana hapa kwetu Zanzibar, kwa nini nikasema hivyo. Kwa sababu kamisheni hii ina majukumu ya kuzisimamia mali zile za Wakfu pamoja na Amana walizowekewa na kuzitunza vizuri.

Lakini Mhe. Spika, hapa nataka niseme kwamba Mhe. Waziri alisema katika kutelekeza majukumu hayo Kamisheni iliweka lengo la kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na ugawaji wa Zakka katika mwaka 2012/2013. Katika

kufanikisha suala hili Elimu ya Zakka imetolewa kupitia semina nne kwa Mikoa ya Unguja, ziara za vikundi 118 na mengineyo.

Mhe. Spika, Zakka ni kitu muhimu sana kama lilivyo jina lake kwamba Zakka ni kutakasa mali na kuzifanya mali za mwenye kutoa Zakka ziwe safi na kuongezeka. Mhe. Spika, pia Zakka lengo lake ni kupunguza umasikini, kwa waislamu wale walionacho kuwapa wale ambao hawana kwa mafungu maalum yaliyotajwa na Mwenyezi Mungu *Subhana wataala* .
Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana mimi naiomba ifanye kazi ya ziada kuhamasisha matajiri wa nchi hii ili waweze kuzitoa mali zao za Zakka, kwa wale ambao hawana mali wafaidikie kupitia kwa matajiri wa Mwenyezi Mungu ili hao matajiri na wao iongezeke mali yao kwa ufanisi zaidi.

Nataka niendelee hapa katika kitabu Mhe. Waziri anasema hapa jumla ya shilingi milioni mia tatu na ishirini na moja nukta nane hapa za Zakka zimegaiwa na shilingi milioni mbili na laki moja zilikusanywa. Aidha misaada ya kheri yenye thamani ya shilingi 9, 30000 kutoka *Bait El Mali* na wachangiaji mbali mbali imetolewa alisema kwamba tuangalie kiambatanisho namba 8

Mhe. Spika, nikikiangalia kiambatanisho namba 8 katika mgao wa Zakka aliugusia Mhe. Farida lakini na mimi nataka niuendeleze hapa. Kinasema kwamba:
Ugawaji wa Zakka katika Wilaya, tunaangalia hapa Wilaya na Mjini kuna kima, vikundi, watu. Hapa naomba ufafunuzi wa kina kwa sababu mafungu ya Zakka yametajwa na Mwenyezi Mungu wala hawakutajwa na kanuni zetu tunazozitunga sisi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniwekee ufafanuzi juu ya mafungu haya ya ugawaji wa Zakka yalioko hapa yaliogaiwa kiwilaya.

Mhe. Spika, miongoni mwa wanaostahiki kupewa Zakka ni mafakiri, masikini, wasafiri waliharibikiwa na wenye madeni wanaoitumikia na wanaoingia sasa katika uislamu na katika mambo ya dini na fungu la nane na wanaojikomboa na utumwa.

Mhe. Spika, kwa sababu haya ni mafungu ya Zakka hayataki mjadala mafungu haya yametajwa na Mwenyezi Mungu ningemuomba Mhe. Waziri atueleze kiufafanuzi wa kina katika mgao wao huu waliougawa kupitia wilaya yamezingatia mafungu ya Mwenyezi Mungu. Naamini kwamba watu wa Kamisheni ya Wakfu na Malia ya Amana ni wataalamu wa dini sana. Sasa miongoni mwa wanaopewa fungu la Zakka ni mambo yale ya *Fisabilillah* yaani mambo ya dini.

Mhe. Spika, nataka hapa niseme kwamba tuna maeneo ambayo yanastahiki kugawa Zakka kwa kiasi kikubwa sana, kwa mfano miongoni mwa mambo ya dini ni ujenzi wa misikiti na madrasa pamoja na kuwasaidia hata walimu wa madrasa ambao wako katika hali ngumu. Je, ugawaji huu wa Zakka Kamisheni ya Wakfu inalizingatia hili.

Mhe. Spika, vijijini hasa katika Jimbo langu la Chambani kuna misikiti iko katika hali ya taabani sana. Kuna walimu wa vyuo wako taabani sana, naamini na majimbo mengine iko hali hiyo hiyo pamoja na ugawaji huu wa kiwilaya wamezingatia hizi hali na migao iligaiwa na Mwenyezi Mungu katika utoaji wa Zakka? Kama hivyo sivyo namuomba Mhe. Waziri kwa kushikirikiana na watu wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kulizingatia hili kwa kina.
Lakini pia katika misikiti mingi tunayosali hapa Unguja tunasikia baadhi ya Ijumaa kwamba leo kuna watu ambao wamesilimu hapa na tutawataja majina yao mbele ili muwaone. Watu hawa ni wale ambao zinazoweshwa nyoyo zao kuingia katika Uislamu. Je, katika mgao huu wa Zakka Kamisheni inawazingatia hawa na ni waislamu wangapi walioingia katika uislamu kipindi hiki waliotoka katika dini nyengine wakaingia katika uislamu kwa kipindi cha ugavi huu wa Zakka ya 2013/2013. Ni wangapi ambao wamefaidika na Zakka hii?

Lakini nikiondoka hapo niingie katika utunzaji wa mali za Wakfu ambazo zimewekwa kwa ajili ya kutunzwa. Tumeona hapa kama kuna mashamba, kuna majumba, kuna maelezo hapa yanaeleza kwamba kuna minazi kama 100 hivi imepandwa katika shamba fulani.

Mhe. Spika, naiomba Kamisheni ya Wakfu kwa makusudi kabisa kutokana na mkusanyo huu wa fedha ambazo zimeelezwa hapa waangalie kwa kina sana wameaminiwa najua ni waaminifu, waendelee na uaminifu wao ili shamba hizi wazitunze na majumba haya ambayo yako katika mamlaka yao wayatunze ili ziweze kudumu, wafaidike waliotoa wakfu lakini pia wafaidike na wao ambao wamewekewa dhamana hii. Kufaidika kwao wao ni kuwa waaminifu na waadilifu na kupata thawabu ndani yake. Katika fungu la Zakka na wao wamo wasije kujisahau kuwa wao wamo.

Kwa hivyo, pamoja na yote ambayo watakuwa wanayatenda hapa basi wahakikishie kwamba mali hizi wanazitunza ili wakafike mbele ya Mwenyezi Mungu wamepata thawabu za kutosha na kutunza mali hii kwa kutosha kabisa.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 44 sehemu ya 124. Mhe. Waziri alisema hapa:

Kamisheni ya Wakfu imeendelea kuimaarisha uhusiano na ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Kamisheni imeanzisha uhusiano wa wizara ya Wakfu ya Oman, Qatar, Taasisi ya Al-Rahma ya Falme za kiarabu (*UEA*) na Shirika la *Danmission* la Denmark.

Mhe. Spika, mimi naipongeza sana Kamisheni ya Wakfu kuwa na uhusianao na nchi hizi ambazo nina imani kubwa kwamba ni nchi za kitajiri kiasi Fulani, ni nchi ambazo zinaweza zikaleta uhusiano mkubwa wa kimapato katika kamisheni hii ya wakfu na Mali ya Amana. Nawaomba watu wa Kamisheni na Mali ya Amana waitumie vizuri nasafi hii ili wananchi wa Zanzibar kupitia uhusiano huu wafaidike katika masuala yao mbali mbali ya dini na wafaidike katika masuala mbali mbali ya kimaendeleo katika shughuli zao za dini.

Mhe. Spika, niendelee kidogo katika suala zima la vizazi na vifo. Mhe. Waziri kwa kweli Ofisi ya Mrajisi wa vizazi na vifo ina kazi kubwa. Ina kazi muhimu lakini nayo inakabiliwa na changamoto, miongoni mwa changamoto ambazo zinaikabili ofisi hii ni kucheleweshwa kwa vyeti vya kuzaliwa kwa hawa wazaliwa watoto wachanga, inasikitisha sana kwamba mtu anazaliwa mtoto mwezi huu wa saba mpaka inafika mwezi wa 12 hajapata cheti chake kulikoni.

Mhe. Waziri tunakuomba kwa heshima kubwa na taadhima kwa sababu ya umahiri wako, tunakuomba suala hili lirekebishike kwa sababu kunaweza kukarundikana vyeti vingi na watu wakashindwa kwenda kwa sababu ya umasikini. Kuna watu wa vijijini nauli ya kutoka kijijini mpaka kufika mjini kwenye Ofisi ya Wilaya kwa siku moja ni shilingi karibu 3000, 1500 kwenda na 1500 kurudi, tuwaonee huruma tarehe wanazopangiwa kwenda kuchukua vyeti vyao viwe tayari vipo.

Lakini Mhe. Spika, changamoto nyengine ambayo ipo katika ofisi hii kwa kweli katika takwimu iliyokuwepo hapa mwaka 2012/2013 imesajili jumla ya vizazi 31540. Lakini afisi pia imesajili vifo 1885 hili ni tatizo. Kwa sababu wananchi wetu wengi hawajashajihika hawajaujua umuhimu wa kusajili vifo pamoja na taarifa ambayo umewataka Wawakilishi waeneze taaluma hii katika majimbo yao, lakini pia afisi ya mrajisi inalazimika kutoa mafunzo maalum katika kila shehia au katika kila wilaya ili watu waujue umuhimu wa kusajili vizazi lakini pia kujua umuhimu wa kusajili vifo.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii nataka nimalizie kwenye mchakato wa Katiba tu. Nasema kuwa Wazanzibari umefika wakati wa kutoa maoni yetu ya katiba kwa ufanisi. Wataalamu wanasema kwa lugha ya kiarabu kupitia sauti ya ndege *al-watwan bil watwan walau fauqaljabal*, mtu kwao ni kwao japo juu ya jabali.

Kwa sababu Zanzibar ni petu tuna haki ya kutoa maoni yetu ya Katiba katika michakato ya wilaya na vyenginevyo ili kuhakikisha kwamba masuala haya hatufanyi makosa. Kuja kufanya makosa kwa kweli tutakuja lia, tutakuja juta na majuto mjukuu. Kwa hivyo imefika wakati kwa Wazanzibari kuwa kitu kimoja kuhakikisha kwamba fursa hii tunaitumia kwa vizuri tusije kuipoteza. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mohd Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kusema machache katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru muumba wetu kwa kutuwezesha jioni hii kuweko hapa tukiwa wazima na kuendelea na shughuli zetu za kazi kama kawaida.
Mhe. Spika, pia nikushukuru wewe kwa umahiri wako kwa kutuongoza katika Baraza hili. Pia nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutumia lugha nzuri na fasaha katika kitabu chake ambacho tunacho mbele hapa kwa majadilinao.

Mhe. Spika, mimi nianze na Mahakama hapa kunaonesha kuna mrundikano wa madai au kesi. Kuna kesi nyingi kuanzia Mahakama Kuu, mahakama ya kazi na mahakama nyengine zote. Sasa kesi nyingi zimerundikana ni chache mno ambazo zimepatiwa ufumbuzi sijui tatizo ni nini. Mahakimu na Majaji hawatoshi au ushahidi haupo au tatizo nini? Kwa sababu Mhe. Spika kila kipengele cha mahakama kesi zilizopatiwa ufumbuzi ni chache mno. Kwa hivyo kila siku kuna mrundikano wa kesi.

Mhe. Spika, mwaka huu unaomalizika kama alivyozungumza aliyepita tumesajili watoto waliozaliwa 31540, wakiwemo wanaume 15930 na wanawake 15610. Katika kipindi hichi wanaume wamezaliwa zaidi kuliko wanawake labda wanataka kuvunja rekodi baada ya kuwa wao ni wengi sasa tunataka kuwa wengi sisi.

Lakini pamoja na idadi hii bado Mhe. Spika, hii ni idadi ndogo sana tukilinganisha na jinsi Wazanzibari tunavyozaana. Hii ina maana kuna watu kadhaa ambao hawasajili watoto wao baada ya kuzaa, hususan sisi watu wa vijijini, wengi wetu bado hatujaona umuhimu wa suala hili na mbele ya safari hufika pahala tukawaachia kazi hawa watoto tunaowazaa. Mfano katika mambo ya elimu na vyenginevyo wanatakiwa na cheti cha kuzaliwa hawana inabidi sasa watafute cheti cha kuchelewa kuandikishwa ambacho cheti hichi Mhe. Spika, kukipata urasimu ni mkubwa mno. Kwa sisi Pemba utoke Kengeja uende Wete ukatafute hiyo fomu uje umtafute Sheha wako umbembeleze, kama akikubakali atakupa siku katika kamati yake, na kamati

inaweza ikakukubalia inaweza ikakataa, ikikubali uende kwa Mkuu wa Wilaya uende Mahakamani na hatimaye na ukifika huko kama utakubaliwa hayo malipo yake si ya kitoto!

Kwa hivyo, kwanza ningeomba huu urasimu wa cheti upunguzwe na ikiwezekana uondoke iwe ni jambo la kawaida kama ilivyo hivi kwa watoto wadogo.
Mhe. Spika, pamoja na umuhimu huu wa cheti za kuzaliwa bado baadhi ya watu hawajaona umuhimu wake, kwa hivyo wizara hii au Taasisi hii ina haja ya kutuelemisha ili tujue umuhimu huo.

Jengine hili la vifo Mhe. Spika, ndio kabisa wengi wetu tunaona kafa tena ya nini kumchukulia cheti cha kifo. Hatuoni umuhimu wake lakini jambo hili au cheti hichi cha kifo kina umuhimu mkubwa mno, kinyume tunavyoona kuwa hakuna haja yoyote aliyekufa ndio keshakufa. Lakini anapofariki mtu na akaandikishwa siku hizi kuna taasisi na mashirika mbali mbali ambayo yanasaidia mayatima, kigezo kimoja baada ya kuwa ni kweli kuwa huyu ni yatima ni kuwepo kesi ya kifo cha baba yake. Sasa kama hakipo cheti hicho msaada ambao mtoto huyu yatima ulikuwa umfikie ataukosa kwa sababu ya kukosa tu hichi cheti.

Lakini hawa mawakala hasa Masheha wana matatizo kila kitu kwao ama hawakujui au hawakutambui au njoo kesho, keshokutwa Mhe. Spika, hata hivi vyeti vya kuzaliwa kwa yule mtoto ambaye hajazaliwa Hospitali lazima akapate kipande kile kwa Sheha wake. Baadhi ya Masheha wanakuwa ni wakaidi na wagumu wa kutoa vikaratasi hivi sijui kwa nini tatizo ni nini? Kumkosesha mtu haki yake ya kisheria ya kikatiba. Kwa hivyo Mhe. Spika, ningemuomba Mhe.Waziri angalau aitake taasisi yake hii iwaelimishe na iwaelekeze masheha juu ya umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa na umuhimu wa kuandika vyeti vya vifo pale ambapo jamaa zetu wanakufa.

Mhe. Spika, niende kama msumeno mbele na nyuma. Nirudi tena katika mahakama. Mahakama ni muhimili mmoja katika mihimili mitatu ya dola, kwenye mahakama kuna mtu anaitwa Jaji Mkuu, ambapo hiki ni cheo, cheo hiki kwa mawazo yangu kama ni sahihi kwa sababu sio mwanasheria, nadhani ndiye kiongozi kwa muhimili huu mmoja. Mtu mwenye cheo hiki mimi namjua na naijua nyumba yake anayoishi, sina hakika kama ni yake au ya serikali au kakodiwa.

Lakini Mhe. Spika, kidhahiri pale nje kwenye nyumba yake iko wazi kama nyumba anayokaa Mohamed Haji na haioneshi kama ni nyumba anayokaa mtu mkubwa, hiki ni cheo kikubwa sana, sioni kidhahiri kama pana ulinzi pale. Kwa mawazo yangu cheo hiki kiwe na ulinzi wa masaa 24 pale

nyumbani kwake na katika safari zake, kama wapo sina hakika. Lakini pale nje kwa sababu huwa napita mara kwa mara, sijaona kama kuna dalili ya kuwa mtu mwenye cheo hiki kuna ulinzi katika nyumba yake. Ni cheo ambacho kinachukua dhamana kubwa, ni cheo ambacho kina maamuzi ya watu ambao wana uhalifu wa mambo mbali mbali. Sasa kumuacha wazi kama alivyo, kwa mawazo yangu ni tatizo.

Mhe. Spika, ningeshauri mimi kuwa mtu mwenye dhamana hiyo ya Jaji Mkuu, ajengewe nyumba rasmi na serikali wala asikae uraiani pamoja na Mohamed Haji na awe na ulinzi nyumbani kwake na katika safari zake. Vile vile hata Spika, kwa sababu yeye ndiye aliyejitwika hili Baraza juu ya kichwa chake. Kwa kweli hawa wana kazi kubwa naona wameachwa tu wanakwenda kama raia wa kawaida, watu wenye vyeo hivi sio wa kawaida ni viongozi wakubwa mno katika nchi hii, wasipewe ving'ora vitakuwa vingi! Watatu wenye ving'ora wanatosha, lakini huduma nyengine za ulinzi majumbani mwao wanamoishi wapatiwe.

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme sana, lakini waliotangulia wote ni kama washairi wana kibwagizo chao, wengi wamebwagiza juu ya rasimu hii ya katiba, rasimu ambayo hatimaye itakuwa ndio katiba ya nchi na ndio itakayoleta hatima ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Zanzibar kabla ya tarehe 26/01/1964 ilikuwa ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na ilikuwa ina mamlaka kamili ya mambo yake yote. Zanzibar kabla ya Mapinduzi ilikuwa ni moja katika nchi nne za Afrika ya Mashariki na zilitajwa kwa ukubwa wake; Tanganyika, Kenya, Uganda na Zanzibar. Kwa wakati huo nchi hizi nne kwa kuwa mfumo wake wa kiutawala ulikuwa chini ya Waingereza, kwa kuwa walikuwa wakitumia sarafu moja.

Sasa tukaendelea baada ya uhuru kila nchi ikaanzisha sarafu yake, Kenya wakawa na sarafu yao, sisi kwa jina la Tanzania tukawa na sarafu yetu na Uganda wakawa na sarafu yao. Huko mwanzo tulikuwa tunatumia sarafu moja nchi zote hizi, lakini baada ya uhuru kidogo kila nchi ikaanzisha sarafu yake. Kwa hivyo, na Zanzibar katika hivi tunavyokwenda na kwa kuwa nayo ni nchi, ni vyema hatimaye ikawa na sarafu yake.

Mhe. Spika, wengi sarafu ya Afrika ya Mashariki hawaijui, hawakuiona. Iko pesa ina kitomo hii (Mjumbe aliionesha hiyo pesa), hii ni senti tano. Wakati mimi nasoma skuli nilikuwa napata badia tatu, senti tano hii. Hii nyengine ina kitomo katikati

Mhe. Spika: Ndio ile nyenye tundu hiyo. Mheshimiwa ndio ile yenye tundu! *(Makofi).*

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ndio, ina tundu katikati. Hii ilikuwa ndio sarafu ya Afrika ya Mashariki na shilingi ilikuwa na picha ya King George wa Sita. Sarafu yetu wenyewe, tulikuwa tuna sarafu ya shilingi ishirini kubwa na nyenginezo, senti tano, senti moja na senti tatu.

Sasa Mhe. Spika, kwa kuwa nchi zote tatu kila moja imeanzisha sarafu yake, sishawishi katika rasimu hii na sisi Wazanzibari tutafika pahala tukaiingiza benki yetu na sarafu yetu kama nchi nyengine za Afrika Mashariki ambazo wana sarafu yao, haidhuru isiwe na kitomo katikati lakini tuwe na sarafu yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Anayetaka kujua historia ya sarafu basi aende kwa Mhe. Mohamed Haji Khalid. Ni zamu yake sasa Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadae Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mchango wangu mfupi katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Abubakar Khamis Bakary.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutekeleza majukumu yake ya kisheria na ya kikatiba. Pili niwapongeze wafanyakazi wa ofisi hii. Mhe. Spika, wizara hii ni nzito kwa sababu imebeba mambo mazito, imebeba muhimili mzima wa mahakama, imebeba ofisi zile kubwa nzito za dini na mambo mengine mazito. Kwa hivyo, tunatakiwa tuwe na hadhari kubwa sana wakati tunapochangia wizara hii juu ya uzito wake na umuhimu wa ofisi ziliopo.

Mhe. Spika, mchango wangu nitauelekeza katika maeneo makubwa matano. Eneo la Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Lakini baadae kwa ufupi nitazungumzia suala la rasimu ya katiba kama livyodokeza hapa Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa mwisho huko, na kutoa maelekezo kwa baadhi ya mambo.

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nikichangia mchango wangu nilizungumzia juu ya Baraza hili watu kulinasibisha na mahakama. Nikasema kwamba watu au wananchi wanapofika pahala wakakosa imani na baadhi ya vyombo vyao, basi kimbilio lao sasa limekuwa ni chombo hiki chao Baraza la Wawakilishi. Kama watakosa imani na mahakama na watakosa imani na baadhi ya vyombo vya serikali, basi chombo chao cha kukimbilia sasa imekuwa hapa. Kwa hivyo chombo hiki kisionekane kwamba ni mahakama, lakini kionekane kwamba ni chombo ambacho wananchi bado wanaendelea kuwa na imani

nacho. Niwasihi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tuendelee kuwasikiliza wananchi wetu na tuwazungumzie mambo yao, ili waendelee kuwa na imani na chombo hiki. Lakini watakapofika pahala wakikosa imani na hapa, basi watabakia *dilemma* hawajui watakakokwenda na hilo sio jambo zuri.

Mhe. Spika, nilisema nianze na utangulizi huu na hoja ambayo ipo na jambo ambalo nataka kulizungumzia. Mhe. Spika, ninayo malalamiko juu ya mwananchi mmoja kuhusu nyumba yake ambayo imeuzwa na Idara ya Mahakama. Mwananchi huyu mkaazi wa jimbo langu, nyumba yake imeuzwa na mahakama akiwa yuko nje ya Zanzibar kwa shughuli za kikazi, baada ya kupelekewa madai kulalamikiwa kuwa anadaiwa kiasi cha shilingi milioni moja na nusu 1.5. Bila ya kufuata taratibu za kisheria za kimahakama, mahakama iliamua kuiuza nyumba ile *min-ghairi* ya yeye mwenyewe kuwepo, *min-ghairi* ya utaratibu wa kutangazwa na *min-ghairi* ya utaratibu wote ule unaohusu uuzaji wa mali kama hizi. Jambo ambalo linasikitishwa kufanywa na chombo cha mahakama.

Lakini Mhe. Spika, cha kusikitisha zaidi nyumba ile wameuziana wenyewe kwa wenyewe wanasheria. Mhe. Spika, tunapofika hatua kama hiyo ni hatua ya kusikitisha. Lakini baada ya kupata taarifa mwenyewe, basi alikuja Zanzibar na kufuatilia na kupata taarifa juu ya kuuzwa kwa nyumba hiyo. Alichofanya yeye ni kuandika barua ya kutaka kuzuia ile amri iliyotolewa na mahakama, ili apate nafasi angalau ya kurejesha zile fedha zilizopo na arudishiwe nyumba yake. Mhe. Spika, mwananchi yule baada ya nenda rudi hakupata majibu.

Kibaya zaidi Mhe. Spika, nyumba ile fedha alizokuwa akidaiwa ni shilingi milioni 1,500,000, lakini imeuzwa shilingi milioni 8,500,000. Baada ya kuona hapati ufumbuzi wa jambo lile aliamua sasa kudai kile kilichobakia, basi nipeni kilichobakia ili sasa na mimi niendelee na maisha yangu, haidhuru nyumba anasema aliijenga kwa gharama za shilingi milioni 10,000,000, lakini imeuzwa kwa shilingi milioni 8,500,000 na wameuziana wenyewe watu wa sheria, majina yao ninayo na barua zao ninazo, lakini sitaki kuwataja hapa.

Mhe. Spika, baada ya kuendelea kudai fedha zile na baada ya kufuata katika hatua mbali mbali. Wengine wanamuambia umezichukua fedha hizo, lakini stakabadhi ya kuonesha kuwa fedha zile amezipokea hakuna, hakuna vielelezo vyovyote hadi leo haki yake ile hajaipata na ni muda mrefu.

Sasa Mhe. Spika, tunapofika pahala chombo kama mahakama ambacho kinategemewa kutoa haki kwa wananchi, kinafanya mambo kama haya, hivi wananchi wetu wakimbilie wapi? Hili ni jambo la kusikitisha sana. Mhe.

Waziri nakumbuka niliwahi kukudokeza kwamba nitakuja na hoja hii, naamini pengine uliifuatilia kwa sababu nilikuambia mapema nje ya ukumbi huu. Sasa nataka uje unipe maelezo ya kutosha juu ya mwananchi huyu na hatua zilizofikia na kwa nini fedha zake zilizobakia, yeye hataki ile nyumba, anataka fedha zake zilizobakia apewe mwenyewe baada ya kuuzwa, na kwa nini fedha zile zilizobakia mahakama hawataki kumpa ambao ndio walioiuza nyumba yake kinyume na taratibu. Mhe. Waziri unipe maelezo ya kutosha ili nikupitishie bajeti yako ukafanye shughuli zako, hilo moja.

Mhe. Spika, katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Spika, ofisi hii ni muhimu na ni ofisi ambayo inatayarisha mashtaka katika kesi mbali mbali. Lakini ofisi hii Mhe. Spika, imekuwa na malalamiko mengi juu ya maslahi ya wafanyakazi wa eneo hili.

Mhe. Spika, wenzangu wengine wamejaribu kulizungumzia, lakini na mimi ninakazia japo Mhe. Naibu Spika, alisema tusikazie, lakini wakati mwengine inafika pahala tukazie ili uonekane umuhimu wa kitu hiki. Namuomba Mhe. Waziri pamoja na wanasheria waliopo, lakini wanasheria waliopo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wana haki ya kuangaliwa maslahi yao kwa uzito unaostahili, kama tulivyoangalia maslahi yao mahakimu na Majaji. Kwa sababu wakati tukiangalia maslahi ya mahakimu na majaji na sisi tulichangia katika kuona wanapewa maslahi yaliyo bora na kuondokana na vishawishi, kwa sababu wako katika *angle* ya vishawishi, wanaweza wakashawishika. Kwa hivyo, tuliwatayarishia maslahi mazuri ili mahakimu hawa wasishawishike kwa wepesi katika upokeaji wa rushwa na mambo mengine. Tunashukuru *Alhamdulillah* maslahi yao sasa sio mabaya.

Mhe. Spika, na hii ofisi ambayo inatayarisha hayo mashtaka, hii nayo ilikuwa inahitaji kuangaliwa zaidi, kwa sababu mahakimu hawawezi kupata kesi za kuendesha bila kesi zile kutayarishwa hapa, mapishi yanapikwa hapa. Kwa hivyo, kama ushawishi wa rushwa na mambo mengine yanatakiwa yaanzie hapa, kwa sababu wao wana uwezo wa kusema hii si kesi, mashtaka haya yako hivi, wanaweza wakababaisha mashtaka badala ya kufungua kesi hii ikawa hii na kesi ile ikawa ni batili, wana uwezo mkubwa wa kubabaisha haki za watu na wanaweza wakapokea rushwa kwa utaratibu mwengine wowote ule. Kwa hivyo, ofisi hii inahitaji kuangaliwa na si kwa utaratibu huu uliopo sasa. Waangaliwe ili waweze kufanya kazi zao vizuri na vile vishawishi ambavyo vinaweza vikawashawishi basi waondokane navyo.

Mhe. Spika, eneo la tatu ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Spika, kamisheni hii inafanya kazi vizuri, lakini nako kumekuwa na matatizo. Kamisheni hii ina majukumu mengi, lakini moja kati ya majukumu yake ni

kusimamia mahujaji. Katika ukurasa wa 44 wa hotuba yako Mhe. Waziri naomba ninukuu unasema hivi;

Ukurasa wa 44 wa hotuba

"Katika mwaka 2012/2013 Kamisheni imesimamia vyema shughuli za Hijja na kuimarisha huduma za Mahujaji, ambapo jumla ya Mahujaji 2,146 waliitekeleza ibada hiyo. Mahujaji 1,255 kati ya hao walisafiri kupitia vikundi vya Zanzibar na vikao tisa vilifanyika ndani na nje ya nchi kuratibu shughuli za Hijja".

Vile vile kamisheni imeendelea kusimamia kwa ufanisi shughuli za sala na mabaraza ya Eid kitaifa. Ukatuambia tuangalie kiambatanisho nambari 8 ambacho kina vikundi hapa vinavyosafirisha mahujaji, kuna vikundi kama 11 nimevitaja kina Ahl Daawa, Jumuiya ya Maimamu ni vingi tu. Hivi ni vikundi ambavyo vinashughulikia kuwasafirisha mahujaji.

Mhe. Waziri, kweli mnaratibu na mnasimamia na ndio wenye dhima. Lakini inakuwaje mahujaji wengine waweze kutapeliwa pesa zao, wanaambiwa toweni pesa nusu na nusu mtatolewa, zikachukuliwa pesa zao na baadae wakati wa usafiri mahujaji wale wakakosa safari na kwenye orodha wakawa hawamo, inakuwaje. Wengine wamepata maradhi, kwa sababu wamejiandaa kwa ajili ya safari ya Hijja, matokeo yake wameshaaga na wameshafunga safari, lakini baadae mahujaji wale wanapotaka kusafiri wanaambiwa kwamba kwenye orodha ya mahujaji wanaosafiri hawamo, ilihali nusu ya fedha za safari yao wameshatoa na waliahidiwa hawa kwamba watapewa nusu nyengine ya fedha ili waweze kusafirishwa.

Sasa nataka kukuambia Mhe. Waziri nataka maelezo juu ya jambo hili. Je ni Jumuiya ipi katika hizi ambayo imeruhusiwa kusafirisha mahujaji kwanza iliyohusika na kadhia hii na kwa nini mahujaji hawa wakatapeliwa, ilihali taasisi yako inayosimamia ulituambia imeratibu vizuri. Lakini kama linatokea tatizo kama hili wananchi hawa waende wapi kudai haki zao. Hili sio jambo la kawaida Mhe. Spika, ikiwa leo tunafikia pahala watu wanataka kwenda kwenye ibada kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu wanatapeliwa na chombo hiki kipo ambacho kinaratibu. Tunataka maelezo Mhe. Waziri ya kina, juu ya taasisi iliyohusika na jambo hili na taasii hii hatua iliyochukua na kama unalielewa hili basi utatuambia, na kama hulielewi utatuambia, hatua zilizochukuliwa na taasisi hizi ambazo mmezisajili na kama ni mtu mwengine nje ya taasisi hizi basi tuambiwe na hatua ambazo mmezichukua. Hili ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Spika ndio maana wananchi sasa wamekuwa chombo hiki ndio kimbilio lao. Kama nilivyotangulia kusema, kwa sababu wanaona kila wanapokwenda kwenye taasisi hizi za umma hawapati majibu

yaliyo sahihi. Watu wanadhulumiwa haki zao, hawashughulikiwi na vyombo hivi vya kushughulikia wananchi vipo.

Mhe. Spika, sisi sote tunawajibika kwa wananchi Rais, mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, sote tunawajibika kwa wananchi tunawatumikia wananchi. Kwa hivyo, tunatakiwa tuwatumikie na sio kuwatumikia kwa kuwababaisha, tuwatumikie kwa imani ili waone kwamba haki zao hazipotei, mambo yao yanakwenda na wanaishi katika maisha yaliyokuwa bora. Sasa inapotokea kwamba kuna mambo kama haya ambayo huko nyuma hayakuwahi kutokea.

Mimi sikumbuki kama kuna utapeli wa kiasi hiki kwamba watu wanatoa pesa zao za Hijja halafu wanakosa safari, mambo haya zamani wakati ule dola ilikuwa mali, hata ukitaka kusafiri basi unaweza kuambiwa usiende Hijja kwa sababu pesa zile za dola hazipo, watu walikuwa wanachukua pesa viwango vilikuwa havitimii, lakini sio wakati huu wa leo, wakati huu sio wa kutokea matokeo kama hayo, katika nchi iliyokuwa ya kidemokrasia na utawala bora haiwezekani hata siku moja.

Kwa hivyo, suala hili Mhe. Waziri uje utuambie, taasisi inayohusika na kama sio taasisi kama ni mtu, lakini dhamana ya ofisi hii au huyo mtu umechukua hatua gani juu ya mtu yule na kuona kwamba haki yao inapatikana, pamoja na kwamba usumbufu umetokea walitaka kwenda Hijja, kwa bahati siku yao pengine haijatimia au haijafika. Kwa sababu mambo haya mpaka Mwenyezi Mungu atake. Lakini hizi haki zao ambazo zimepotea na matarajio ya wananchi katika siku za baadae katika masuala haya ya Hijja.

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Namalizia Mhe. Spika, dakika tano na Ofisi ya Mrajisi, Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo inashughulikia mambo ya vyeti vya kuzaliwa. Sasa hivi kumekuwa na vyeti vya kuzaliwa *fake*, vyeti hivi hatuvifahamu vinatokea wapi, vyeti vya kuzaliwa *fake*. Vyeti vya kuzaliwa vilivyotolewa sasa hivi utakuta vingine vina saini ya Topiwala ambaye keshafariki lakini vinatolewa leo. Hii ni aibu kwamba watu wanabuni kitu kama hicho, wanatengeneza vyeti *fake* vya kuzaliwa vinawekwa mihuri ya serikali, vinawekwa saini za watu ambao wamefariki tunakwenda wapi. Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, kuna baadhi ya watu wamekamatwa na wakapelekwa kituo cha polisi juu ya vyeti vile, lakini kuna wakubwa wameamrisha wale watu watolewe.

Sasa nataka nimuambie Mhe. Waziri sijui unalielewa hili kama kuna watu walikamatwa na vyeti vya *fake* na kuna watu wakaamrisha watolewe ndani

polisi je unalijua hili? Wakati utakapofanya majumuisho uje utuambie juu ya jambo hili, utupe ufafanuzi juu ya vyeti *fake* ambavyo vimezagaa mitaani vyenye saini ya watu wa zamani ambao sasa hivi wameshafariki! Hii ni hatari Mhe. Spika, hata takwimu zetu zitapotea. Kwa hivyo, suala hili kama unalifahamu nakuomba uje utuambie kama kweli watu wamekamatwa na walipelekwa kituo gani? Sisi tuna ushahidi kwamba watu hawa walipelekwa katika kituo vya Mazizini, lakini ikatoka amri watu hao waachiwe na wakaachiwa. Sasa hebu utakapokuja kufanya majumuisho utueleze kama hili unalifahamu na waliohusika ni nani na wizara yako inachukua utaratibu gani juu ya mambo ya aina hii.

Mhe. Spika, nimalizie dakika mbili za mwisho juu ya suala langu la mwisho. Mhe. Waziri kwenye kitabu chake ameeleza mambo mazuri juu ya Rasimu ya Katiba, namalizia mwisho. Kwa kweli ameeleza mambo mazuri na ametoa nasaha nzuri juu ya wananchi, isipokuwa naona moja amelisahau.

Kwa mfano, amezungumzia masuala ya uchumi, demokrasia pamoja na mambo mengine, lakini kuna jambo moja ambalo amelisahau ni juu ya namna ya kuimarisha Muungano. Mhe. Spika, Katiba hii tunayokwenda nayo, lazima wananchi tuhakikishe kwamba inaimarisha muungano na tusije tukafika pahala tukawa na Katiba ambayo itavunja muungano. Rasimu ya Katiba tuliyonayo ina-*create* kuwa na marais watatu. *(Makofi)*

Sasa katika hali ya marais watatu sisi wananchi tunatakiwa tupime na tuone ni kweli tunaimarisha muungano au vipi, kwa sababu nchi yenye rais watatu labda ni nchi ya kusadikika na mimi sijaiona kwamba nchi moja inakuwa na marais watatu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sitaki kusema zaidi, kwa sababu wananchi ndio waamuzi. Lakini Rasimu ya Katiba yetu wananchi waelewe kwamba twende tufike pahala tuwe tunaimarisha muungano, yaani muungano wetu uweze kuimarika na wala hatuwezi kuwa na Katiba ambayo inavunja Muungano. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni naunga mkono hotuba hii na nina matumaini katika maeneo ambayo Mhe. Waziri nimeyaeleza basi atanipa ufafanuzi, ili niridhike na niweze kuidhinisha fedha kwa ajili ya wizara yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Ashura Sharif Ali na baadaye Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, ahsante awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *Subhanahu Wataalla* aliyetujaalia uhai, uzima na tukawepo hapa katika Baraza lako tukufu kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, sina budi pia Mhe. Spika nikushukuru na wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika mada iliopo mezani wakati huu.

Mhe. Spika, nianze na kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake pamoja na watendaji wake.

Sasa niende katika kitabu cha hotuba kwenye ukurasa wa 14 kifungu cha 38 kuhusiana na mahakama. Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba wanyonge wengi hukimbilia mahakamani kwenda kudai haki zao, na wakati huu pamoja uangaliaji wangu wa kitabu hichi kwenye viambatanisho mbali mbali vilivyoonesha kesi za mahakama vimeonesha wazi wazi kwamba kesi hizo mara nyingi huwa zinachelewa mno na kukosa maamuzi.

Kwa hivyo, hili ni tatizo na linahitaji kutatuliwa, kwa sababu wananchi wanategemea sana mahakama hizo kudai haki zao. Kwa kweli mahakama zetu kwa wakati huu zimezungukwa sana na mazingira ya rushwa, jambo ambalo tunajua kwamba rushwa ni adui wa haki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atuelimishe kwamba labda kuna uchache wa mahakimu au tatizo nini, kwa sababu kwa hali hii inaonesha kwamba kila siku zinaripotiwa kesi mpya, lakini hukumu zake zinakuwa hazipatikani.

Sasa kukosekana huku kwa haki mahakamani kunawakatisha tamaa wananchi, kwa kweli tunaondokana na ile dhana nzima kabisa ya utawala bora. Kwa hiyo, ni vizuri mahakama hizo zikafanya iwezekanavyo na wananchi wakapata haki zao za msingi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika ukurasa wa 18 kifungu cha 52. Mhe. Spika, hapa sikuwa na lolote, isipokuwa ninaipongeza ofisi hii pamoja na kuiombea kila la kheri na iendelee na majukumu yake ya kutoa ushauri wa kisheria kwa ajili ya kuisaidia serikali pamoja na taasisi zake, ili tusijetukafikia yale mambo ambayo tulikuwa nayo nyuma ya kusaini mikataba ambayo ilileta mizozo na matatizo.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 30 kifungu cha 83 Tume ya Kurekebeisha Sheria. Kwa kweli kama kuna sheria zimebana zina matatizo, basi sasa umefika wakati kwamba sheria hizo lazima zifanyiwe marekebisho na kwa nini niliseme hili? Nalisema hili kwa kuona kwamba hali imekuwa ngumu sana katika upande wa udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Kwa kweli kesi hizo ni nyingi mno na nimezoea au tumezoea kuripotiwa kesi hizo kupitia wizara tofauti ikiwemo ya Wizara ya Ustawi wa jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, lakini Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nako nimekuta zimeripotiwa,na wala kesi hizo hazikupatiwa ufumbuzi, hali ambayo inajenga unyonge kabisa na wala haijengi matumaini.

Mhe. Spika, hali tuliyonayo kwa wakati huu ni ngumu, ya kutisha tena ni aibu kubwa sana kwa Zanzibar yetu ambayo kihistoria mila na utamaduni wake haiendani na mambo yaliopo katika nchi yetu, yaani ubakaji. Hali hii ni ngumu inatisha na inatia aibu. Vile vile, tukizingatia kwamba asilimia 95 ni waislamu na sisi tumekatazwa acha kufanya kukaribia tu hilo tendo baya acha kwa wakubwa na leo wamekuja watoto ndio wanaodhalilika.

Hali hii ni mbaya sana, kwani kuna kesi nyingi ambazo zimelimbikana na hata Wizara yenyewe ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ni kilio chake. Kwa mfano, iliona kwamba ikifungua Kituo cha Mkono kwa Mkono (*One Stop Center*) inawezekana kesi hizi zinaweza kupatiwa ufumbuzi, lakini wapi hazikupatiwa.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tunamuangalia kwa jicho kubwa na wananchi wanajenga matumaini na awaambie sasa, wapi waelekeze matatizo haya yanapojitokeza na kuripotiwa na mahakamani yanakosa ufumbuzi na ushahidi unakosekana inavyosemekana, lakini hata kama mtu ameonekana, basi mara nyingi inakuja kwamba ushahidi haukukamilika, hivi wazanzibari waelekee wapi katika hili? Kwa hivyo, kama sheria tulitengeneza sheria hapa, je ni kufuata sheria au sheria zetu bado zimebana katika hali hii.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze ana utaratibu gani juu ya kesi hizi za udhalilishaji wa watoto na wanawake, na nini anakusudia hapa na sheria gani anakusudia kuzirekebisha, ili tuweze kuona wapi tunafikia.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 38 kifungu cha 100 kuhusu Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, ni mara nyingi sana imekuwa ni tatizo upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Sheria hii tumeiweka sisi kwamba kila

mtoto atakayezaliwa apatiwe cheti cha kuzaliwa na apewe cheti chake, kwa hiyo nini hasa kinachokwaza mpaka inafikia muda mrefu mtoto bila ya kupata cheti chake?

Mhe. Spika, ninadhani umefika wakati sasa tuone na twende na sisi kama wenzetu wanavyokwenda huko duniani, kwa sababu tunaweza kujipangia mipango yetu mizuri ya kimaendeleo kwa ajili ya utoaji wa huduma pale ambapo tutakuwa na *database* ya kuonesha hasa mwaka huu wamezaliwa watoto wangapi na watoto hao wamechukua vyeti na hata utakapotaka kuwapatia.

Kwa mfano, huduma ya elimu basi unajua mwaka huu tunao watoto kadhaa kwa ajili ya kuwapatia elimu ambao wamefikia umri fulani. Kwa hivyo, hali kama hiyo haileti usumbufu na tunajua mpango wetu mzima kwa kupitia vyeti vya kuzaliwa, kwa sababu na huu ni usajili.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri suala hili alifikirie kwa kina na wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi aje atueleze ni sababu zipi zinazokwamisha kufikia muda mrefu vijana wetu hawajapatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Ukurasa wa 42 kifungu cha 117 kuhusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Spika, hapa Waziri amezungumza na mimi naomba ninukuu kidogo.

Ukurasa wa 42 kifungu cha 117 kinaeleza hivi:-

> “Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina jukumu la kusimamia masuala yote yanayohusiana na mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Eid ya Kitaifa, Hijja Zakka na Misaada ya Kheri”.

Sasa hapa mimi ninachotaka kukifahamu namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi anieleze kuhusu hii misaada ya kheri ndio ipi na wanaohusika kupata misaada hiyo akina nani na inagaiwa kwa utaratibu upi? Na hapa ningependa kujua hilo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kifungu cha 83 kuhusu Ofisi ya Mufti Zanzibar. Kwanza hapa niseme kwamba nampa pole sana na Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri na ampe afya yake, kwani kilichotendeka sio kizuri.

Lakini baada ya kuyasema hayo, niseme kwamba ofisi hii ndiyo yenye kutoa miongozo kuhusu masuala yote ya kidini Zanzibar. Mhe. Spika, kwa kweli kwa hali hii ningeomba nipate maelezo kidogo katika mambo yetu ya dini ukizingatia kwamba sisi wananchi wa Zanzibar wengi wao ni waislamu, na mambo hayo yametengewa sehemu hii ya Ofisi ya Mufti Zanzibar. Kwa hivyo, ningependa kuelewa huu utaratibu mzima wa kuporomoka kwa maadili hapa nchini, nini hasa kimesababisha na ofisi hii ipo na ukizingatia hali halisi.

Vile vile kumekithiri sana udhalilishaji wa watoto, jambo ambalo tunakwenda kinyume na utaratibu na kitabu cha Mwenyezi Mungu au katika dini ya kiislamu na udhalilishaji huu wa watoto, jambo ambalo linatisha sana kwa sasa na mwenzangu Mhe. Abdalla Juma Abdalla alipokuwa akizungumza alilisema hilo, tena jambo hili si mchezo lipo na linatendeka na linaendelea, na huko kisiwani Pemba limekithiri hilo na tunazo taarifa hizo.

Mhe. Spika, tukijiuliza sisi kama waislamu hivi tutafikia vipi hatua hizi na hawa vijana itakuwa vipi hatima yake, kwamba hali ikiwa hivi. Kwa hivyo, ni utaratibu gani ofisi hii itautumia ili kuona kwamba tunaondokana na balaa hili.

Pia niseme tena kwamba tunapoteza vijana wetu kwa kutumbukia katika madawa ya kulevya, ambao hao ndio tunaowatarajia wawe Masheikh na Maimamu wa misikiti. Sasa hali hii iko vipi na ofisi hii inaangalia vipi jambo hili, kwa sababu hao ndio tunaowatarajia waje kuwa mamufti wa kuiongoza Zanzibar hii katika waislamu na hili liko vipi nalo?

Katika ofisi hii niulize swali jengine tena kwa ofisi hii kuhusu suala la mavazi hapa kwetu Zanzibar, ambapo mila na utamaduni wetu ilikuwa kuna mavazi maalum ambayo yalijengeka kuonekana hayo hasa kwamba ni utamaduni wa kizanzibari na kusomeka na wengi wageni wapokuja hapa hutupa majina ya kuionesha ile taswira yetu hapa. Sasa haya maporomoko ya mavazi yaliyokithiri tumefikia hatua gani hasa? Kwa nini Ofisi yetu hii ipo tena serikalini, lakini nini hasa kinachangia hadi tumefikia hatua hiyo?

Mhe. Spika, kwa kuwa sikuwa na mchango mkubwa, lakini mwisho kabisa kwa kuwa Mhe. Waziri amegusia hii Rasimu ya Katiba haitakuwa vyema na mimi nichangie, lakini nisiliguse hili jambo kubwa ambalo liko mbele yetu sote wazanzibari sote kwa pamoja.

Mhe. Spika, kama ni zama za kupata bahati basi hii ni bahati ya aina yake. Kwa kweli yeyote anayesoma historia ya taifa hili tangu mwaka 1964 hatukuweza kuipitia Katiba ya Muungano na kuweza kuona ni nini hasa wanachokihitaji wazanzibari tokea mwanzo. Kwa hivyo, kama alivyosema

Mhe. Waziri kwamba kuna wanahistoria ambao walitueleweshe hayo na historia imeshasema kuwa hayo hayakupatikana.

Kutokana na hali hiyo, basi ni imani yangu kusema kwamba nafasi hii ni kweli kabisa wazanzibari inapaswa tushikamane na tujiulize maswali nini hasa kama wazanzibari tunakihitaji katika rasimu ambayo iko mezani wakati huu na yepi hasa tunayoyahitaji.

Sasa baada ya kuona yepi au nini tunakihitaji kwa umoja wetu bila ya kujali itikadi ya vyama vyetu vya siasa, kwa sababu vyama vilikuwepo mwanzo, viliondoka na vimerudi tena. Kwa mfano, tulikuwa na mfumo wa vyama vingi nyuma, ukaja mfumo wa chama kimoja na sasa vimerudi vyama vingi, lakini nchi yetu ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu kujua nini tunakihitaji katika rasimu hiyo kwa ajili ya kupiga hatua taifa letu hili.

Mhe. Spika, niwaombe wazanzibari wote kwa pamoja tushirikiane, tushikamane na tuwe pamoja bila ya kuhitilafiana, tuweze kuona ni nini tunachokihitaji, ili tuweze kukifikia kwa pamoja kwa maendeleo ya taifa letu hili sisi na kizazi kinachofuata.

Baada ya kuyasema hayo, Mhe. Spika niseme kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia 82, kwa sababu kuna mambo nataka ufafanuzi. Kwa hiyo, nitakapopata ufafanuzi nitaunga mkono kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* kwa kunijaalia leo kupata nafasi adhimu ya kuzungumza machache kuhusu hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa mwaka wa 2013/2014.

Pia naomba kutoa shukrani za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuchangia bajeti hii.

Sasa nianze moja kwa moja na mahakama. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 14 wa kitabu hichi cha bajeti imeeleza naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 14 kitabu cha bajeti mwaka 2013/2014 unaeleza hivi:-

> “Mahakama ndicho chombo chenye jukumu la kikatiba la kusimamia utoaji wa haki. Katika kufanikisha jukumu hili usikilizaji wa kesi za jinai, madai pamoja na rufaa za jinai na madai ni jambo la msingi …”

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie ufafanuzi tu kuhusu namna ya kesi zinavyokwenda.

Kwa kweli mahakama ni pahala pekee panapotoka haki. Lakini jambo ambalo mimi wakati mwengine huwa ninajiuliza ni kuona kuwa kuna watu wanapelekwa mahakamani na kesi zinafunguliwa na wakakaa muda mrefu ndani wakakosa dhamana ya kutoka nje eti kwa sababu wakitolewa wataharibu ushahidi na wakati upelelezi unaendelea.

Mhe. Spika, swali langu hapa kwa sababu mimi si mtaalamu wa mambo haya, basi nilifikiria kwamba mpaka mtu akikamatwa na kuwekwa kizuizini huwa tayari ameshabainika kuwa na kosa, na nadhani si vizuri na wala si haki kumuweka mtu kizuizini kwa kusingizia tu akakaa muda mrefu na halafu mwisho kesi ikawa *dismissed* na kuonekana kuwa hana kosa.

Kwa hivyo, swali langu hii mahakama kimamlaka hasa inakuwa vipi mpaka huyu akubali kukaa kizuizini chini ya amri ya mahakama na kesi yake iendelee, lakini mara nyingi kila ikipangiwa tarehe, basi kesi ile huwa inapangiwa tarehe kwa kisingizio kuwa upelelezi bado unaendelea.

Sasa kwa nini mtu akawekwa kizuizini bila ya kufanywa upelelezi wa kutosha na kuonekana kuwa iko haki au kuna sheria iliyosema kuwa mtu yeyote anaweza kuwekwa kizuizini wakati wowote na upelelezi utaendelea baadaye. Kwa hivyo hapo naomba nipate maelezo, kwa sababu sote tunashuhudia kuna kesi nyingi za namna hiyo hutokea, na mtu hukaa kwa muda mrefu na halafu mwisho ikawa hakuna kosa.

Kesi inayopelekwa huwa ni kesi inayomuhusu binaadamu. Kwa maana hiyo, wajibu wa uzuri wa kesi ihukumiwe na hukumu itoke, na baadaye yafuatie mambo mengine. Lakini utaona zinapelekwa kesi nyingi mahakamani na mwisho pengine ni chache zinazofunguliwa mahakamani na kusikilizwa nyengine huwa zinabakia kama zilivyo. Kwa mfano, tukiangalia ukurasa huu wa 61 wa kitabu chetu cha bajeti, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 61 wa kitabu cha bajeti mwaka 2013/2014 unaeleza:-

> “Vuga katika sehemu ya mahakama jumla ya kesi za madai zilizofunguliwa ni kesi 100, kesi zilizofunguliwa ni 50 na zilizotolewa uamuzi ni 6”.

Kwa hivyo, pamoja na kesi zilizofunguliwa kuna kesi 94 bado hazijatolewa uamuzi na kati ya hizo 50 hazijafunguliwa hasa na zinapelekwa tu. Mhe.

Spika, kuna sababu zipi kuwa na mrundikano huu wakati mtu ukimfungulia kesi anakuwa yumo katika matatizo ya kutaka kujua ni kitu gani kitatokea.

Mfano wa pili Kadhi wa Rufaa Unguja kesi za madai; kuna jumla ya kesi 50 zilizofunguliwa, lakini hakuna hata moja iliyofunguliwa kwa kusikilizwa. Kwa hivyo, hakuna hata moja iliyotolewa uamuzi.

Mhe. Spika, tukiendelea na suala kama hili kwenye ukurasa 62 Mkoa wa Wete kuna jumla ya kesi 53 na kesi zilizofunguliwa ni mbili tu na wala hakuna iliyotolewa uamuzi. Kwa kweli ni kesi nyingi kwa mfano Wilaya ya Mfenesini jumla ya kesi ni 200 na hakuna kesi iliyofunguliwa na wala iliyotolewa hukumu hakuna.

Sasa ikiwa taarifa hiyo ndio kama nilivyofahamu mimi mwenyewe basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi anisaidie maelezo ya kina kwamba kwa nini kuna mrundikano mkubwa sana wa kesi kama hizi hazifunguliwi kwa ajili ya kutolewa uamuzi, ni kwa sababu mahakimu tulionao ni kidogo au kesi za ina yake mahakimu wetu hawana uwezo na zinawekwa kwa ajili ya kutafuta mahakimu wengi au kuna sababu nyengine kuhusu jambo hili.

Vile vile Mhe. Spika, nataka kuuliza kwa wale watu wanaofunguliwa kesi halafu tena baada ya kukaa sana gerezani bila ya dhamana na mwisho ikaonekana hawana hatia, je wanalipwa chochote au inakuwa ndio basi? Hili pia naomba kupatiwa maelezo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kwenye ukurasa wa 36 wa kitabu chetu cha bajeti, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kitabu cha bajeti mwaka 2013/2014 ukurasa 36, unaeleza hivi:-

> “Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kisheria ina majukumu ya kusajili vizazi na vifo na kutunza kumbukumbu zitokanazo na usajili huo …”

Katika kifungu cha 102 kinaeleza hivi:-

> “Usajili wa Vizazi na Vifo umekuwa na matatizo mengi kwa muda mrefu na unaleta usumbufu wa mara kwa mara kwa watu wanaohitaji huduma ya vyeti vya kuzaliwa. Ukosefu wa magamba ya kuchapishia vyeti, uwezo mdogo

wa uchapishaji na ukosefu wa fedha ndio matatizo ya msingi yanayosababisha hali hiyo …"

Mhe. Spika, siendelei namna gani wizara inachukua juhudi kuondoa mambo hayo, lakini hii ndio hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, takwimu ni kitu muhimu sana kwamba kujua wangapi wanazaliwa na wangapi wanakufa ni jambo muhimu sana. Kwa kweli ninashukuru kwamba masheha wetu kwa hili mtu anapozaliwa tu basi wazazi wanapokwenda huwa wanapata karatasi ambayo ndio kitambulisho cha kupata hicho cheti cha kuzaliwa, yaani hiyo *register*. Lakini kwa ukosefu wa magamba hivi sasa watu wengi hawana vyeti.

Hata hivyo, kuna manung'uniko ya baadhi ya watu kwao wao sijui ni kwa umaarufu wao wanapokwenda tu huwa wanapata vyeti ghafla. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze, kwamba kwa nini wengine wanachukua muda mrefu sana na wengine wanapata kwa muda mfupi, kitu gani kilichosababisha hivyo?

Sasa Mhe. Spika, najua cheti cha kuzaliwa kina umuhimu wake tokea Kikatiba na mpaka mambo ya kujalizwa tu. Kwa hivyo, hivi sasa kwa mujibu wa sheria mwananchi yeyote mzanzibari na mkaazi wa Zanzibar aliyetimia umri wa miaka 18 na kuendelea anatakiwa awe na Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi japo kuwa ameshatimia umri wa miaka 18 na kuendelea, lakini kwetu sisi kama hana cheti cha kuzaliwa huwa hatambuliwi, anajulikana ndiye, sura inaonesha tena anacho kila kielelezo, isipokuwa cheti tu hana, basi huwa hatambuliki.

Kwa maana hiyo, kama hukupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, basi maana yake huandikishwi kuwa ni mpiga kura japo Sheria ya Vitambulisho na hata Sheria ya Uchaguzi hakuna mahala ilipoelezwa kwamba cheti ni lazima.

Mhe. Spika, kwa kadhia hii tuliyonayo ya kukosa vyeti vya kuzaliwa inafanya mambo makubwa kukosekana ambayo ni ya kumkosesha mtu haki yake.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri, kwamba kuna mambo mengine ni lazima yawe ni ya dharura kwa vile Katiba ama Sheria imesema kuwa "Mtu akitimia umri wa miaka 18 na kuendelea anayo haki ya kupewa kitambulisho hicho wakati ni mzanzibari mkaazi na ametimiza masharti ya uzanzibari" na wala hakikutajwa cheti, lakini ni kwa sababu lazima awe na cheti sasa aone kutokupatikana cheti kwako basi ni kumzuia

mtu kukosa kitambulisho kile na akikosa kitambulisho kile, maana yake hapati kitambulisho cha kupigia kura na anabakia apige kura ya Muungano.

Mhe. Spika, jambo hili nalipenyeza kwa sababu ninayezungumza naye ni Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Wakati Tume ya Vitambulisho haina ushauri wa mtu wala taasisi yoyote isipokuwa ushauri wao wa karibu wa mara kwa mara ni kwa Tume ya Muungano. Sasa kwa nini huku kwenye Tume ya Muungano ikiwa hakuna matatizo na cheti cha kuzaliwa, lakini hawa wanaokwenda kutafuta ushauri kule watu wanakwenda kutafuta ushauri kule wao wanatuwekea vikwazo na inakuwa haki inatendeka.

Jambo jengine katika vyeti vya kuzaliwa kuna wazazi kwa sababu ya kutojua, kupitikiwa au sijui hawakuwatafutia watoto vyeti vya kuzaliwa wakati walipozaliwa na ni wazanzibari ambao wametimiza masharti. Kwa mfano, hivi sasa kuna wazee hasa ambao miaka 80 au 90, watu wazima , vijana na kuna wengine vijana wadogo kuanzia umri wa miaka 18 na kuendelea kidogo pia hawana, yaani ni kundi kubwa sana na kundi hili lote linakosa kutumia haki yake ya kidemokrasia ya kueleza serikali wanayoitaka kwa sababu ya kukoseshwa kitambulisho cha kupigia kura. Kwa vile hili ni janga la kitaifa na limetokea kwa watoto hawa na wao hawakuwa na makosa. Mimi ningelimuomba Waziri wetu wa Katiba na Sheria. Nchi hii ni nchi ya demokrasia, na serikali iliyopo ni serikali inayofanana na wananchi wenyewe na wananchi kosa lao hawakupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Kwa hivyo ifanye kila inavyowezekana itafute fedha kama itakapopatikana, au ishirikiane na wizara inayohusika kwa namna anavyojua yeye mwenyewe ni mtaalamu ili watu hawa kwa sababu tunajua watu wetu ni masikini sana, hakuna mtu anatumia Tsh. 219 kwa siku, akapata pesa Tsh 42,000/- kwa habari ya cheti. Hasa watu wasaidiwe waingie katika kazi ya kupigania haki yao ya kuweka serikali yao na kushirikia na watu wao katika mambo ya siasa na mambo ya chaguzi ili nchi yetu iweze kuimarika

Hili naliomba sana na hili ni lazima lifanyiwe haja ya dharura. Nasema hivyo kwa sababu kabla hatujaweka ulazima wa vyeti vya kuzaliwa kuna watu hapa walipewa vipande vya kupigia kura na walipiga kura miaka yote hiyo ya nyuma,lakini hivi sasa wamebakia na vipande vyao vya nyuma watu wazima, lakini wanakosa haki yao, wakipiga kura wanapiga ya Muungano tu. Jambo hili linatuumiza kuona siku ya kupiga kura watu kuwachagua viongozi wao wenzetu wanawachagua Rais wa Jamuhuri ya Muungano peke yake, wakati ni Wazanzibari hasa.

Kwa hivyo naomba Mheshimiwa kwa kuondoa tatizo hili atusaidie, afanye kama inavyowezekana atafute mfuko wa fedha hawa watu kwa utaratibu wa kuwatumia masheha waorodheshwe, wasaidiwe ili waweze kuiingiza katika shughuli hizi ipasavyo pamoja na wenziwao.

Mheshimiwa jengine ni Ofisi ya Mufti. Ofisi hii ina kazi kubwa sana tena kazi ya uadilifu, tena kazi ya kidini, kazi ambayo inataka taaluma kwa mujibu wa hali ya juu halafu na uadilifu. Tukiangalia ukurasa wa 30 wa kitabu chetu cha bajeti hapa kwa ruhusa yako naomba kusoma Mhe. Spika.

"Ofisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhima kisheria ya kutoa miongozo kuhusu masuala ya kidini kwa Zanzibar. Ofisi ya Mufti kwa mwaka wa fedha 2012/2013 imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa malengo yake ya kibajeti, yakiwemo kuratibu na kusimamia shughuli za kiislamu kama vile mikutano ya Baraza la Maulamaa, mikutano ya mikutano ya kuandama kwa mwezi, ziara za misikitini na madarasani na kutatua migogoro na kushajihisha amani na utulivu, hii imefanya kazi kubwa sana."

Mhe. Spika, mimi hapa sina wasi wasi. Kwanza kwenye migogoro ya ndoa. Hapa kazungumzia yule kijana wetu kwa bahati mbaya, wanaopata ujauzito kwa njia ambayo siyo ya kihalali, maana ni watu ambao hawajaolewa au kwa bahati mbaya wanaokamatwa na kitendo hicho kabla ya watu kuoana. Mara nyingi hukmu huwenda na watu hawa wakaozeshwa na mambo yakamaliza hapo.

Mimi suala langu nauliza kwa mujibu wa sheria za ndoa ni sehemu gani iliyoeleza kuwa watu wakifanya zinaa kuozeshana ndio suluhishi. Hii naomba nielekezwe kwa sababu ninavyojua dini ya kiislamu imeweka hukumu zake kwa watu kama hawa. Na kama sikosei kwa sababu sikusoma nasikiliza tu dini hakuna kuoana watu waliokamatwa katika hali hiyo.

Pili hii Ofisi ya Mufti Mhe. Spika, moja katika kazi yake inayofanya vile vile ni kuzungumza kuhusu mambo ya kuandama kwa mwezi na kwa mujibu wa utaratibu kama mwezi haukuonekana wa Ramadhani hatutakiwi tufunge, na kama haukuonekana hatutakiwi tufungue. Na hii ni nchi moja, tena ni kisiwa lakini utamaduni tulionao ambao unatokea si miaka mingi sana iliyopita. Tunajua kuwa mwezi ni mmoja na tarehe ni moja, na kila kitu kimewekwa kwa wakati wake. Imekuwaje leo Zanzibar na baadhi ya sehemu za dunia iwe watu wanafunga katika siku tofauti na kufungua siku tofauti wakati dini yao ni moja.

Naomba nipatiwe maelezo yanayoruhusu kila mtu kujiamua siku yake ya kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na siku yake ya kufungua ya mwisho

kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambayo inaruhusu kuchagua kila mtu siku yake. Na ikiwa hakuna basi iwe ni moja tu kwa vile dini yetu ni moja na tunatakiwa tushirikiane tuwe kitu kimoja katika mambo ya dini na wala tusifarikiane. Ikiwa kuna mambo tofauti ya kitu kimoja lazima mmoja atakuwa kapitikiwa kufunga au kutofunga kwa siku ya kufunga, na kufunga kwa siku ya kutofunga ni kosa kubwa sana. Na watufafanulie hapa ili tujue ni nani mwenye makosa kwa sababu sote tutakufa na tutahukumiwa.

Jengine naomba niingie katika Rasimu ya Katiba ya Muungano. Mhe. Spika, hakuna asiyejua kuwa muungano ni wa nchi mbili. Muungano wa Tanzania ni Muungano wa nchi mbili ni muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na hizi ni nchi mbili zilizokuwa huru. Hapana asiyejua kuwa kama ilivyoandikwa katika Katiba ya Muungano Sehemu ya Kwanza, Jamhuri ya Muungano na watu wake kuwa Tanzania ni nchi moja na Jamhuri ya Muungano hili ni kosa sana ni kuitoa Zanzibar na kuitoa Tanganyika katika ramani ya dunia. Hapana asiyejua kuwa waliotunga Katiba hii ya Zanzibar toleo la 2010 walikuwa wanaijua zaidi Katiba ya Muungano kuliko sisi tunaozungumza, na wakaona waandike Zanzibar ni nchi pamoja na mipaka yake. Wanajua wazi kuwa kusema hivi ni kupingana na kifungu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kuwa eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Zanzibar ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania imepakana nayo, lakini na sisi tumesema eneo la Zanzibar ni eneo lote la visiwa hivi viwili vikubwa pamoja na bahari iliyopakana nayo. Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenye mamlaka ya kuigawa Tanzania katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengine, isipokuwa kwa Zanzibar atashauriana na Rais wa Zanzibar na huku kuna kifungu cha Rais wa Zanzibar ndiye mwenye mamlaka kwa kufuata maelekezo yanayotumwa na Baraza la Wawakilishi.

Sasa Mheshimiwa, Mwenyezi Mungu katujaalia tumepata Rasimu ya Katiba ya Muungano na wakati tunajua kuna matatizo chungu nzima tunaziita kero za Muungano. Hao wenzetu wanaosema twende kule kule katika nchi moja. Haya lakini ujue huku ndio tulikokwenda mpaka tukaambiwa Tanzania ni nchi moja ndio mwisho hapa hakuna zaidi. Lakini kuna kero zilizokuwa hapa hazimithiliki. Sote ni binaadamu tumepelekwa na sheria, tuna akili na tunafanya kazi kwa maslahi ya kuuliza muungano wetu lakini kila nchi ijue kuwa ipo na ina mamlaka yake na inafanya shughuli zake.

Mhe. Spika, hatuendelei maisha kama mambo ya nje yatakuwa ni mambo ya muungano. Sisi tupate kwa kutoka Tanganyika, hatuendelei maisha, wenzetu wa Tanganyika wakajiita Tanzania Bara kwa kufanya ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wakaitumia kwa mambo yale, na mambo yote sisi tukabakia na

serikali kibutu. Mimi ningezungumza sana hapa lakini wakati umekwisha. Ushauri wangu Mheshimiwa waitumie fursa hii, tukijua muungano tunaokwenda nao unaingia katika miaka 50 hivi sasa umekuwa na matatizo tele yasiyomithilika, tena mengine yalikuwa ni ya kijeuri hasa.

Sasa tuitumie fursa hii tuone kuwa Zanzibar ipo kama Zanzibar na mamlaka yake kamili hakuna Tanzania Bara kuwe na Tanganyika na mamlaka yake kamili, halafu ule muungano ambao utakuwa endelevu wa kuitwa dunia nzima kwa maslahi yetu sote. Kwa hayo machache Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuandalia hotuba hii na kuiwasilisha leo hii tukaweza kuijadili hapa. Mhe. Spika, nataka niende haraka haraka ili na wenzangu kuweza kuchangia.

Nianze na ukurasa wa 8 kwenye Idara ya Mipango Sera na Utafiti, paragrafu ya 22 ambapo Mhe. Waziri alikuwa anatuzungumzia miongoni mwa majukumu ya Idara hii ya mipango, sera na utafiti ni kuratibu shughuli za NGOs.

Mhe. Spika, mimi nima maswali kidogo hapa katika suala hili la NGO maana kuna baadhi ya NGO zinapata misaada kutoka nje zinaingiziwa moja kwa moja kwenye NGO hakuna ambako labda zipite kwenye wizara, halafu wizara ndio iitafute ile NGO izipelekee. Zinakuwa zinaomba kwa wafadhili na zinaletewa moja kwa moja kutoka kwa wafadhili zinapewa zile NGO, lakini nilikuwa nataka kujua tu Mhe. Waziri sijui utaratibu wake ni upi wa kuzikagua hizi NGO katika masuala ya fedha.

Je, fedha zile wanapopewa zinakaguliwa. Kwa sababu zile pesa zinapoletwa zinaletwa kwa niaba ya wananchi. Kwa sababu wale wanafanya shughuli za wananchi. Na zile shughuli mara nyingi sana wanakuwa hawawalipishi au wanatoza kodi ndogo sana, lakini mara nyingi zinakuwa *free* katika mambo ya sheria na vitu vyengine. Sasa nilikuwa nataka kujua utaratibu unaotumika na wizara katika kuona kwamba NGO zile zinakaguliwa na matumizi yale yanakwenda kwa mujibu wa utaratibu, maana yake zile ni fedha za wananchi lakini haikuletwa serikalini moja kwa moja imeletwa kwenye NGO na NGO ndio maana zikawa zinasajiliwa na yeye ndiyo anasema kwamba idara hii inaziratibu. Sasa nilikuwa nataka kuona namna inavyoratibu katika masuala ya fedha.

Mhe. Spika, nisogee kwenye ukurasa wa 14 kwenye Mahkama. Mahkama ni chombo kikubwa sana maana huu ni muhimili kuna kazi kule ya tafsiri sheria. Mahkama ni mahala ambapo panatendwa haki au mtu kama mna matatizo yenu mnapokwenda pale mnakwenda kutatuliwa kwa namna ya haki ilivyo, lakini nimejaribu kuangalia kwenye hiki kitabu nikakaangalia kwenye buku kubwa huku nilikuwa naangalia zaidi kwenye lile fungu la wale mashahidi. Tulikuwa tunapata malalamiko mengi sana Mhe. Spika, kwamba mashahidi wanakwenda kutoa ushahidi lakini ile haki yao kulipwa inakuwa pagumu. Na si kosa la Idara ya Mahkama wanatwambia ni ukosefu wa fedha. Kwanza fedha zenyewe ni chache halafu kule kuingizwa kwenyewe nako ni tatizo.

Sasa nilikuwa nataka niiombe serikali katika eneo hili kwa kweli pale mahala wapatizame kwa macho mawili. Nimechungulia buku mara hii nimeona kidogo limetononoka lile fungu la mashahidi ilikuwa mia moja na kidogo mwaka jana lakini mwaka huu naona kama lina milioni 300 na kitu kidogo hivi, sasa nikasema kidogo afadhali. Sasa niwaombe na hawa waratibu wa shughuli hizi katika Idara ya Mahkama hii kwamba wasimamie vizuri. Haiwezekani mtu amekwenda au ameitwa Mahakamani kwenda kutoa ushahidi lakini pana haki yake. Yaani ile Mahakama tunaiita ndio chombo cha kutoa haki, halafu inafika mahala mtu na yeye haki yake na chombo kile kile hapewi, hawezi kuelewa mwananchi wa kawaida kule kwamba bajeti ndogo, bajeti finyu, pesa hazijaingia. Anachojua kwamba ni Mahkama kwamba haijamtendea haki.

Sasa nilikuwa nataka niombe sana hili, kwamba tuliangalie vizuri na tuwe wasimamizi wazuri katika hili, kuhakikisha kwamba mashahidi wanaokwenda kutoa ushahidi, basi wale wenye stahiki zao za kulipwa pale walipwe baada tu ya kwisha kufanya ile kazi. Maana wengine wanakuja kwa nauli ya kukopa wanakuja pale anasema nakwenda nikirudi nitarejesha. Matokeo yake anatakiwa aende tena kwenda kuisikiliza, anarudi haijawa tayari, anakwenda tena kuisikiliza mwisho wake hicho ambacho alikuwa apewe kinamalizia kwenye nauli. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana hili Mhe. Spika, naiomba Wizara ilisimamie vizuri hili la kuwapa haki zao mashahidi.

Mhe. Spika, jengine katika hili ni baadhi ya Mahakimu wetu wanakula rushwa, inasikitisha sana. Mahakama ni chombo cha kutoa haki, lakini inasikitisha kuona kwamba kuna baadhi ya watendaji katika chombo hichi sio waaminifu. Nilikuwa nataka nimuombe sana Mhe. Waziri katika hili awe mkali kweli kweli, ingawa naye atakwambia huu ni muhimili kando, yeye anatokea muhimili mwengine wa serikali. Lakini yeye ndiyo msimamizi. Anakwambia yupo msimamizi Mkuu, lakini na yeye ndiye anayeiangalia kwenye Sera yupo yeye na ndio maana leo akawa anaiombea hapa.

Hakushuka hapa Mrajis wa Mahkama kuja kuomba yupo yeye Mhe. Waziri ndiye anayeomba fedha kwa ajili ya matumizi ya chombo hichi.

Sasa nilikuwa nataka nimuombe sana, na nafikiria Mrajisi mwenyewe yupo anatusikia, katika eneo hili Jaji Mkuu mwenyewe yupo kuna baadhi ya Mahakimu wanatia aibu kabisa kabisa. Hichi ni chombo kwa kutoa haki, anapofika mtu mahala anakwenda kudai haki yake kile chombo cha kutoa haki ndicho kinachomdhulumu, tunafika pabaya. Tunawakatisha tamaa wananchi wetu na mwisho wa siku watakuwa chombo hichi hawakiamini tena. Matokeo yake Mwenyezi Mungu atuepushie mbali ndio zitaanza vurugu, maana sasa mtu atakuwa anaona hana haja ya kwenda Mahakamani kwa sababu haki haipati, ataanza kung'ang'ana huku huku mitaani.

Kwa hivyo tuondoshe hili, tujaribu sana. Mimi nafikiri hata ukiangalia maslahi katika chombo hichi yamesaidiwa sana, yamekuzwa kwa ajili ya kuwatengeneza mahakimu wetu ili wakae vizuri, lakini sasa kuna baadhi ya wengine wanaharibu. Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hili hata kama una takwimu hebu tuambie kidogo kama wapo wawili watatu ambao umeshawahi kuwachukulia hatua katika jambo kama hili hebu utakapokuja tusaidie utupe matumaini kidogo. Tuone kama hili jambo kweli mnalisimamia, kwa sababu hata mwaka jana lililalamikiwa sana hili ya namna ya chombo hiki cha kutoa haki kinavyowanyima haki watu.

Kuna baadhi ya Mahakimu kwa kweli wanatia aibu, Mhe. Waziri ni aibu kweli hii. Unamkuta mtu dhaifu kabisa keshadhulumiwa huku anakwenda kule anaambiwa aaa! Hapa tengeneza laki mbili kwanza ndio mambo yakae sawa. Ni aibu kama angelikuwa nayo angetengeza huku huku, lakini kaja kwenye chombo cha kutoa haki, mpeni haki yake hata kama ni mnyonge, haki yake apewe.

Kwa hivyo nakuomba sana Mhe. Waziri tusaidie katika hili na utakapokuja hapa utusaidie tuone kama kweli unalisimia vizuri ili na sisi kidogo utupe moyo. Tuambie zile hatua ambazo umewahi kuwapata wawili watatu ambao wamefanya hili jambo na umewachukulia hatua, tuone katika hilo.

Mhe. Spika, nisogee mbele kidogo katika ukurasa wa 18 wa kitabu cha Mhe. Waziri kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar. Mhe. Spika, kwanza mimi nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa jitihada zake anazofanya za kuhakikisha kwamba chombo hiki anakiweka katika mwenendo mzuri. Ni hivi majuzi tu tulipitisha sheria yake hapa ya kuanzishwa kwake kwa ile ofisi kuiweka vizuri. Maana ipo lakini sasa tulikuwa tunaiweka katika sheria vizuri. Nina hakika Mhe. Spika, Mwanasheria Mkuu ni mtu makini

atasimamia yale ambayo tulikubaliana nayo katika chombo hichi. Atayasimamia na atayafanyia kazi vizuri.

Lakini Mhe. Spika, nimuombe sasa Mwanasheria Mkuu kwenye suala la mikataba ile ya serikali. Kuna mikataba huku tukipita kukaguakagua kwa kweli inatia aibu. Ingawa ile sheria wakati ule ilikuwa haijapita, lakini ilikuwa imeshafungwa ile mikataba. Kwa kweli ni mikataba ya ajabu kweli kweli. Mikataba mingi unayoitizama hakuna pahala ambapo unaikuta serikali inashika kitu, yote imeelemea kwa yale makampuni au kwa wale watu wa upande wa pili dhidi ya serikali.

Mhe. Spika, juzi liliulizwa swali la msingi, halafu tukauliza maswali ya nyongeza kwenye Wizara ya Miundombinu, juu ya mikataba ya barabara zile za Gando, Wete n.k. Tumeona namna ya jawabu ya nyongeza lilivyokuja kwamba serikali imekula hasara zaidi ya 1.2 *billion*. Ukitizama sababu ya hasara ile ni mikataba mibovu. Umewekwa mkataba mbovu, basi watendaji inaonekana walikuwa wana ujanja ujanja katika mikataba ile.

Sasa nimuombe sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kama upo uwezekano kuna baadhi ya mikataba ambayo tayari imeshafungwa ni bora mkai - *review*. Tuangalie tunaweza kuukoa kiasi gani kwa hasara ambayo serikali itaipata. Kwa sababu fedha hizi tunaposema za serikali maana yake ni pesa za wanalipa kodi, wao ndio wanaokuja kuzilipa fedha hizi. Ukizitizama zile fedha za mikataba ya barabara si fedha za wahisani. Muhisani kama amakuidhinishieni fedha zile amekupeni kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Hamkuzitumia wenyewe au mmezitumia lakini kuna madai yameletwa na Mkandarasi hayaendi kwa muhisani, yanakwenda kwa wananchi wetu. Walipa kodi ndio wanaotozwa fedha zile.

Sasa nilikuwa nataka niombe sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ajaribu kuipitia ile kama kuna utaratibu basi namuomba sana aipitie baadhi ya mikataba tuiangalie upya, kwa sababu namna ilivyofungwa aaa! Itakuwa ni hasara siku zote kwa serikali. Hili nilikuwa nataka nimuombe sana Mhe. Spika.

Mhe. Jengine katika Ofisi hii ni maslahi ya watendaji katika ofisi hii. Mhe. Spika, ukiangalia kwa haraka haraka tu utaona kada ile yalivyokaa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, haipitishani sana na hata ya hawa kwenye Mahakama na pia wa Muendesha Mashtaka. Lakini maslahi ya hawa wenzetu wamekuwa wanalalamika. Nilikuwa naiomba sana serikali iangalie suala la maslahi katika ofisi hii.

Nisogee mbele Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 26 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa kweli pale mahala mimi nataka nitoe pongezi nyingi sana

kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli tumeona jitihada zake na uwezo wake Mwenyezi Mungu amzidishie. Ukiangalia hapa kwenye paragrafu ya 75, Waziri wa Katiba na Sheria anasema

"Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilikusudia kukamilisha kazi ya kuweka mfumo wa uendeshaji mashtaka kiraia katika Wilaya ambazo bado polisi wanaendesha mashtaka.Katika kutekeleza hilo Ofisi imeajiri Wanasheria wapya watano ili kuwapeleka kwenye Wilaya hizo."

Lakini Mhe. Spika, mimi ndio maana nikasema nampongeza sana Mkurugenzi wa Mashtaka kwa jitihada zake. Anataka kuhakikisha kuwa mahala ambapo pana Mahakama basi polisi ile kazi ya kuendesha mashtaka sio ya kwao. Ni kazi ambayo inatakiwa iendeshwe kiraia. Polisi waendelee na kazi zao za uchunguzi, wampelekee Mkurugenzi wa mashtaka ili yeye aweze sasa kuendeleza kesi zile.

Mhe. Spika, hapa napo pana tatizo kama watu hawa au watendaji hawa nao hatukuwatengenezea maslahi mazuri basi hii kazi itashindikana. Na hii kazi ni muhimu sana kabisa. Kwa sababu wananchi wetu wanakitegemea sana chombo hichi kwamba ndio kiwaandalie mambo yao na wanakiamini kwamba ndicho kinachoandaa mambo yao. Yaani ile kesi nzima inaandaliwa hapa halafu ndio inafunguliwa kule. Sasa ni lazima kuwe na ushirikiano baina ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama. Sasa kama maslahi tumeyapeleka upande mmoja Mhe. Spika, upande wa pili tumeuacha hapa naona utendaji utakuwa si mzuri. Matumaini ya serikali kufanya hivi kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapatiwa haki sawa kwa wote. *(Makofi)*

Hee! Nimekufahamu Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Spika, hawa watendaji tusipowaangalia vizuri kwenye hii ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka basi ile kazi ya tafsiri ya sheria au utoaji wa haki kule kwenye Mahkama nao utaonekana kuwa dhaifu. Kwa sababu wao ndio wanaolianza lile shauri lenyewe mpaka likaenda huko Mahakamani. Lakini wao kwenye maslahi tumewaacha kando. Basi nilikuwa naiomba sana serikali Mhe. Spika, iliangalie hili. Maslahi kwa waendeshaji wa mashtaka. Ni tatizo na kweli wanachokizungumza, haya wanayazungumza Mhe. Spika, wanachokizungumza ukikizama kina mantiki.

Ukiangalia hata elimu hawa wanafanana elimu zao wote, wote wamesoma sheria kama mtu ana- digirii kama mtu ana *Master* kama mtu ana *PHD* ya Sheria. Lakini kwenye maslahi unaweza ukamkuta ana digrii au ana *Master* lakini kwa sababu yupo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ukamkuta yeye

anapata kidogo kuliko yule ambaye yupo kwenye muhimili mwengine wa Mahkama akawa yeye anapata kikubwa. Sasa nilikuwa naiomba serikali katika hili iliangalie sana.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuingia kwenye vifungu kidogo, sina mengi kwenye vifungu kidogo, naomba nivumilie. Niende kwenye kifungu 0601 Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwenye Kasma ya 220700 Matengenezo ya Ofisi Kifungu 220701 Matengenezo madogo ya Ofisi. Hapa kidogo nilikuwa nataka Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie matengenezo ya Ofisi kuna milioni 9 zimetengwa wakati mwaka jana alikuwa ana 12.

Mhe. Spika, nisogee hapo hapo kwenye 272108 Kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii. Nilikuwa nataka ufafanuzi katika fungu hili maana kuna milioni 5 nalo pia aje atusaidia Mhe. Waziri sijui shughuli zipo. Lakini nende kwenye Kasma 14 hii ya Mahakama kifungu 0601 Ofisi ya Kadhi Mkuu kwenye fungu 211201 kuna kodi ya nyumba hapa milioni 28 nayo pia nilikuwa nataka maelezo yake kidogo aje atusaidie Mhe. Waziri.

Halafu niende kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu fungu 15 kasma 311200 ununuzi wa mashine na zana kwenye kifungu kidogo 311202 Ununuzi wa gari, pana milioni 80 lakini mwaka jana alichukua milioni 60, mwaka juzi 65 sasa hebu kidogo Mhe. Waziri utakapokuja uje utusaidie labda mara hii Mwanasheria Mkuu unataka kumnunulia Prado kama lile analopanda Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nimalizie kwa fungu 0301 Afisi Kuu Pemba. Nikiangalia mafungu mengi haya imekuwa kama *copy and paste* maana mwaka jana alitumia hicho hicho na mwaka huu anaomba hicho hicho, mengi sana yapo katika staili hiyo. Lakini kwenye fungu la virudishaji 220200 naomba nipate ufafanuzi katika fungu 220201 Chakula la Vinywaji. Naomba hapa nisaidiwe ufafanuzi kuna milioni kumi na tano na laki sita. Mwaka jana ilikuwa ina milioni nne na laki tisa, mara hii ime-*shoot* mpaka kumi na tano na laki sita. Nilikuwa naomba ufafanuzi katika hilo, *and then* narudi tena na kwenye kifungu 0501 Ofisi ya Mufti kwenye matengenezo ya Ofisi na nyumba 220700 basi nipate maelezo katika mafungu yote mawili 220701, 220702 matengenezo madogo na matengenezo makubwa. Mhe. Spika, ninakushukuru ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na vile vile namuomba aniongoze katika kuchangia.

Mhe. Spika, vile vile ninakushukuru wewe sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwanza kutokana na hali yangu, pili naona muda umeshamalizika isipokuwa kuna mambo kidogo tu naomba Mhe. Waziri anipatie ufafanuzi ili niweze kuunga mkono bajeti yake.

Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba yake na pia kwa vile anavyotekeleza majukumu yake. Mhe. Spika, pia ninampongeza Mhe. Waziri kwa ujenzi wa jengo kubwa, zuri na la kisasa la Wizara yake. Na pia ninampongeza Mwanasheria Mkuu kwa jengo zuri na la kisasa. Vile vile Mhe. Spika, nawaomba na Mawaziri wengine waige mfano wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, Ofisi ya Katiba na Sheria ina majengo yake katika Kisiwa cha Pemba ambayo ni mabovu, na hayana hadhi hasa. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri anieleze ana mpango gani katika kisiwa cha Pemba au amekusudia nini katika ujenzi wa Ofisi zao katika Kisiwa cha Pemba hasa katika Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Spika, majengo haya yote mawili yapo katika eneo la Mazizini, katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anieleze ana mpango gani wa kujenga Ofisi zake katika kisiwa cha Pemba, na vile vile namuomba alitizame jengo la Mahkama ya Chake Chake kwa jicho la huruma kwa kulifanyia matengenezo ili hadhi ya mahkama iweze kutunzwa.

Mhe. suala jengine ambalo naomba nipate ufafanuzi ni kuwa Mhe. Spika, kwa muda mkubwa siku nyingi hasa kulikuwa kuna haja ya Jaji mkaazi Pemba. Sasa naomba Mhe. Waziri anieleze suala hili limepata ufumbuzi gani.

Vile vile Mhe. Spika, sasa naomba nichangie katika Ofisi ya Mufti. Ofisi ya Mufti inafanya kazi kubwa tena nzuri. Naipongeza sana hasa kwa kuanzisha maktaba hii itasaidia sana kueneza taaluma kwa wananchi wetu. Lakini Mhe. Spika, katika kiambatanisho namba 1 ukurasa wa 54 na 55 wa kitabu cha bajeti una mambo naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi.

Kwanza ni matumizi mengineyo ya Ofisi ya Mufti ni asilimia 39 tu lakini matumizi mengineyo ya Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana ni asilimia 102. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anaweza kunieleza ni sababu gani ya tofauti hii kubwa ya upatikanaji wa fedha. Mhe. Spika, vile vile Mhe. Waziri haoni hapa hii ni kuidumaza Ofisi ya Mufti. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri

atakapofanya majumuisho anipe sababu nzito ili niweze kumpitishia bajeti yake.

Mhe. Spika, vile vile nataka niende kwenye ukurasa wa 67 kiambatanisho namba 8(a) Mhe. Spika, hapa mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa sababu Sheikh wa Baraza Mhe. Sheikh Mohammed Mbwana kaeleza sana hapa. Kwa hivyo Mhe. Spika, hapa mimi naomba nipate maelezo kidogo, ni vigezo gani anavyotumia Mhe. Waziri katika ugawaji wa hii zaka katika Mawilaya. Kwa sababu Mhe hapa inaonesha kuna Wilaya pamewekwa Wilaya wamenufaika vikundi na watu. Sasa katika Wilaya nyengine kuna vikundi 28 lakini katika Wilaya nyengine kuna vikundi 8. Na vile vile kwenye upande wa watu kuna Wilaya nyengine zina watu 8 lakini Wilaya nyengine hakuna kama Micheweni.

Sasa Mhe. Spika, ninamuomba hapa Mhe. Waziri anieleze wanatumia vigezo gani kugawa hiyo zaka, hivyo kweli Micheweni hakuna watu wanaostahiki kupata zaka? Ninamuomba hapa Mhe. Waziri anipe ufafanuzi mzuri.

Vile vile Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 70 na 71 hapa Mhe. Spika, mimi ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada aliyoonesha ya kuwasomesha wafanyakazi wake. Mhe. Spika, ingelikuwa Wizara zote ni kama hii basi ninaamini tungeliendelea mno. Na vile vile Mhe. Spika, nazidi kumpongeza hapa Mhe. Waziri kwa kuangalia *gender,* kwa sababu ikiwa kila Wizara itazingatia *gender* kama Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria basi naamini wanawake, wanaume lazima wajitahidi sana kutufukuza.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba sasa nije katika Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, ama kweli *mkamia maji hayanywi* na binaadamu akipanga yake na Mungu hupanga yake. Siku niliyochangia katika Wizara Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nilizungumzia sana kuhusu watu wanavyohangaishwa katika kupatikana vitambulisho vya Uzanzibari kwa sababu ya vyeti vya kuzaliwa. Na Mhe. Spika, nilisema kwamba nitazuia fungu na nilikuwa nimedhamiria kweli kweli, lakini Mwenyezi Mungu ana rehema alinipa mtihani sikuweza kuingia humu Barazani. Wengine wananiambia ni ndumba lakini Mhe. Spika, kwa vile tatizo moja lililojitokeza ni vyeti vya kuzaliwa, na Wizara ya Katiba na Sheria ndio inayoshughulika na vyeti vya kuzaliwa. Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja anijibu masuala yangu.

Mhe. Spika, wakati watu wote wanapokwenda kutafuta vitambulisho vya uzanzibari wanaambiwa kama vyeti vya kuzaliwa ni feki na havifai. Hata hivyo na changu nilichokipata 1994 leo kimekuwa feki. Na Mhe. Spika, watu

wa vitambulisho walinipa kopi ya saini hizi, wakasema wao saini wanazozitambua ni za watu wawili, Mohammed na Mganja sijui ni Mgonjwa.

Sasa Mhe. Spika, mimi hapa nashangaa, hivyo kweli vyeti vya kuzaliwa saini ni za watu wawili hawa tu? Changu mimi hakina saini ya watu hawa kwa sababu nilikipata kwa Mkuu wa Wilaya. Na hata cha huyo mwanangu kuna saini ya Mkuu wa Wilaya. Sasa leo nashangaa kuambiwa kama vyeti vyote saini ni hizi. Namuomba Mhe. Waziri akija awe na jawabu zuri au nitazuia fungu. Ikiwa saini Mhe. Spika, ni hizi mbili basi atwambie vile vyeti vyengine ilikuwaje Wizara yake itoe vyeti vile? Na ikiwa hizi mbili vile vile atwambie ana mpango gani wa kuvibadilisha vyeti vile viwe halali ili wananchi wasihangaike.

Mhe. Spika, ikiwa Mhe. Waziri atanifahamisha jinsi ya saini ya vyeti vya kuzaliwa vinavyokubalika kama ni hivyo vya watu wawili, kwa sababu hata hao nasikia hawapo tena hasa. Lakini leo ukienda pale unaambiwa saini ni hii na Mhe. Spika, mimi sikujitambulisha kusudi na waliponambia saini ni za watu wawili niliwaambia nitazipata vipi wakanambia sisi tunayo karatasi ambayo tumeletewa na Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Nikawaambia naomba mnisaidie kopi na wakanipa kopi hii.

Kwa hivyo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anipe jawabu nzuri ya kuridhisha ili niipitishe bajeti yake. Ikiwa hakunipa jawabu nzuri nazuia fungu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha kikao hiki kuna tangazo moja dogo lakini muhimu.

Tunaarifiwa kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe ambao bado hamjachukua vitambulisho vyenu yaani vitambulisho vya NIDA kwamba kesho maafisa wa vitambulisho hivyo watafika hapa Ofisini kuanzia saa 3.00 asubuhi ili kuwapatia Waheshimiwa hao Wajumbe ambao hawajachukua vitambulisho vyao wavichukue kutoka hapa hapa Ofisini kwetu.

Lakini pili wale ambao hawakuwahi kupiga picha kwa ajili ya kupatiwa vitambulisho hivyo na hawajasajiliwa kazi hiyo pia itafanyika hiyo hiyo kesho kuanzia hiyo saa 3.00 za asubuhi. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndio taarifa. Ambao hawajachukua vitambulisho wakachukue hapa hapa Ofisini watakuja wenyewe, na wale ambao hawakuwahi kujisajili watapiga picha hapa na hatimaye hatua nyengine kufuata mkondo wake.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni na sasa ninaakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 5/7/2013 siku ya Ijumaa saa 3.00 za asubuhi.

(Saa 1.45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 05/07/2013 saa 3.00 asubuhi)